

*Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu akiongozana na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan tarehe 07 Machi, 2020 wakati wakikagua Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu ambapo ni utekelezaji wa ahadi za Serikali katika kuboresha huduma za Afya nchini.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akimuelekeza kitu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu tarehe 14 Aprili, 2019 wakati walipotembelea moja ya mabanda ya maonyesho wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Taifa wa magonjwa yasiyo ya kuambukizwa katika viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma.*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akiongea na Madaktari na Wataalam wengine wa Afya nchini wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Madaktari Kitaifa tarehe 20 Februari, 2020 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mwalimu Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam ambapo alitoa nafasi za ajira kwa watumishi wa afya 1,000 katika mwendelezo wa jitihada za kuboresha huduma za afya nchini.*

**APRILI, 2020** **DODOMA**

KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA MKUU WA SERIKALI, DODOMA - TANZANIA



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akimpongeza Waziri wa Afya Ummy Mwalimu tarehe 26 Aprili, 2019 mara baada ya kufungua Jengo la Ofisi za Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) Nyanda za Juu Kusini lililopo jijini Mbeya.*



*Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua mradi wa kutokomeza vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto katika maeneo ya masoko tarehe 30 Julai, 2019 Jijini Dodoma.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akimkabidhi Tuzo Maalumu Ofisa Tabibu Wilson Koweli Chota Mganga kutoka kijiji cha Uturo, Mbalali, Mbeya, katika kutambua mchango wake mkubwa katika tasnia ya afya wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Madaktari Kitaifa mwaka 2020 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwalimu Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam tarehe 20 Februari, 2020. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utawala Bora) Mhe. George Mkuchika, Naibu Waziri wa Afya Dkt Faustine Ndugulile, na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. Zainabu Chaula, Mlezi wa Chama cha Madaktari (MAT) Profesa Lawrence Museru na Rais wa MAT Dkt. Elisha Osati.*



*Mwenyekiti Msaidizi Mtandao wa Wazee Tanzania Mzee Abdalla Mohamed Majumba akimkabidhi zawadi ya kiti Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) wakati wa Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Wazee Duniani katika Uwanja wa Nnangwanda Sijaona Mkoani Mtwara tarehe 1 Oktoba, 2019.*

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21

## A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2019/20 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2020/21. Hotuba hii pia imeainisha mafanikio yaliyopatikana ndani ya Sekta za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha miaka mitano (5) ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2020/21.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara na pia kwa dhamira yake, maono yake na uthubutu wake ambao umekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii nchini. Ni dhahiri kuwa katika kipindi cha uongozi wake Watanzania wameshuhudia mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma za afya nchini ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya katika halmashauri na mikoa yote nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi katika hospitali za rufaa za mikoa, kanda na za ngazi ya Taifa. Kipekee, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa dira na miongozo yake ya kuhakikisha nchi yetu inaendelea kusimama imara katika wakati huu ambapo dunia pamoja na nchi yetu inapitia katika kipindi kigumu cha mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu ujulikanao kwa lugha ya kitaalamu *COVID-19.* Ninamuahidi Mheshimiwa Rais kuwa Wizara itaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ili

kuhakikisha tunashinda vita dhidi ya adui wa afya na maendeleo ya watanzania, Corona.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, lishe, mapambano dhidi ya Kifua Kikuu, kuhimiza usawa wa jinsia, uwezeshaji wa wanawake na kuzingatia haki za mtoto katika jamii.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 1 Aprili, 2020 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2020/21.

**5.** ***MheshimiwaSpika,***ninapendakukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yako kwa ufanisi mkubwa katika

kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Naibu Spika **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb)** katika utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano walionipatia ambao umeiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kuwa watanzania wana afya bora ili washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa viwanda, na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Peter Serukamba (Mb)**, na Makamu wake, **Mheshimiwa Juma Nkamia (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha

upatikanaji wa huduma bora za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Ninawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wenu na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi kwa **Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene,** na **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu** kwa kuteuliwa kuwa Mawaziri. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri. Ninawaahidi kuwapa ushirikiano ili tuendelee kuwatumikia wananchi kwa pamoja. Pia, nitumie fursa hii kuwakaribisha na kuwapongeza **Prof. Mabula Daudi Mchembe** kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Idara Kuu ya Afya na **Prof. Abel Makubi** kwa kuteuliwa kuwa Mganga Mkuu wa Serikali. Pamoja na pongezi hizo, napenda kuwahikikishia kuwa mimi pamoja na watumishi wote wa Wizara tunaahidi kuwapatia ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao ili kwa pamoja tushiriki katika kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya nchini.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa familia na wananchi wa jimbo la Newala Vijijini kwa kifo

cha **Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar** aliyefariki Januari 2020. Aidha, natoa pole kwako, familia na waumini wa Kanisa la Mlima wa Moto kwa kifo cha **Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare** aliyefariki tarehe 20 Aprili, 2020. Pia, nitoe pole kwa familia na wananchi wa Mkoa wa Morogoro kwa janga la **ajali ya moto** lililotokea tarehe 10 Oktoba, 2019 na kugharimu maisha ya wananchi 115, wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa **janga la mafuriko** lililotokea mwezi Januari, 2020 na kusababisha uharibifu wa mali na vifo vya watu 21, lakini pia kwa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajali ya kukanyagana iliyotokea tarehe 1 Februari, 2020 na kusababisha vifo vya watu 20. Vilevile, natoa pole kwa watanzania wote, waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali, majanga pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia hususan watoto na maeneo mengine. Napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2019/20, Mpango na makadirio ya mapato na matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2020/21.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/20 FUNGU 52 NA FUNGU 53

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Sera, Mpango Mkakati pamoja na makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya, ustawi na maendeleo ya jamii nchini. Maeneo ya vipaumbele vya Wizara yametokana na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati 2016/17 – 2020/21, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2015-2020, na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's 2030). Aidha, Wizara imezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Afya (2007) na Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2015/16 – 2019/20) pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee (2003); Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); na Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22).

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala wa Serikali na Wadau wa Maendeleo

ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za afya, ustawi na maendeleo ya Jamii katika maeneo yafuatayo:-

i. Kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo ili kuwakinga watoto chini ya miaka mitano dhidi ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo;

ii. Kuendelea kuimarisha hali ya lishe na usafi wa mazingira ili kuwezesha wananchi kujikinga na magonjwa;

iii. Kuendelea kuboresha huduma za Afya ya uzazi, Mama na Mtoto, ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wa chini ya miaka mitano;

iv. Kuendelea na utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuimarisha na kupunguza maambukizi ya UKIMWI, TB na Malaria;

v. Kuendelea kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo, Saratani, Kisukari, Shinikizo la Damu na Magonjwa ya Moyo;

vi. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa Tiba, vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya;

vii. Kuimarisha udahili wa wanafunzi katika vyuo vya Afya, kuboresha mitaala na miundombinu ya kufundishia vyuoni;

viii. Kuboresha Miundombinu na utoaji

huduma katika Hospitali zote za Rufaa za mikoa;

ix. Kuimarisha huduma za Kibingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda nchini;

x. Kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa pamoja na ile ya Kielekitroniki katika Hospitali za Rufaa za Mikoa;

xi. Kukamilisha Mchakato wa maandalizi ya kutunga sheria ya Bima ya Afya itakayomtaka kila mwananchi kuwa na Bima ya Afya ikiwa ni mkakati mahususi wa kufikia lengo la Taifa la Afya kwa wote ifikapo mwaka 2030;

xii. Kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na wadau wengine wote katika utoaji wa huduma za afya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa viwanda vya dawa;

xiii. Kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo;

xiv. Kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake;

xv. Kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto;

xvi. Kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto wakiwemo wale walio katika mazingira hatarishi;

xvii. Kusimamia na kuratibu utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kuleta maendeleo ya jamii;

xviii. Kuwezesha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22); na

xix. Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Taasisi ya Ustawi wa Jamii pamoja na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara.

**Mapato na Matumizi ya Fedha Fungu 52 (Idara Kuu ya Afya)**

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Fungu 52 (Afya) inalo jukumu la kusimamia upatikanaji na utoaji wa huduma za Afya nchini. Wizara hukusanya mapato kutokana na huduma za Tiba zitolewazo na Hospitali zilizo chini yake, tozo za huduma katika Taasisi mbalimbali, ada za Vyuo na uuzaji wa zabuni.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **shilingi 368,536,195,026** ambapo kati ya fedha hizo, **shilingi 21,354,361,184** zilitarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani

katika Makao Makuu ya Wizara na **shilingi 54,567,570,602** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa. Aidha, Mashirika yaliyo chini ya Wizara yalikadiriwa kukusanya **shilingi 292,614,263,240.** Hadi kufikia Machi 2020, jumla ya **shilingi 262,476,691,602.13** zilikuwa zimekusanywa, sawa na **asilimia 71.2** ya lengo kutoka vyanzo vya ndani, hospitali za Rufaa za Mikoa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kusimamia na kuboresha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa kuendelea na utaratibu wa kulipia huduma kupitia Benki, uhamasishaji kuhusu kulipa Maduhuli ya Serikali, Udhibiti wa Makusanyo na kuwaongezea watendaji ari ya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, uboreshwaji wa huduma za bima na kuimarishwa kwa mfumo wa malipo kwa njia ya ki-elektroniki.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara kupitia Fungu 52 iliandaa bajeti ya jumla ya **shilingi 959,152,164,597** ambayo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 415,014,262,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha **shilingi 93,927,890,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 321,086,372,000** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, fedha zilizopitishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni **shilingi 544,137,902,597.** Kati ya fedha hizo **shilingi 270,600,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 273,537,902,597** ni fedha za nje kutoka kwa Wadau wa Maendeleo wanaochangia Sekta ya Afya kupitia Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, TB na Malaria (Global Fund), Benki ya Dunia na wengineo.

**18.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 2020, Wizara ilipokea jumla ya **shilingi 391,732,923,520** ya bajeti iliyoidhinishwa ya **shilingi 959,152,164,597** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya **matumizi ya kawaida** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 ni **shilingi 302,946,918,091** sawa na asilimia 73 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka. Kati ya fedha hizo **shilingi 76,996,172,572** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 82 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Mishahara (Fungu 52) ni **shilingi 225,950,745,518** sawa na asilimia 70 ya bajeti ya mishahara iliyoidhinishwa.

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa miradi ya maendeleo kiasi cha **shilingi 88,786,005,429** kilipokelewa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa **shilingi 27,724,614,149** na fedha za nje ni shilingi **61,061,391,280.** Aidha, Wizara kupitia miradi

msonge ilipokea dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya **shilingi 216,000,000,000,** pia Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) ilinunua dawa zenye thamani ya **shilingi bilioni 125.1.** Aidha, Wizara ilipokea kiasi cha **shilingi bilioni 86.2** kutoka Mfuko wa Afya wa Pamoja ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 68.3** kilipelekwa moja kwa moja OR – TAMISEMI kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za afya katika ngazi msingi.

**Mapato na Matumizi ya Fedha – Fungu 53 (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii)**

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara kupitia **Fungu 53** (Maendeleo ya Jamii), ilitarajia kukusanya kiasi cha **shilingi 4,763,596,000** kutokana na ada za wanafunzi kutoka katika Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli, ada za wanafunzi katika Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara pamoja na ada za mwaka na faini za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hadi kufikia Machi, 2020 Wizara pamoja na Taasisi zake imefanikiwa kukusanya kiasi cha **shilingi 2,574,658,966.61** sawa na **asilimia 54** ya makadirio ya mapato.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara kupitia **(Fungu 53)** iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu matumizi ya **shilingi 31,537,431,013**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 28,777,370,000** sawa na

**asilimia 91** ya bajeti ni kwa ajili ya **Matumizi ya Kawaida** ambapo **shilingi 15,825,478,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo na **shilingi 12,951,892,000** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, Wizara (Fungu 53) iliidhinishiwa **shilingi 2,760,061,013** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **shilingi 1,000,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 1,760,061,013** ni fedha za nje.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2020, Wizara imepokea jumla ya **shilingi 22,364,375,125** sawa na **asilimia 71** ya bajeti kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, Matumizi ya Kawaida ni **shilingi 20,720,199,454** sawa na **asilimia 72** ambapo **shilingi 11,950,678,000** ni Matumizi Mengineyo na **shilingi 8,769,521,454** ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi 1,644,175,671** sawa na **asilimia 60** ya bajeti ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA IDARA KUU YA AFYA (FUNGU 52)

### HUDUMA ZA KINGA

#### Chanjo

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara ilihakikisha chanjo na vifaa vya kutolea chanjo

vinapatikana kulingana na mahitaji ya mikoa yote nchini. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa watoto 2,061,343 wenye umri wa chini ya mwaka mmoja, wajawazito 2,229,015 na wasichana 685,580 wenye umri wa miaka 14 ambao ni walengwa wa huduma za chanjo kwa mwaka 2019/20 wanapata huduma za chanjo kwa wakati.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2020, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Chanjo iliweza kutoa huduma za chanjo kwa kiwango cha asilimia 99 kwa watoto wenye umri wa chini ya mwaka mmoja, ukilinganisha na asilimia 97 iliyofikiwa mwaka 2015/16 wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia madarakani. Vilevile, Wizara ilipanga kutoa Chanjo ya Kuzuia ugonjwa wa Surua na Rubella kwa watoto 7,216,840 na chanjo ya kuzuia kupooza kwa watoto 3,544,433 kupitia kampeni ya kitaifa ya Chanjo iliyofanyika mwezi Oktoba, 2019. Kutokana na kampeni hiyo kuendeshwa kwa ufanisi mkubwa, jumla ya watoto 8,082,861 walipata chanjo ili kuzuia ugonjwa wa surua na rubella, sawa na asilimia 112 ya lengo la watoto 7,216,840 na watoto 4,040,654 sawa na asilimia 114 ya lengo la watoto 3,544,433 walipata chanjo ya kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa nchi nzima. Aidha, Wizara iliendelea na ukarabati wa maghala ya kutunzia chanjo yaliyoko Mabibo, Dar es Salaam, ikiwa ni mkakati wa kuimarisha shughuli za utunzaji na usambazaji wa chanjo nchini.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Serikali ilitoa fedha kiasi cha **shilingi 10,671,805,300** kwa ajili ya ununuzi wa chanjo na vifaa vya kutolea chanjo ambavyo vilikidhi mahitaji ya chanjo nchini kwa asilimia 95. Chanjo zilizonunuliwa ni pamoja na dozi 2,000,000 za BCG kwa ajili ya kuwakinga watoto wachanga na ugonjwa wa Kifua Kikuu; dozi 2,000,000 (bOPV) za kuzuia virusi mbalimbali vinavyosababisha ugonjwa wa kupooza; dozi 2,000,000 (TT) za kuzuia ugonjwa wa Pepopunda kwa mama wajawazito; dozi 3,520,600 (PCV-13) za kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa ya Nimonia na homa ya uti wa mgongo; dozi 4,237,800 (Rota) za kuwakinga watoto dhidi ya ugonjwa wa kuhara, dozi 580,000 za HPV, kwa ajili ya kuwakinga wasichana dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi, dozi 6,232,800 za IPV, ambayo ni chanjo ya sindano ya kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa watoto na dozi 4,048,850 za Penta kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Kupooza, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuimarika kwa huduma za chanjo za watoto nchini, kumechangia kupungua kwa **vifo vya watoto wa umri chini ya mwaka mmoja kutoka vifo 43 kati ya vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 9 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20.** Aidha, **Vifo vya watoto wa umri wa chini ya miaka mitano**

**navyo pia vimepungua kutoka vifo 67 kati ya Vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 11 kati ya vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20.** Hii ni kulingana na takwimu zinazokusanywa na Wizara kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya.

### Afya na Usafi wa Mazingira

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha hali ya afya na usafi wa mazingira, Wizara imeandaa mikakati mbalimbali kama vile Mkakati wa Usafi wa Mazingira wa mwaka 2020 – 2026 na Mkakati wa Kudhibiti Mbu na Wadudu wadhurifu wa mwaka 2019 - 2024 yenye lengo la kuboresha ya hali ya usafi wa mazingira pamoja na udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza nchini. Katika kutekeleza mkakati wa kudhibiti mbu na wadudu wadhurifu, Wizara imenunua jumla ya mashine kubwa 4 za kupuliza dawa *(fogging machine)* kwa ajili ya kudhibiti mbu na wadudu wote wanaoruka, ambapo mashine 2 zilipelekwa Mkoa wa Dar es salaam, mashine 1 ilipelekwa Dodoma na mashine 1 ilipelekwa Tanga na baada ya kumaliza kazi ilipelekwa Mkoa wa Kigoma.

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara iliendelea kutekeleza Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira yenye kaulimbiu isemayo

**USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO** yenye lengo la kuhimiza **ujenzi na matumizi ya vyoo bora** ambapo mikutano ya uhamasishaji jamii imefanyika katika Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na Shinyanga. Kwa ujumla uhamasishaji huu mpaka sasa umefanyika katika mikoa 16 kati ya 26 iliyopo. Lengo ni kuhakikisha mikoa yote 26 inafikiwa ifikapo Juni, 2021. Pia katika kipindi hiki matangazo 6,982 ya Redio na Televisheni yalirushwa.

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, Kupitia utekelezaji wa kampeni hii, idadi ya kaya zilizojenga au kuboresha vyoo ilikuwa 632,854 kati ya lengo la kaya 850,000 kwa mwaka 2019/20 sawa na asilimia 74. Hili ni ongezeko la vyoo bora 2,905,493 ukilinganisha na vyoo bora 1,662,550 vilivyokuwepo mwaka 2015/16 wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia madarakani. Kwa upande wa kunawa mikono kwa maji na sabuni baada ya kutoka chooni, kaya 227,143 kati ya lengo la kaya 850,000 ziliweza kutengeneza sehemu maalum ya kunawia mikono baada ya kutoka chooni. Kutokana na ongezeko hili la vyoo bora na sehemu za kunawa mikono, hali ya usafi wa mazingira kwa ujumla inaonesha kwamba; **kaya zenye vyoo bora nchini hadi kufikia Machi 2020 ni asilimia 62.8 kutoka asilimia 39.4 mwaka 2015/16**, kaya zenye sehemu maalum ya kunawa mikono (maji na sabuni) ni asilimia 22.7 ikilinganishwa

na asilimia 14.4 mwaka 2015/16 na **kaya ambazo hazina vyoo kabisa zimepungua kutoka asilimia 6.1 mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 1.8 Machi 2020**, na juhudi zinaendelea kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo bora na kinatumika. Kuongezeka kwa kaya zenye vyoo bora nchini imechangia katika kupunguza magonjwa yanayosababishwa na kutozingatiwa kwa kanuni za usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa kuhara, homa ya matumbo, kichocho, minyoo ya tumbo, kuhara damu na kipindupindu.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendesha Mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira ambayo hufanyika kila mwaka nchini kwa lengo la kuhamasisha na kuhimiza ushiriki wa jamii katika kuzingatia kanuni za usafi. Mashindano haya yalihusisha Halmashauri 184 za Tanzania Bara. Mshindi wa jumla katika mashindano ya mwaka 2019/20 ilikuwa ni **Halmashauri ya Wilaya ya Njombe** ambayo ilipata tuzo ya mshindi wa kwanza na fedha taslimu shilingi 50,000,000. Mshindi wa pili ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilipata tuzo ya mshindi wa pili na fedha taslimu shilingi 15,000,000 na mshindi wa tatu ilikuwa Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi ambayo ilipata tuzo na zawadi ya fedha taslimu shilingi 5,000,000. *Kupitia Bunge lako tukufu, ninapenda kuendelea kusisitiza na kutoa rai kwa jamii nzima kuzingatia kanuni bora za afya ikiwemo kunawa mikono kwa maji*

*na sabuni baada ya kutoka chooni na kabla ya kula vile vile kujenga na kutumia vyoo bora katika kaya na taasisi.*

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2019/20, Wizara imeendelea kuimarisha mfumo wa udhibiti taka zitokanazo na huduma za afya kwa kuanzisha teknolojia rafiki ya mazingira ambapo taka zinatakaswa kwa njia ya mvuke na baadaye kufanyiwa urejeshaji (Recycling), kwenye viwanda vyetu. Vilevile, Wizara yangu imeanzisha teknolojia ya kuchakata taka aina ya makondo ya nyuma ya kinamama wajawazito (placenta) na kutengeneza nishati rafiki ya mazingira na kutumika kwenye hospitali husika. Teknolojia hizi zimeanza kutekelezwa kwenye hospitali 5 zilizoko Mkoa wa Dar es salaam ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwananyamala, Hospitali ya Palestina-Sinza, na vituo vya Afya vya Buguruni na Mbagala. Serikali inaendelea na taratibu za kuhakikisha teknolojia hii inasambazwa katika Hospitali zote za Rufaa za Mikoa nchini.

**Huduma ya Lishe nchini**

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, Lishe bora ni muhimu kwa uhai, ukuaji na maendeleo ya binadamu kiakili na kimwili na hivyo kuchangia katika kuongeza tija katika uzalishaji mali

kwa kaya na kuimarisha uchumi wa Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe (2016/2017 – 2020/2021). Katika kipindi cha Desemba, 2019 Wizara katika kuimarisha afya na **lishe ya watoto wadogo** imefanikisha zoezi la Kitaifa la utoaji wa matone ya Vitamini A na dawa za kutibu maambukizi ya minyoo kwa watoto walio chini ya miaka mitano; malengo ya zoezi hili yalikuwa ni utoaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto milioni 8.5 na dawa za minyoo kwa watoto milioni 7.5. Zoezi hili lilikamilika kwa kuweza kuwafikia walengwa kwa zaidi ya asilimia 95.

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, gharama za matibabu ya magonjwa yanayosababishwa na ulaji duni na mtindo wa maisha zinaendelea kuongezeka, magonjwa haya ni pamoja na kisukari, baadhi ya saratani, figo, shinikizo la juu la damu na moyo. Magonjwa haya kwa kiwango kikubwa yanachangiwa na ongezeko la tatizo la uzito uliozidi na kiribatumbo. Wizara imeendelea na mikakati ya kutoa elimu kwa umma na miongozo kuhusu njia za kukabiliana na tatizo hili. Mwongozo wa Kitaifa wa Ulaji (National Food Based Dietary Guideline) umeshaandaliwa na kufanyiwa majaribio kupitia maoni ya wadau kutoka katika Mikoa ya Mwanza, Dar es salam na Iringa.  Mwongozo huu utasaidia jamii

kuondokana na tatizo la ulaji usiofaa na hivyo kupunguza athari za gharama za magonjwa sugu yasiyoambukizwa, upotevu wa nguvukazi yenye uwezo wa kuzalisha kwa tija kutokana na wahusika kutumia muda mwingi katika matibabu na upotevu wa maisha katika umri mdogo kwa nguvukazi inayotegemewa na Taifa hivi sasa.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) imeendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watoa huduma za afya kuhusu matibabu sahihi ya utapiamlo katika vituo vya kutolea huduma katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Mafunzo haya yanalenga kupunguza vifo miongoni mwa watoto chini ya miaka mitano kwa kuwawezesha watoa huduma kuwabaini mapema na kuwapatia matibabu stahiki watoto hao. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, mafunzo yalitolewa katika Mikoa tisa (9) ambayo watoa huduma wake walikuwa bado hawajapatiwa mafunzo. Mikoa hiyo ni Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Singida, Tabora, Rukwa, Katavi, Dar es Salaam na Pwani.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kuimarisha Mikakati ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu faida za lishe bora na athari za utapiamlo kwa makundi mbalimbali, kupitia vyombo vya habari na mitandao ya

kijamii. Mathalan, jumla ya vipindi 24 (mada 32) vya redio na runinga vimefanyika katika vituo vya TBC Taifa, TBC FM, Azam TV, UFM, East Africa Redio, Redio One na ETV. Taarifa 71 zimechapishwa katika akaunti za Taasisi za mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram na Twitter) na Makala tano (5) za magazeti ziliandikwa na kuchapishwa kwenye magazeti ya Mwananchi, Mtanzania na Uhuru. Video fupi tatu (3) pamoja na matangazo au taarifa zikihusisha masuala mbalimbali ya lishe ziliandaliwa na kurushwa kwenye mitandao ya kijamii na Tovuti ya Taasisi na kupata wafuatiliaji (followers) wapatao 8,541; Facebook 4,466, Instagram 2,478, Twitter 223 na Tovuti ya Taasisi 1,374. Pia Taasisi imeanzisha blogu "Lishe blog" ili kuweza kuwafikia vijana kwa urahisi zaidi.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe imeendelea kutekeleza mkakati wa kuhamasisha tabia chanya zinazoboresha hali ya lishe ya wajawazito, wanawake wanaonyonyesha, watoto wadogo na wachanga, pamoja na wajibu wa wazazi/walezi, kupitia mafunzo yanayotolewa kwa kutumia Mkoba wa siku 1000. Watoa huduma 487 katika ngazi ya jamii na maafisa ugani 169 kutoka Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Shinyanga, Rukwa, Iringa na Simiyu walinufaika na mafunzo haya. Katika kipindi hiki, tafiti kubwa tatu zimefanyika, ambazo ni: 1) Kutathmini Mtawanyiko wa Wazalishaji

Chumvi nchini pamoja na kiwango cha uzalishaji; ambapo ilibainika kuwa, uzalishaji wa chumvi nchini unafikia tani 330,712 kwa mwaka. Kati ya hizo, tani 189,485 zimeongezwa madini joto; 2) Tathmini ya Ufanisi wa Mawasiliano ya Kubadili Tabia katika Jamii (SBCC) kwa lengo la kuhamasisha unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee nchini; ambapo tathmini hii imefanyika kwa kutumia njia ya "Stable Isotope" na sampuli 1,722 za mate na 120 za vyakula zimekusanywa na uchambuzi wa kimaabara wa sampuli hizo unaendelea; na 3) Utafiti wa Kaya na Viashiria vya Lishe miongoni mwa wanawake walio katika umri wa kuzaa mkoani Morogoro; ambapo sampuli 965 za damu zilichukuliwa ili kubaini viwango vya: wingi wa wekundu wa damu, vitamini A, asidi ya foliki pamoja na vitamini B12. Aidha, sampuli za unga wa mahindi 500 zilikusanywa katika kaya ili kupima viwango vya virutubishi vilivyomo. Matokeo ya tafiti hizi ni muhimu kwa kuwa yatatumika kuboresha afua za lishe nchini.

**37. *Mheshimiwa Spika,*** Maabara ya Chakula na Lishe ya Taasisi pia imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa kuongeza aina na idadi ya viashiria vinavyopimwa kupitia maabara ya Maikrobiolojia. Taasisi imeanza matumizi ya mashine mpya ya kisasa ijulikanayo kama *"High Performance Liquid Chromatography (HPLC)"* ambayo ina uwezo mkubwa wa kupima kwa usahihi viwango vya

virutubishi kwenye damu. Mashine hiyo ina uwezo pia wa kupima virutubishi na molekuli mbalimbali kwenye sampuli za vyakula kwa ajili ya kuangalia usalama na ubora wa lishe. Kwa sasa, Taasisi inajadiliana na wadau ili kuongeza wigo wa kutafiti viwango vya vitamini na madini nchini kupitia utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto (TDHS) utakaofanyika mwishoni wa mwaka 2020.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe imefunga pia mtambo wa kisasa wa "MPAES 4200" ulionunuliwa kupitia uhisani wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA). Mashine hii ina uwezo mkubwa wa kupima kwa usahihi kiwango cha asidi ya foliki katika chakula na damu. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Taasisi ilipokea na kufanya uchunguzi wa sampuli kutoka kwa wadau mbalimbali; ikiwa ni pamoja na baadhi ya nchi barani Afrika, Mashariki ya Kati na Marekani. Maabara ilipokea jumla ya sampuli za chumvi 2,106, mikojo 1,813 na maji 1,208 kutoka nchini Somalia kwa ajili ya kuangalia viwango vya madini joto. Pia imepokea sampuli za chumvi 2,294 na sampuli za mkojo 2,271 kwa ajili ya uchunguzi wa viwango vya madini joto kutoka Angola.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** *kutokana na juhudi na mikakati mbalimbali iliyotekelezwa, hali ya lishe nchini imeendelea kuboreshwa ambapo hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano imepungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2015/ 16 hadi kufikia 31.8 mwaka 2018.*

## Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa **huduma kabla ya Ujauzito**, Wizara kwa kushirikiana na wadau imenunua na kusambaza dawa mbalimbali kwa ajili ya uzazi wa mpango ili kuwezesha wanawake na wanaume kuamua lini, na ni watoto wangapi wanataka kuzaa na kwa kupishanisha muda gani. Dawa za uzazi wa mpango zilizonunuliwa na kusambazwa kupitia Bohari ya Dawa (MSD) ziliweza kukidhi wastani wa asilimia 90 ya mahitaji halisi. Dawa hizo ni pamoja na sindano ya *Depo-provera* dozi 1,483,828, dawa ya vidonge yenye vichocheo viwili vya homoni *Combined oral contraceptives* dozi 2,556,283. Aidha, Vitanzi 251,248, Vipandikizi 229,713, Kondomu za kiume pakiti 58,582,988 Kondomu za kike pakiti 292,884 na dawa za dharura za uzazi wa mpango dozi 53,476, zilinunuliwa na kusambazwa katika vituo mbalimbali nchini. Kwa mujibu wa takwimu zinazokusanywa kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya kupitia mfumo wa DHIS2 zimeonesha kuwepo kwa ongezeko

la akina mama wanaotumia njia ya uzazi wa mpango za kisasa kutoka asilimia 39 mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 44 Machi 2020.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha **huduma za afya wakati wa ujauzito** (Antenatal Care), kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya wajawazito 1,744,668 walihudhuria kliniki wakati wa ujauzito, kati ya wajawazito 1,822,500 waliotegemewa, ambapo **wajawazito 1,343,228 walitimiza mahudhurio manne au zaidi (ANC4+) sawa na asilimia 77 ikilinganishwa na asilimia 41 kwa kipindi kama hicho mwaka 2015/2016 wakati serikali ya awamu ya tano ikiingia madarakani**. Aidha, jumla ya wajawazito 1,512,764 walipatiwa dawa za kukinga Malaria (IPT2+), wajawazito 1,644,834 walipatiwa dawa ya kuzuia upungufu wa damu (FEFOL) na wajawazito 1,452,345 walikunywa dawa za kutibu minyoo ya tumbo (Mebendazole/ Albendazole). Jumla ya wajawazito 1,682,646 walipimwa kipimo cha Malaria na kati yao 105,546 sawa na asilimia 6.3 walikutwa na maambukizi ya Malaria na kuanzishiwa dawa. Kulingana na taarifa zinazokusanywa katika vituo vya kutolea huduma ya afya kupitia mfumo wa DHIS2, **hadi kufikia Machi 2020 asilimia 41 ya wajawazito wote walihudhuria kliniki ndani ya wiki 12 za kwanza tangu kuanza kwa ujauzito wao, ikilinganishwa na asilimia 14 ya wajawazito waliohudhuria kliniki**

**ndani ya wiki 12 za kwanza kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/16**. *Nitumie fursa hii kuwahimiza wanawake wajawazito wote kuhudhuria kliniki kama inavyoshauriwa na wataalam wa afya kwa ajili ya uzazi salama.*

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **huduma wakati wa kujifungua**, Wizara ilinunua dawa za uzazi salama na kuzisambaza kupitia Bohari ya Dawa (MSD). Dawa hizo ni pamoja na sindano ya *Magnesium Sulphate* dozi 104,428 kwa ajili ya matibabu ya kifafa cha mimba, dawa ya vidonge ya *Fefol* kwa ajili ya matibabu ya upungufu wa damu dozi 90,686,287, dawa ya sindano ya *Oxytocin* dozi 1,126,970 ambayo ni sawa na asilimia 91 ya mahitaji halisi. Dawa hizi hutibu tatizo la kutokwa damu kwa wingi bila kukoma kwa kina mama wakati au baada ya kujifungua. Lengo kuu la dawa hizi ni kupunguza vifo vya akinamama vitokanavyo na uzazi pingamizi. Aidha, dawa za watoto chini ya miaka mitano zilizonunuliwa na kusambazwa ni Zinki na ORS zilizofungashwa kwa pamoja dozi 1,331,316 kwa ajili ya matibabu ya kuharisha pamoja na dawa ya kidonge myeyuko ya Amoxicillin dozi 27,272,973 kwa ajili ya matibabu ya nimonia.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi ya msingi ili viweze kutoa huduma bora ikiwa

ni pamoja na huduma za uzazi wa dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni (CEmONC). Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI iliendelea kukamilisha ukarabati wa vituo vya afya 81 na ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya vituo 198. Vituo hivyo, vimewezeshwa kutoa huduma za CEmONC pamoja na huduma zingine za upasuaji na hivyo kuongeza idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Wizara imenunua magari 50 ya kubebea wagonjwa yenye thamani ya **shilingi 6,286,756,436.70** ambayo yamesambazwa kwenye Halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kusaidia wagonjwa na hasa kina mama wajawazito pale watapohitaji kwenda kwenye rufaa ngazi za juu. **Takwimu zinaonesha kuwa idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma imeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 83 mwezi Machi 2020 ikilinganishwa na asilimia 64 kwa kipindi kama hicho mwaka 2015/16**. Ongezeko hili limechangiwa na uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya kutolea huduma uliofanyika katika vituo vya kutolea huduma vya umma, kupitia utekelezaji wa kampeni mbalimbali za uzazi salama ikiwemo Kampeni ya **Jiongeze Tuwavushe Salama** ambayo pia inajikita katika kutoa elimu kwa umma kuhusiana na umuhimu wa mama mjamzito kuhudhuria kliniki angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito, na kuhakikisha anaenda kujifungulia katika kituo cha kutolea huduma za afya. *Napenda kutoa*

*wito kwa wanawake wajawazito wote nchini, wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya ili kupunguza vifo na changamoto za uzazi kwa mama na mtoto.*

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha **huduma kwa mtoto na mtoto mchanga**, Wizara imefanya tathmini na uraghibishaji kwa kamati za Afya ngazi ya hospitali, Halmashauri na Mikoa juu ya uanzishwaji wa vyumba maalum kwa ajili ya matibabu ya watoto wachanga kwenye hospitali 38 za halmashauri katika Mikoa ya Mbeya, Shinyanga, Simiyu, Ruvuma, Dodoma na Pwani. Kutokana na uhamasishaji huo vyumba kwa ajili ya matibabu ya watoto wachanga vimeanzishwa katika hospitali mbalimbali nchini na kufikia vyumba 77 kutoka 32 vilivyokuwepo mwaka 2018/19.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imetoa mafunzo kwa watoa huduma 193 juu ya mwongozo wa kitaifa wa huduma za mtoto mchanga na uanzishwaji wa vyumba maalum vya kuhudumia watoto wachanga (National Guideline for Neonatal Care and Establishment of Neonatal Care Units). Vilevile, jumla ya watoa huduma 553 toka vituo vya kutolea huduma 281 vya Halmashauri za Wilaya 9 za mikoa ya Tabora na Mbeya wamepatiwa mafunzo juu ya Udhibiti wa Magonjwa ya Watoto kwa Uwiano *Integrated Management of Childhood Illness (IMCI)*. Utekelezaji wa afua hizo umechangia

kupunguza **vifo vya watoto wachanga kutoka 25 kati ya vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 7 kati ya vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20** kulingana na takwimu zinazokusanywa na Wizara kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya. Ili kuimarisha ufuatiliaji wa makuzi na maendeleo ya mtoto, Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imechapisha nakala 67,957 za kitabu cha afya ya mtoto wa kike na kiume, tayari vitabu hivyo vimesambazwa kwenye ofisi zote za Kanda za Bohari ya Dawa ili halmashauri ziagize kwa utaratibu wa kawaida.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kupambana na **Saratani ya mlango wa kizazi**, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanzisha vituo vipya kumi (10) kwa ajili ya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi katika Halmashauri 7 za Ilemela, Buchosa, Morogoro vijijini, Kiteto, Njombe vijijini na Sengerema. Aidha, usimamizi shirikishi pamoja na mafunzo elekezi yamefanyika katika vituo 185 vinavyotoa huduma za saratani ya mlango wa kizazi katika Mikoa 13 ambayo ni; Ruvuma, Lindi, Mtwara, Arusha, Manyara, Tanga, Dodoma, Singida, Simiyu, Shinyanga, Mara, Kilimanjaro na Geita. Kupitia zoezi hili, watoa huduma 370 toka katika mikoa tajwa wamejengewa uwezo wa kufanya huduma hizi za uchunguzi kwa ufanisi zaidi. Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya wanawake 217,169 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi. Kati ya wanawake hao, wanawake 8,525 sawa

na asilimia 3.9 walikutwa na mabadiliko ya awali ya Saratani ya Mlango wa kizazi, na kati yao, wanawake 5,671 sawa na asilimia 66.5, walipatiwa matibabu ya tiba mgando kwa kutumia “cryotherapy” na upasuaji mdogo “LEEP”.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utoaji wa **huduma za afya kwa waliopatwa na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto**, Serikali imeanzisha vituo vipya vinne (4) vya kutolea huduma jumuishi kwa waliopatwa na Ukatili wa Kijinsia na Ukatili dhidi ya Watoto katika hospitali za Rufaa za mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tabora na Mwananyamala na kufanya vituo hivyo kufikia 13 ukilinganisha na vituo 9 vilivyokuwepo mwaka 2015/16. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, jumla ya wahanga 134,415 walihudumiwa katika vituo 13 ukilinganisha na wahanga 96,500 waliohudumiwa katika vituo 9 vinavyotoa huduma jumuishi ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto mwaka 2015/16.

**Udhibiti wa VVU/UKIMWI**

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, Huduma za **Ushauri Nasaha na Upimaji wa VVU** zimeendelea kutolewa kwa wananchi wote bila malipo mijini na vijijini. Idadi ya watu wanaopima afya zao ili kutambua hali zao za maambukizi ya VVU

imekuwa ikiongezeka kila mwaka kutoka jumla ya watu 6,800,000 mwaka 2015 hadi kufikia 12,392,268 Desemba 2019, sawa na ongezeko la asilimia 82.2. Ongezeko hili limetokana na mikakati iliyowekwa na Wizara ya kuhakikisha watu wengi zaidi hasa wanaume wanajitokeza kupima VVU, kutambua hali zao na kupata huduma stahiki. Mikakati hiyo inajumuisha pamoja na kuwashauri watu wazima wanaogundulika na maambukizi mapya ya VVU, kuwaleta wapenzi/wenzi, watoto wao na washirika wa dawa za kujidunga ili nao wapatiwe huduma ya kupimwa VVU. Aidha, vituo vya kutolea huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU vimeongezeka kutoka vituo 5,600 mwaka 2015 hadi vituo 6,397 Desemba 2019.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha huduma za utoaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI zinakuwa karibu zaidi na wananchi na pia kutanua wigo wa huduma hiyo mijini na vijijini ili kupunguza gharama za nauli na kuondoa msongamano katika vituo vya kutolea huduma hiyo. Hadi kufikia Machi 2020, vituo vinavyotoa dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI vilikuwa vimefikia vituo 6,529 ikilinganishwa na vituo 5,555 vilivyokuwa vinatoa huduma hiyo mwaka 2015/16.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza Kampeni, inayojulikana kama **Furaha Yangu, Pima, Jitambue, Ishi** inayolenga kuongeza idadi ya watu wanaopima VVU na kutambua hali zao ili kuanza dawa za ARV mapema. Kampeni hii imeongeza hamasa kwa Watanzania hasa wanaume kujitokeza kupima VVU na hivyo kuchangia katika mafanikio yaliyofikiwa ya Upimaji wa VVU nchini ambapo idadi ya **watu wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU nchini na wanaotambua hali zao (lengo la 90 ya kwanza) imeongezeka kutoka watu 816,408 ambayo ni sawa na asilimia 58.3 ya wananchi 1,400,000 waliokadiriwa kuishi na VVU mwaka 2015 hadi kufikia watu 1,289,125 Desemba 2019 ambayo ni sawa na asilimia 80.6 ya watu 1,600,000** wanaokadiriwa kuwa na VVU nchini. Ili kuongeza kasi ya watu kupima VVU na kutambua hali zao, mwezi Novemba 2019 Bunge lilipitisha mapendekezo ya Serikali ya kufanya mabadiliko ya Sheria ya UKIMWI Sura ya 431 ambayo imeongeza kifungu kinachoruhusu wananchi kujipima VVU (Self testing), na kuruhusu umri wa kupima VVU bila hitaji la ridhaa ya mzazi au mlezi kutoka miaka 18 hadi 15 kuridhiwa na Bunge na kusainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba 2019. Kwa sasa, Wizara ipo katika hatua za mwisho za mchakato wa kutunga kanuni za sheria hii kwa ajili ya utekelezaji wake.

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutimiza lengo la kuhakikisha watu waliopimwa na kutambua hali zao za VVU wanaunganishwa kwenye huduma na wanaanzishiwa ARV **(lengo la 90 ya pili) takwimu zinaonyesha hadi kufikia Desemba 2019, kati ya watu 1,289,125 waliotambua hali zao za VVU watu 1,271,666 sawa na asilimia 98.6 walianza kutumia dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI yaani ARV, hivyo kuvuka lengo la 90 ya pili.** Hili ni ongezeko la asilimia 58.2 ikilinganishwa na watu 740,745 walioanzishiwa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI mwaka 2015. Ongezeko hili la watu kutumia dawa limesababishwa na kuanzishwa kwa utaratibu wa kuanza kutumia dawa mara mgonjwa anapothibika kuwa ana maambukizi ya VVU.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, katika lengo la kutimiza **tisini ya tatu** ambalo ni kuhakikisha kuwa asilimia 90 ya wanaotumia ARV's wamefanikiwa kupunguza wingi wa VVU mwilini, takwimu zinaonyesha kwamba mpaka kufikia Desemba, 2019 watu 786,485 sawa na asilimia 85 ya watu 922,980 wanaostahili kupata huduma hiyo, na kati yao, **asilimia 91 wamefanikiwa kupunguza wingi wa VVU mwilini.** Mafanikio haya ni makubwa ukilinganisha na idadi ya watu 42,236 tu waliopima wingi wa virusi vya VVU na kati

ya hao ni watu 35,087 sawa na asilimia 83 tu ndio walikuwa wamefanikiwa kupunguza wingi wa VVU mwilini mwaka 2015. Watu hawa watapunguza uwezekano wa kuwaambukiza VVU wenza wao, ila ikumbukwe kwamba hali hii si ya kudumu iwapo hawatazingatia matumizi sahihi na endelevu ya ARV.

**53.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Huduma za kuzuia **maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT**), zimeendelea kutolewa, ambapo kwa mwaka 2019, jumla ya akina mama wajawazito 2,232,500 sawa na asilimia 98 ya akina mama 2,272,866 walipatiwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU. Kati yao akina mama 34,764 sawa na asilimia 1.6 waligundulika kuwa wanaishi na VVU. Akina mama 82,408 sawa na asilimia 91 ya akina mama wenye maambukizi ya VVU walipatiwa dawa (ARV) kwa ajili ya kufubaza virusi vya UKIMWI. Aidha, jumla ya Watoto 44,711 sawa na asilimia 52 walipata kipimo cha awali cha utambuzi wa maambukizi ya VVU ambapo watoto 1,128 sawa na asilimia 2.5 walikutwa na maambukizi ya VVU. Kiwango hicho cha maambukizi kinaashiria Tanzania ipo katika kasi sawia ya kuweza kufikia maambukizi chini ya asilimia 2 ifikapo mwaka 2021 kama inavyoainishwa katika mpango mkakati wa kutokomeza kabisa maambukizi ya VVU kwa watoto.

## Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanikiwa kuongeza kasi ya ugunduzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu na kufikia lengo kwa asilimia 98.3 kwa kugundua wagonjwa 61,583 kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 ikilinganishwa na wagonjwa 50,130 waliogundulika katika kipindi kama hiki mwaka 2015/16. **Hivyo kiwango cha ugunduzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu kimepanda hadi kufikia asilimia 53 Machi mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 40 mwaka 2016**. Wagonjwa waliogundulika kuwa na Kifua Kikuu wamepatiwa matibabu ambapo asilimia 91 ya wagojwa waliopewa matibabu wamepona Kifua kikuu kabisa na kuendelea na shughuli zao za ujenzi wa Taifa. **Vifo vitokanavyo na ugonjwa wa Kifua Kikuu vimepungua kutoka vifo 30,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia 22,000 mwaka 2020**.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Kifua Kikuu Sugu, takwimu zinaonesha kuwa jumla ya wagonjwa 449 waligundulika kuwa na Kifua Kikuu Sugu na walianzishiwa matibabu. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2019/20, maambukizi mapya ya TB yamepungua na kufikia watu 253 kati ya watu 100,000 ikilinganishwa na maambukizi 306 kati ya watu 100,000 mwaka 2015/16 na hivyo kufanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 7 tu duniani ambazo zipo katika mwelekeo sahihi wa kufikia

malengo ya Mpango Mkakati wa Shirika la Afya Duniani ya kutokomeza TB ifikapo Desemba 2020.

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuboresha huduma za uchunguzi wa TB, Wizara imeongeza mashine za kisasa za kupima TB (GeneXpert) kutoka mashine 65 mwaka 2015 hadi mashine 239 Machi, 2020. Kati ya mashine hizi ambazo zinazotoa majibu ya TB ndani ya masaa 2 kulinganisha na hadubini zinazotoa majibu baada ya masaa 24, mashine 55 zina uwezo wa kupima wingi wa VVU na hali ya maambukizi kwa watoto wachanga. Hadi sasa, jumla ya Halmashauri 113 kati ya 184 sawa na asilimia 62 zimeshapatiwa mashine hizo. Halmashauri 71 zilizosalia zinategemewa kupatiwa mashine hizi kwa mwaka 2020/21. Pia, Wizara inaendelea kufanya ununuzi wa hadubini 941 ambazo 552 tayari zimesambazwa kwenye Mikoa 15.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea na ugatuzi wa huduma za Kifua Kikuu Sugu, Wizara imeendelea na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma kwa kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya 284 na kuongeza vituo 255 ili viwe na uwezo wa kutoa huduma hiyo. Hadi Machi 2020, jumla ya vituo 1,201 viliwezeshwa kutoa huduma za Kifua Kikuu Sugu ikilinganishwa na vituo 662 vilivyokuwepo mwaka 2016/17. Aidha, katika juhudi za kutanua wigo wa uibuaji wa wagonjwa wa Kifua

Kikuu, Wizara ilifanikiwa kuongeza maduka ya dawa muhimu yenye uwezo wa kuwaibua wahisiwa wa Kifua kikuu na kuwapatia rufaa kwenda kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa uchunguzi zaidi kutoka maduka 300 katika mikoa 10 mwaka 2017 hadi maduka 870 katika mikoa 19 Machi 2020.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **huduma za Ukoma**, kaya 131 zimetembelewa (contact tracing) na kufanya uchunguzi wa Ukoma katika wilaya za Muheza, Mkinga, Chato, Ifakara, Kilombero, Nanyumbu na Liwale. Zoezi hili limegundua wagonjwa wapya 45 ambao pia wameanzishiwa matibabu ya Ukoma. Hadi kufikia Machi, 2020 idadi ya wagonjwa waliokuwa wamegunduliwa ilikuwa 1,151 nchi nzima ikilinganishwa na wagonjwa 2,297 kwa kipindi kama hiki cha mwaka 2015/16. Vilevile, idadi ya watoto wanaougua Ukoma imepungua kwa asilimia 54, kutoka watoto 98 mwaka 2015/16, hadi kufikia watoto 53 Desemba, 2019.

**Udhibiti wa Malaria**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kuhakikisha kuwa, dawa za kutibu malaria na vitendanishi zinapatikana wakati wote kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya. Kwa kipindi cha Mwezi Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara imenunua na kusambaza

Dawa Mseto (ALu) dozi 8,228,910, Sindano *Artesunate* vichupa 1,624,985 sawa na asilimia 100 ya mahitaji kwa ajili ya Malaria kali (severe Malaria) na Vitendanishi 32,220,900 ambazo zimewafikia wananchi kupitia vituo vya kutolea huduma za Afya.

**60. *Mheshimiwa Spika***, asilimia ya wagonjwa waliothibitishwa kuwa na vimelea vya malaria kwa kutumia vipimo vya mRDT imeongezeka hadi kufikia asilimia 98 mwezi Machi 2020 ikilinganishwa na asilimia 95 mwaka 2015/16. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji wa jamii ili kutambua umuhimu wa kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kufanyiwa vipimo na kuthibitisha uwepo wa vimelea vya Malaria kabla ya kutumia dawa kwa kutumia kaulimbiu ya "Sio kila homa ni Malaria". **Maambukizi ya Malaria yamepungua kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 7.3 Machi 2020. Aidha, vifo vitokanavyo na malaria vimepungua kutoka vifo 6,311 mwaka 2015 hadi kufikia vifo 2,079 Machi 2020**.

**61. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 Wizara imeendelea kuwakinga wananchi dhidi ya maambukizi ya malaria, ambapo iligawa jumla ya vyandarua 1,951,689 vyenye dawa bila malipo kwa wajawazito katika hudhurio la kwanza na watoto wenye umri wa miezi 9 waliohudhuria kwenye

vituo vya kutolea huduma kwa ajili ya kupatiwa chanjo ya kwanza ya Surua Rubella (MR1). Vilevile jumla ya vyandarua 1,261,059 vimegawiwa kwenye mikoa 4 ya Kigoma, Kagera, Geita na Mwanza kupitia shule za msingi ambapo lengo lilikuwa ni kusambaza vyandarua 6,750,381. Maandalizi ya kampeni ya ugawaji vyandarua katika kaya (Mass Replacement Campaign-MRC) yanaendelea kufanyika, ambapo uhamasishaji na mafunzo kwa watekelezaji ngazi ya mikoa na Halmashauri yameendelea kufanyika kuanzia mwezi Januari 2020. Jumla ya vyandarua 7,097,565 vitagawiwa katika Mikoa 10 ya; Mbeya, Njombe, Rukwa, Songwe, Dodoma, Singida, Iringa, Tanga, Kilimanjaro na Manyara katika Halmashauri zipatazo 50.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuangamiza mbu wakiwa katika hatua ya viluwiluwi kwenye mazalia, Wizara katika kipindi cha mwaka 2019/20 imenunua viuadudu (biolarvicides) lita 96,000 ikiilinganishwa na lita 60,000 zilizonunuliwa mwaka 2018/19, na kuzisambaza kwenye Halmashauri za Mikoa 12 ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Kagera, Geita, Kigoma, Tanga, Tabora, Ruvuma, Morogoro, Dodoma na Mwanza. Utekelezaji wa Afua hii, sio tu kuwa unadhibiti mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria pekee, bali pia magonjwa mengine ikiwa ni pamoja na Dengue, Zika, Matende, Homa ya Manjano (Yellow Fever), Chikungunya na Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley). Pia,

kupitia ufuatiliaji wa mbu wapevu, jumla ya sampuli 954 za mbu zilikusanywa kutoka katika Halmashauri 57 na kuwasilishwa katika maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kanda ya Muheza-Tanga kwa uchunguzi zaidi. Matokeo ya utafiti huo yanategemea kutolewa mwezi Oktoba, 2020.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetekeleza zoezi la upuliziaji wa viuatilifu-ukoko majumbani (Indoor Residual Spray) katika Halmashauri za Mikoa 4 yenye kiwango kikubwa cha maambukizi ya malaria nchini, ambayo ni; Kagera, Mwanza, Geita na Kigoma, ikijumuisha kambi 3 za wakimbizi za Nduta, Mtembeli na Nyarugusu zilizopo Mkoani Kigoma. Kati ya Oktoba, 2019 hadi Machi 2020, upuliziaji wa dawa umefanyika katika Halmashauri 4 za Kasulu, Kakonko, Kibondo, na Biharamulo ambapo jumla ya nyumba 331,044 kati ya nyumba 336,806 sawa na asilimia 98.3 zimepuliziwa na wananchi 1,346,219 wamekingwa dhidi ya maambukizi ya malaria katika maeneo hayo. Awamu ya pili upuliziaji wa viuatilifu-ukoko unatarajiwa kufanyika mwezi Mei 2020, katika Halmashauri 2 zilizobaki za Ukerewe na Bukombe ili kukamilisha idadi ya Halmashauri 6 zilizokusudiwa kufikiwa.

**64.** ***Mheshimiwa spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza kampeni ya **Ziro Malaria Inaanza na Mimi** inayohusisha Bara zima la Afrika na

inasimamiwa na Taasisi ya Roll Back Malaria Partnership to End Malaria pamoja na Umoja wa Africa (African Union). Kampeni hii ilianzishwa ili kusaidia nchi zenye maambukizi makubwa ya Malaria barani Afrika kufikia malengo ya kutokomeza ugonjwa wa malaria kabisa ifikapo mwaka 2030 kulingana na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya mwaka 2030. Kampeni hii ilizinduliwa rasmi kitaifa tarehe 8 Novemba 2019, Kibaha Mkoani Pwani wakati wa Siku ya Malaria Kwa Nchi za Jumuiya ya SADC. Kampeni hii inatekelezwa kwa kujumuishwa katika shughuli zote za uhamasishaji jamii kupambana na malaria zinazoendelea hapa nchini. Aidha, uzinduzi wa kampeni hii umefanyika katika mikoa 5 ya Mtwara, Lindi, Tabora, Morogoro na Ruvuma. Kampeni hii itaendelea kuzinduliwa kimkoa katika mikoa mingine iliyobaki ili kuweza kuendelea kuhamasisha zaidi juu ya mapambano dhidi ya malaria hapa nchini.

## Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utayari wa kukabiliana na tishio la mlipuko wa Ugonjwa wa **Ebola; Ugonjwa ya Homa Kali ya Mapafu (COVID-19);** na **Homa ya Manjano** Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kudhibiti magonjwa haya. Katika kudhibiti kuingia kwa ugonjwa wa **Ebola** nchini, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za kinga

katika maeneo ya mipakani kwa kuwajengea wataalam uwezo wa kudhibiti na kukabiliana na ugonjwa huu endapo utaingia nchini. Jumla ya wataalam 204 walijengewa uwezo wa utayari wa kukabiliana na ugonjwa wa Ebola ambapo wadau 42 kutoka katika sekta ya usafiri na usalama walihamasishwa kuhusu udhibiti wa ugonjwa huo kupitia sekta ya usafiri. Vilevile, Wizara imewezesha mipaka 18 kuandaa Mipango ya Dharura yaani *Contingency Plans* na kutoa mafunzo ya utayari kwa watumishi 150 waliopo mipakani pamoja na watumishi zaidi ya 200 wa sekta zingine zilizopo mipakani kama vile Uhamiaji, Polisi, Forodha na Usalama wa Taifa. Hatua zingine zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kufanya uhamasishaji kwa jamii kuhusu ugonjwa huu na namna ya kukabiliana nao. Uhamasishaji huo umefanyika zaidi katika maeneo ya mipakani hususan mikoa yote yenye mwingiliano na nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC).

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Desemba 2019, kulitokea ugonjwa wa mlipuko ulioanzia katika Jimbo la Wuhan nchini China unaojulikana kama **Corona Virus Disease 2019 (COVID-19)** kwa lugha rahisi Corona**.** Ugonjwa huu hauna tiba wala kinga, na unasababishwa na kirusi kipya aina ya *Novel Corona* ambacho huathiri zaidi mfumo wa upumuaji wa muathirika na huweza hata

kusababisha kifo kama mgonjwa hatapatiwa uangalizi wa uhakika. Shirika la Afya Duniani liliutangaza rasmi ugonjwa huu wa COVID-19 kuwa ni Dharura ya Jamii Kimataifa (*Public Health Emergency of International Concern)* tarehe 30 Januari 2020 na tarehe 11 Machi, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza ugonjwa huu kuwa ni Janga la Dunia *(Pandemic)*. Takwimu zinaonesha kuwa kuanzia ugonjwa huu ulipoanza katikati ya Desemba, 2019 hadi tarehe 24 Aprili 2020 jumla ya nchi 210 duniani zimeripoti kuwa na wagonjwa ambapo watu 2,250,709 wameugua, watu 572,105 wamepona na kati yao, watu 154,256 wamefariki dunia. Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizoathirika na janga hilo, ambapo hadi tarehe 24 Aprili, 2020 jumla ya **wagonjwa 284** walithibitika kuwa na maambukizi ya COVID-19 nchini. Kati yao waliopona ni **48** na waliofariki ni ni 10, wagonjwa wengine wote waliobakia (226) isipokuwa 7 hali zao ni nzuri na wanaendelea na matibabu katika sehemu walizotengwa. *Napenda kuwashukuru watumishi wote wa Afya nchini hususani walio mstari wa mbele kwa kujitoa na kufanya kazi bila kuchoka katika kukabiliana na ugonjwa huu tokea ulipoingia nchini. Serikali itaendelea kutambua na kuthamini mchango wao katika kuhudumia wagonjwa na kuokoa maisha. Nasi tutaendelea kutimiza wajibu wetu kwa kuhakikisha uwepo wa vifaa kinga na vifaa tiba katika utoaji wa huduma kwa wananchi.*

**67. *Mheshimiwa Spika***, katika kudhibiti na kuhakikisha kuwa ugonjwa huu hauathiri watu wengi zaidi, Serikali imeendelea kuchukua

hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha ufuatiliaji wa wasafiri wanaoingia nchini kupitia viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu ili kuweza kubaini wasafiri wanaoonyesha dalili za ugonjwa. Hadi tarehe 24 Aprili, 2020 jumla ya wasafiri 2,001,670 wamepimwa joto la mwili (thermol screening) ili kubaini kama wana homa ikiwa ni dalili za awali za ugonjwa huu na wasafiri 3,064 wamewekwa karantini katika maeneo mbalimbali hapa nchini ambapo wasafiri 2,101 wamekamilisha muda wa siku 14 na kubainika kuwa hawana maambukizi ya COVID-19 na hivyo kuruhusiwa kuendelea na shughuli zao za kawaida. Katika kuhakikisha kuwa wasafiri wote wanaoingia nchini wanapimwa joto la mwili, Serikali imenunua jumla ya vipima joto 324 (vya mkono 307 na vya kupima watu wengi kwa mpigo 17) ambavyo vimefungwa na vinatumika katika maeneo ya mipakani ikiwemo viwanja vya ndege na bandari. Vilevile, watumishi 120 wameajiriwa kwa muda ili kuimarisha ufuatiliaji wa wasafiri wanaoingia nchini kupitia maeneo ya mipakani. Serikali imeandaa utaratibu maalum wa kuwaweka chini ya uangalizi wa siku 14 wasafiri wote wanaoingia nchini kwa gharama zao.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeimarisha uwezo wa kupima sampuli kwa watu wote wanaohisiwa kuwa na viashiria au dalili za ugonjwa huu, ambapo kwa sasa Maabara yetu ya Taifa ya Afya ya Jamii imejengewa uwezo kwa

kupatiwa mahitaji yote muhimu katika kupima virusi vinavyosababisha ugonjwa huu, ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi na uungaji wa vifaa katika jengo jipya.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa huduma za matibabu kwa wagonjwa, Serikali inaendelea kuwapatia matibabu wagonjwa wa COVID-19 ambapo kwa upande wa Dar es salaam matibabu yanatolewa katika Kituo cha Magonjwa hatari ya kuambukiza Temeke, Kisoka-Mlonganzila na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana. Aidha Serikali inajenga kituo cha kisasa cha wagonjwa wa Magonjwa hatari ya kuambukiza eneo la Kisoka-Mloganzila, Dar es Salaam. Vilevile, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara wameelekezwa kuandaa maeneo maalum kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa katika mikoa endapo watajitokeza katika maeneo yao. Hadi tarehe 24 April, 2020, jumla ya mikoa 17 ina vituo vya matibabu ya wagonjwa wa corona.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa sekta ya afya ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na magonjwa ya milipuko na majanga ikiwemo jinsi ya kutoa matibabu, kuchukua sampuli, uelimishaji na kuzingatia kanuni za afya. Hadi sasa wataalam wa afya 2,113 wamepatiwa mafunzo ya kukabiliana na ugonjwa wa corona kutoka mikoa 11 ya Dar es

salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Rukwa, Songwe, Tabora, Dodoma, Tanga, Mbeya na Pwani, mafunzo yanaendelea kwa mikoa iliyobakia. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya namna ya kujikinga na kutambua dalili za ugonjwa huu. Elimu hiyo imeendelea kutolewa kwa njia ya vyombo vya habari (magazeti, redio na runinga), mitandao ya kijamii, shuleni, vyuoni, nyumba za ibada na vyombo vya usafiri.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi kwa kuzingatia maelekezo mbalimbali tunayowapatia ikiwemo kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima. Tunaendelea kuwakumbusha watanzania kuwa ugonjwa huu ni wa hatari na hauna kinga wala tiba, na njia pekee ya kujikinga na ugonjwa huu ni kufuata maelekezo ambayo yamekuwa yakitolewa na wataalam wa afya kuhusu namna bora za kujikinga na ugonjwa huu. Nitumie fursa hii pia kumshukuru Mhe Rais, kwa maelekezo yake ya mara kwa mara katika kudhibiti ugonjwa huu nchini. Kipekee ninamshukuru Mhe. Waziri Mkuu kwa ushirikiano mzuri alionipatia katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya janga hili la Corona. Aidha, ninawashukuru Wadau wa ndani na nje ya nchi wanaoendelea kuunga mkono jitihada za Serikali za kudhibiti ugonjwa huu nchini**.**

**72.** ***Mheshimiwa Spika***, **Ugonjwa wa Homa ya Manjano** ni kati ya magonjwa ya kuambukiza yenye hatari ya kusambaa Kimataifa kupitia maeneo ya mipakani, Wizara imeendelea kudhibiti kuingia kwa ugonjwa huu nchini kwa kufanya ukaguzi wa wasafiri wanaotoka katika nchi zenye maambukizi ya Homa ya Manjano. Katika kipindi hiki, Wizara ilipanga kuwakagua wasafiri 20,800 wanaosafiri kwenye nchi zenye maambukizi na Wizara yangu imeweza kuwakagua wasafiri 32,000. Aidha, Wizara imeimarisha huduma ya chanjo kwa kuongeza vituo kutoka 19 hadi 25. Vituo vilivyoongezeka vipo katika mipaka ya Mabamba, Manyovu, Murongo, Kirando, Bandari ya Mtwara na Hospitali ya Rufaa ya Dodoma. Vilevile, Serikali imenunua jumla ya dozi 18,500 za chanjo ya homa ya Manjano na kuzisambazwa katika vituo vyote 25 vya kutolea chanjo hiyo.

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, njia mojawapo ya kupambana na magonjwa haya ya milipuko ni kuhakikisha kuwa taarifa sahihi kuhusiana na mlipuko husika zinapatikana kwa wakati na kutoka katika vyanzo husika. Katika kuboresha utoaji wa taarifa, Wizara imeboresha mifumo ya utoaji wa taarifa mapema za magonjwa ya milipuko kwa njia ya kielektoniki (e-IDSR) kuanzia ngazi ya vituo vya kutolea huduma. Hadi kufikia Machi 2020, mikoa yote 26 ya Tanzania bara imeanza kutoa taarifa kwa njia ya kielektroniki.

## Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, Wizara imehakikisha kuwa wataalam, dawa, vifaa na vifaa tiba vya kutosha vinapelekwa katika maeneo ambayo yameonekana yanasumbuliwa zaidi na magonjwa hayo, baadhi ya magonjwa hayo ni pamoja na **Usubi, matende na mabusha, kichocho** na **trakoma**. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) ilisambaza dawa aina ya *Ivermectin (Mectizan)* vidonge 26,620,500 na *Albendazole* vidonge 7,817,400 vya kudhibiti na kukinga magonjwa ya Usubi, Matende na Mabusha. Aidha, Wizara ilisambaza dawa aina ya *Praziquantel* vidonge 7,966,000 kudhibiti na kukinga ugonjwa wa Kichocho; *Zithromax* vidonge 1,944,500 na Zithromax ya maji, chupa 16,088 kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa wa Trakoma katika halmashauri za Ngorongoro, Longido, Kiteto na Simanjiro.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020, Wizara ilitoa Kingatiba kwa ugonjwa wa Usubi (Onchocerciasis) kwa watu wapatao 5,297,491 kati ya walengwa 6,476,193 sawa na asilimia 82 katika Halmashauri 28, na watu wapatao 1,161,582 kati ya walengwa 1,414,264 sawa na asilimia 82 kwa ugonjwa wa Matende na Mabusha katika Halmashauri 9. Aidha, kwa ugonjwa wa Trakoma, Wizara ilitoa kingatiba kwa watu wapatao 794,564 kati ya watu 888,213 sawa na asilimia 89 katika Halmashauri nne (4).

**76. *Mheshimiwa spika,*** Wizara ilifanya tathmini ya kwanza ya kuangalia kiwango cha maambukizi kwa ugonjwa wa Matende na Mabusha katika Halmashauri tisa (9) za Mikoa ya Lindi, Morogoro na Tanga. Halmashauri zote tisa (9); Lindi Mjini, Nachingwea, Ruangwa, Kilosa, Morogoro Vijijini, Morogoro Mjini, Mvomero, Mkinga na Tanga Jiji zilikidhi vigezo vya zoezi la kusitisha utoaji wa Kingatiba. Aidha, Wizara ilifanya tathmini ya pili ya kuangalia kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa Matende na Mabusha katika Halmashauri 20 za Mikoa ya Morogoro, Manyara na Tabora ambazo zilishasitisha utoaji wa Kingatiba. Kufuatia tathmini hiyo, Halmashauri zote 20 zilibainika kutokuwa na wagonjwa. Tathmini nyingine ilifanyika kwa ugonjwa wa Trakoma katika Halmashauri 10. Halmashauri 8 zilikidhi vigezo vya kutoendelea na zoezi la Kingatiba. Halmashauri 2 ambazo hazikukidhi vigezo, ni Chamwino na Kongwa ambazo zitaendelea na zoezi la utoaji wa kingatiba kwa mwaka mmoja.

### Elimu ya Afya kwa Umma

**77. *Mheshimiwa Spika*** Wizara imeendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya lishe, huduma za mama na mtoto, afya ya mazingira, namna ya kujikinga na majanga, magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza. Vilevile, Wizara imetangaza *"toll free number"* ambazo ni: 0800110124 na 199 kwa lengo la kuhamasisha jamii kupiga

simu pale wanapoona mtu mwenye dalili za magonjwa ya kuambukiza au kifo kinachohisiwa kusababishwa na ugonjwa wa kuambukiza ikiwa ni pamoja na COVID-19. Kupitia namba hizo, Serikali imeendelea kupokea maswali mbalimbali kutoka kwa wananchi ambao wamekuwa wakipatiwa ufafanuzi na ushauri ikiwa ni sehemu ya utoaji wa elimu ya afya kwa umma.

**78. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara iliandaa na kusambaza vielelezo vya kutoa elimu kwa jamiii kama ifuatavyo: Mabango 1,433,320; stika 3,800; fulana 4,800; kofia 4,000; vipeperushi 2,910,800; matangazo 328 ya Runinga na matangazo 1,760 ya Redio. Aidha, Wizara iliratibu vipindi 262 vya Redio, Vipindi vya Runinga 124 na kurusha kupitia mitandao ya kijamii vipeperushi 287, jumbe fupi 221 zenye picha na sauti. Pia, kusambaza *flash* 4,720 zenye jumbe mbalimbali za kuelimisha jamii kuhusu masuala ya afya.

## HUDUMA ZA TIBA

### Usimamizi wa Vituo vya kutolea huduma za Afya

**79. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za afya nchini zinazotolewa kupitia vituo vya kutolea

huduma vya Serikali, binafsi na mashirika ya dini. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka kufikia 8,446 ikilinganishwa na vituo 7,113 mwaka 2015/16 wakati Serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani. Kati ya vituo hivyo Serikali inamiliki vituo 5,844 sawa na asilimia 69.2, mashirika ya dini vituo 1,521 na watu binafsi 1,081. Kati ya vituo 8,446 vilivyopo nchini, hospitali ni 294, vituo vya afya ni 910 na zahanati ni 7,242.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kupitia Bodi ya Ushauri wa Hospitali za Watu Binafsi imesajili Kampuni/Shirika na vituo vya kutolea huduma katika ngazi mbalimbali ambavyo ni; Kampuni/ Taasisi/ Shirika 45, Hospitali ngazi ya Wilaya 12, Hospitali ngazi ya Mkoa 2, Hospitali za Kibingwa 1, Vituo vya Afya 7, Zahanati 89, Polyclinic 57, na kliniki za kawaida 47 na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa katika kipindi hiki kufika **215.**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Ushauri wa Hospitali za Watu Binafsi na kitengo cha Tehama, imetengeneza Mfumo wa Usajili wa Kielektroniki, ambao utatumiwa na wamiliki wa Hospitali za Watu Binafsi na Umma kutuma maombi yao ya usajili na kulipia ada mbalimbali kupitia

mfumo huu ambao umeunganishwa na Mfumo wa GePG. Kwa kufanya hivi Mfumo utarahisisha upatikanaji wa haraka wa huduma ya usajili wa vituo na kupokea malipo mbalimbali ili kupunguza gharama za usafiri kufuata huduma hii Dodoma na kuepuka usumbufu usio wa lazima.

### Upatikanaji wa Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba na Vitendanishi

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma unakuwa wa kuridhisha. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) hununua, hutunza na kusambaza zaidi ya aina 2,545 za dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Kati ya hizo, dawa aina 1,865 ni dawa zilizo katika utaratibu wa Miradi Msonge na aina ya dawa 680 ni dawa muhimu. Dawa za aina 312 ndizo zimeainishwa kuwa ni dawa muhimu na za kipaumbele cha Wizara kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinapatikana nyakati zote katika Bohari ya Dawa (MSD). Tathimini ya upatikanaji wa aina hizo 312 katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini hadi kufikia Machi, 2020 ilikuwa ni asilimia 80 Aidha upatikanaji wa dawa aina 312 katika maghala ya Bohari ya Dawa ilikuwa ni asilimia 56. Vilevile, Bohari ya Dawa imeendelea kununua Dawa kutoka kwa wazalishaji wa dawa ambapo

hadi kufikia mwezi Machi 2020, Bohari ya Dawa ilikuwa imeingia mikataba ya muda mrefu (Framework Agreement) na jumla ya wazalishaji 161 kati yao 18 wakiwa ni wazalishaji wa ndani. Hatua hii inakusudiwa kuhakikisha upatikanaji wa aina zote 680 za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi unaendelea kuimarika katika maghala yote ya Bohari ya Dawa (MSD) kulingana na upatikanaji wa fedha.

**83. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi wa fedha za dawa katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara imeandaa mwongozo wa Mfuko Endelevu wa Bidhaa za Afya (*Health Commodities Revolving Fund)* kwa lengo la kuhakikisha fedha zitokanazo na huduma za dawa, uchunguzi na upasuaji zinalindwa na kurudi kununua dawa na vitendanishi vya maabara. Pia, katika kuhakikisha suala la dawa kuchina/kuchotora linapatiwa ufumbuzi, Serikali iliandaa mwongozo wa kuandaa maoteo ya dawa. Mwongozo huo umeanza kutumika katika kuandaa maoteo ya bidhaa za afya kwa mwaka 2020/21. *Ninawaelekeza waganga wakuu wa mikoa na halmashauri zote kuhakikisha wanatumia miongozo hiyo katika kulinda fedha za dawa na vitendanishi, pamoja na kuandaa maoteo ya dawa ili kuepukana na changamoto za dawa kukosekana au kuchina katika vituo vya kutolea huduma za afya.*

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bohari ya Dawa ilisambaza dawa muhimu zenye thamani ya shilingi bilioni 99.3 na dawa za Miradi Msonge zenye thamani ya shilingi bilioni 361.5 katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020. Dawa hizo zilisambazwa moja kwa moja hadi vituo vya kutolea huduma za afya 5,749 kwa gharama ya shilingi bilioni 15.06. Katika kipindi hicho, Bohari ya Dawa imenunua dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 125.1 na kupokea dawa za miradi msonge (TB, UKIMWI, Malaria) zenye thamani ya shilingi bilioni 216. Aidha, katika kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa, Wizara imenunua Mashine 4 za X-ray za Kidigitali na kupelekwa katika hospitali za Rufaa za Mikoa ya Manyara, Mt Meru (Arusha), Songwe na Mwananyamala (DSM) na kufanya jumla ya X-ray hizo kufikia 12. X-ray hizo zimenunuliwa kupitia mradi unaotekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Uholanzi kupitia mradi wa ORIO ambao mkataba wake ulianza mwaka 2014 na una gharama ya shilingi bilioni 60.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na USAID kupitia mradi wa *Medicines Technology and Pharmaceutical Services (*MTaPS) imetoa mafunzo ya kukusanya taarifa ya mwenendo ya matibabu ya kutumia dawa za antibiotiki kwa kutumia mfumo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) ujulikanao kama

*Point Prevalence Survey (PPS)*. Mafunzo hayo yamefanyika kwa Hospitali za Rufaa za Kanda za Mbeya na Benjamin Mkapa Dodoma; Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRH) za Temeke, Kagera, Sekou Toure (Mwanza) na Maweni (Kigoma). Vilevile, ukusanyaji wa taarifa za matumizi ya dawa za antibiotiki (*antibiotic use*) kwa kutumia mfumo wa PPS umefanyika kwa hospitali hizo sita.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bohari ya Dawa pia imekamilisha maandalizi ya ununuzi wa dawa za nchi 16 za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kupitia mfumo wa *Pooled Procurement Services* (PPS). Hadi kufikia Mwezi Februari 2020, Bohari ya Dawa imesaini mikataba 40 na washitiri mbalimbali kwa ajili ya manunuzi ya pamoja ya nchi za SADC. Aidha, mikataba hiyo imeleta unafuu wa bei kwa asilima 30 mpaka 60 kwa dawa zinazonunuliwa kupitia mfumo wa manunuzi ya pamoja.

### Upatikanaji wa Damu Salama

**87.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama ilipanga kukusanya chupa za Damu Salama 375,000 ili kukidhi mahitaji ya Damu Salama nchini katika kipindi cha mwaka mzima wa 2019/20. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020,

Wizara ilifanikiwa kukusanya na kusambaza idadi ya chupa za damu salama **227,677** sawa na **asilimia 61** ya lengo**.** Damu zote zilizokusanywa zilipimwa makundi ya damu, pamoja na magonjwa makuu manne ambayo ni UKIMWI (HIV), Homa ya ini B na C (HBV &HCV) na Kaswende (Syphilis). Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la chupa 21,427 sawa na asilimia 10 ikilinganishwa na idadi ya chupa za damu **206,250** zilizokusanywa, kupimwa na kusambazwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018. Aidha, kumekuwepo na ongezeko la upatikanaji wa damu salama ikilinganishwa na mwaka 2015/16 wakati Serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani ambapo jumla ya chupa za damu salama 104,632 zilikusanywa, kupimwa na kusambazwa.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara yangu katika ukusanyaji wa chupa za damu na kuhakikisha damu salama inapatikana kwa wahitaji wa damu katika vituo vyote vya afya vya kutolea huduma, Wizara pia inazalisha aina tatu za mazao ya damu ambazo ni Chembe Sahani (Platelates) ambazo husaidia damu kuganda hasa kwa wagonjwa wa saratani, Chembe nyekundu (Packed red cells) ambazo husaidia kubeba oksijeni mwilini na Plasma (Fresh frozen Plasma) ambazo husaidia kugandisha damu isiendelee kutoka hasa kwa mama wajawazito wanaotokwa damu wakati wa uzazi/kujifungua.

Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya chembe sahani 2,594, chembe nyekundu 46,854, na plasma zilizogandishwa 7,076 zilizalishwa kwa ajili ya kuweza kutumika katika hospitali mbalimbali. Mazao haya ya damu huzalishwa kupitia kanda saba za Mpango wa Taifa wa damu salama. Aidha, Mpango unaendelea na mkakati wa kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kupitia hospitali zote za Rufaa za Mikoa kwa kuwajengea uwezo na kuwanunulia vifaa kwa ajili ya uzalishaji.

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara ilipanga kujenga vituo vitano (5) vya Damu Salama katika mikoa ya Njombe, Iringa, Manyara, Rukwa na Kigoma ambapo hadi sasa ujenzi wa kituo cha Njombe umeshaanza na utaratibu wa kupata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vingine vya Mikoa unaendelea. Vilevile, Wizara inajenga kituo cha damu salama cha Kanda ya Kati – Dodoma kupitia ufadhili wa KOICA na UNICEF. Ujenzi huu unapelekea kuwa na jumla ya vituo nane (8) vya Kanda vya Damu Salama ikilinganishwa na vituo saba vilivyokuwepo tangu kuanzishwa kwa Mpango mwaka 2005.

## Uimarishaji wa huduma za Matibabu ya Kibingwa nchini

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa nchini, ili kuokoa maisha ya wananchi wengi sambamba na kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020 Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa ziliwasilisha Wizarani idadi ya wagonjwa 92 waliokuwa na mahitaji ya kupatiwa matibabu nje ya nchi, ambapo wagonjwa 53 walipatiwa kibali cha kwenda kutibiwa nje ya nchi ikilinganishwa na rufaa 554 zilizowasilishwa wizarani mwaka 2015/16 ambapo wagonjwa 385 walipatiwa kibali na kwenda kutibiwa nje ya nchi.

**91.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kupitia hospitali ngazi ya Taifa na kanda imehudumia jumla ya wagonjwa 1,763,950. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 1,613,841 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 150,109 ikilingalinishwa na wagonjwa 1,388,286 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2018/19. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 1,160,243 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 247,979 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.1** hapo chini. Aidha, kati

ya wagonjwa hao 1,763,950 waliohudumiwa katika hospitali hizo, jumla ya wagonjwa 304,735 walikuwa ni wagonjwa wa misamaha, na walizigharimu Hospitali hizo za Rufaa za Taifa na kanda jumla ya shilingi 31,430,076,324.

**Jedwali Na.1; Idadi ya Wagonjwa waliohudumiwa katika Hospitali ngazi ya Taifa na Kanda - Julai 2019 hadi Machi 2020.**

| Na. | Jina la Hospitali | Wagonjwa wa Nje (OPD) | Wagojwa wa kulazwa (IPD) | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) | 391,230 | 36,819 | 428,049 |
| 2 | Hospitali ya Mloganzila | 66,769 | 7,242 | 74,011 |
| 3 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) | 173,846 | 6,153 | 179,999 |
| 4 | Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) | 74,369 | 2,831 | 77,200 |
| 5 | Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI) | 58,208 | 14,504 | 72,712 |
| 6 | Hospitali ya Benjamin Mkapa-Dodoma | 85,619 | 4,062 | 89,681 |
| 7 | Hospitali ya Afya ya Akili (Mirembe) | 103,013 | 2307 | 105,320 |
| 8 | Hospitali ya Kibong'oto | 18,808 | 3,802 | 22,610 |
| 9 | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya | 200,444 | 34,964 | 235,408 |

| Na. | Jina la Hospitali | Wagonjwa wa Nje (OPD) | Wagojwa wa kulazwa (IPD) | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 10 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa (Bugando) | 249,535 | 19,746 | 269,281 |
| 11 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC) | 192,000 | 17,679 | 209,679 |
| | **Jumla** | **1,613,841** | **150,109** | **1,763,950** |

**Chanzo:** *WAMJW, Aprili 2020.*

## Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

**92.** ***Mheshimiwa spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Hospitali ya Taifa Muhimbili imehudumia jumla ya wagonjwa 428,700. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 391,230 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 36,819. Aidha, wagonjwa wa misamaha walikuwa 121,136 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 15,267,868,594 katika kipindi hicho.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya wagonjwa 13 walipata huduma ya **upandikizaji wa figo**. Hospitali kwa sasa imefikisha jumla ya wagonjwa 56 tangu huduma hizi zilipoanza kutolewa mwaka 2018. Hospitali imetumia jumla ya shilingi bilioni 1.68 kwa wagonjwa 56 ikiwa ni wastani wa shilingi milioni 30 kwa mgonjwa mmoja. Wagonjwa hao wangepatiwa

matibabu hayo nje ya nchi wangeigharimu Serikali jumla ya shilingi bilioni 6.72 kwa gharama ya shilingi milioni 120 kwa mgonjwa mmoja, hivyo Serikali imeokoa jumla ya shilingi bilioni 5.04. Aidha, Hospitali imeweka lengo la kufanya upandikizaji wa figo kwa wagonjwa watano (5) kila mwezi.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imetoa huduma ya **upandikizaji vifaa vya usikivu kwa watoto** 9 na kufikisha jumla ya wagonjwa 30 waliopata huduma hii tangu ianze kutolewa mwaka 2017. Hospitali imetumia kiasi cha shillingi bilioni 1.08 kwa gharama ya shilingi milioni 36 kwa mgonjwa mmoja ambapo kama wagonjwa hawa wangepatiwa matibabu nje ya nchi ingegharimu kiasi cha shilingi bilioni 3 kwa gharama ya shilingi milioni 100 kwa kila mgonjwa mmoja, hivyo Serikali imeokoa kiasi cha shilingi bilioni 1.92. Vilevile, jumla ya wagonjwa 288 walipata huduma ya **interventional radiology** ili kuruhusu upasuaji wa shingo na kichwa, kuondoa uvimbe kwenye sehemu ya kinywa, uso na shingo, kuweka mirija kwenye figo, kuzibua mirija ya nyongo iliyoziba, kuzibua mirija ya uzazi na kuondoa usaha ndani ya tumbo. Tangu huduma hii ilipoanza Oktoba 2017 jumla ya wagonjwa 846 wamehudumiwa ambapo Hospitali imetumia kiasi cha shilingi bilioni 6.78 kwa gharama ya shilingi milioni 8 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na gharama ya shilingi milioni 98 kwa mgonjwa

mmoja kama angepata huduma nje ya nchi na hivyo Serikali kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 76.14.

**95. *Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeendelea na maandalizi ya kuanzisha huduma za **kupandikiza uloto (bone marrow transplant)** baada ya kupokea shilingi bilioni 6.22 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango mwezi Juni, 2019. Kazi ya ununuzi wa mashine na vitendea kazi pamoja na kuandaa miundombinu kama vile kutengeneza chumba kwa ajili ya *cell processing* na *chemo day care* ambavyo vimeshakamilika na baadhi ya mashine zimeshawasili. Aidha, Hospitali imepeleka timu ya wataalamu 11 katika mafunzo ya mwezi mmoja nchini India. Huduma hii inatarajia kuanza kutolewa mwezi Mei 2020.

**96. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Hospitali ya Taifa Muhimbili imepokea kiasi cha shilingi millioni 900 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambazo zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba mbalimbali ikiwa ni pamoja na: *Endoscopy machine* kwa shilingi 397,246,886; *lung function test* kwa shilingi 140,000,000; na *full blood picture machine* mbili kwa shilingi 362,753,114.

**97. *Mheshimiwa Spika,*** Hospitali ilifanya ufunguzi rasmi wa Chumba cha Wagonjwa

Mahututi (ICU) ya watoto njiti (Neonatal ICU) pamoja na ICU ya watoto (Peadriatic ICU). Ukarabati pamoja na ununuzi wa vifaa umegharimu kiasi cha shilingi bilioni 4.9 ambapo shilingi bilioni 2.6 ilitumika kwa ICU ya watoto njiti na shilingi bilioni 2.3 kwa ICU ya watoto zaidi ya mwezi mmoja mpaka miaka 5. Aidha, Hospitali imekarabati jengo la Chuo cha Tiba Shirikishi kilichopo Muhimbili pamoja na hosteli za wauguzi kwa gharama ya shilingi milioni 250. Kwa upande wa **Mafunzo**, Hospitali imeendelea kudhamini mafunzo ya shahada za uzamili katika tiba kwa wataalam wake. Jumla ya wataalam 81 wapo masomoni kati ya hao madaktari 27 wapo nje ya nchi kwa ajili ya kupata mafunzo katika Nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma za ICU, magonjwa ya kinamama, huduma za masikio, pua na koo.

### Hospitali ya Mloganzila

**98. *Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020 Hospitali imehudumia jumla ya wagonjwa 74,011 ukilinganisha na wagonjwa 40,639 waliohudumiwa kipindi kama hiki kwa mwaka 2018/19. Kati ya wagonjwa hao, wagonjwa 7,242 walikuwa ni wa kulazwa (IPD) na wagonjwa 66,769 walikuwa ni wa nje (OPD). Aidha, wagonjwa wa misamaha walikuwa 9,586 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 1,337,673,597 katika kipindi hicho. Hali ya

upatikanaji wa damu katika Hospitali imefikia wastani wa asilimia 94.4 ya mahitaji. Hali ya upatikanaji wa dawa ilifikia wastani wa asilimia 95 ya mahitaji ambapo jumla ya Shilingi bilioni 2.95 kutoka mapato ya ndani zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

**99.** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuanzisha **huduma za kupandikiza uloto (Bone marrow transplant)**. Huduma hii itafanywa kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), ambapo vyumba vya kulaza wagonjwa watakaopatiwa huduma hii vimekamilika na vitakuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa sita (6) kwa wakati mmoja. Huduma hii inatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2020. Aidha, Hospitali imeweza kuanzisha chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (High Dependency Unit – HDU) ambayo ina uwezo wa kulaza wagonjwa 10 kwa wakati mmoja. Vilevile, eneo maalum lililopo *Mortuary* kwa ajili ya ndugu wa marehemu kupumzika wakati wakisubiri kuchukua miili ya wapendwa wao limekamilika.

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kudhamini mafunzo ya shahada ya uzamili katika tiba kwa wataalam wake. Jumla ya wataalam 45 wapo masomoni. Pia, Hospitali kwa kushirikiana na *Korea Foundation for International Healthcare (KOFIH)* na vyuo vikuu

vya Afya vya nchini Korea imeweza kufadhili watumishi 7 kwenda nchini Korea kwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Vilevile, Hospitali imeendelea kushirikiana na wataalam toka Korea katika kuwajengea uwezo wataalam wa hapa nchini na hasa katika Hospitali ya Mloganzila, katika maeneo ya magonjwa ya kina mama pamoja na Upasuaji wa Ubongo (NeuroSurgery).

## Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020 Taasisi iliendelea kutoa huduma zake za kibingwa kulingana na miongozo ya Serikali, sera na malengo yaliyowekwa ambapo jumla ya wagonjwa 180,856 walihudumiwa. Kati yao, wagonjwa wa nje (OPD) ni 173,846 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) 6,153 ikilinganishwa na wagonjwa 172,920 kati yao wagonjwa wa nje (OPD) 166,854 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) 6,066 kwa kipindi kama hiki mwaka 2018/2019.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imekamilisha chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (*High Dependant Unit* - HDU) na kukiwekea vitanda vipya vya kisasa 16 na *monitor* zake na hivyo kuwezesha kupunguza idadi ya wagonjwa wanaosubiria upasuaji hasa wa kichwa ambao baada ya upasuaji

hutakiwa kupelekwa chumba cha uangalizi maalum. Hospitali pia imeboresha chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) na kufikia kiwango cha kimataifa kwa kuwekewa vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja na vitanda 18 vyenye *monitor* na *ventilator* za kisasa, na hivyo kuwezesha kupunguza idadi ya vifo (mortarity rate) kufikia asilimia 3.8 ikilinganishwa na asilimia 4.9 kipindi kama hicho mwaka 2015/16

**103. *Mheshimiwa Spika***, Hospitali ilifanya upasuaji kwa wagonjwa 4,978 kati yao wakiwemo: upasuaji mifupa mbalimbali 1,758; kubadilisha nyonga 145; goti 159; upasuaji wa goti kwa kutumia matundu 198; upasuaji wa mfupa wa kiuno 46; upasuaji wa uti wa mgongo 330; ubongo 139; watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 284; upasuaji wa mfupa wa paja (femur) 266; na wagonjwa wa dharura 1,653. Aidha, kwa mara ya kwanza Taasisi imeweza kutoa matibabu ya kifafa (Epilepsy) kwa njia ya upasuaji. Aidha Hospitali inakamilisha ujenzi wa chumba maalum cha kisasa kwa ajili ya kufanya matibabu ya ubongo kupitia mishipa ya damu (Angio Suite) na imeshanunua mitambo ya kisasa ya kufanyia upasuaji huo, ambapo ujenzi na usimikaji wa mitambo utakamilika Mei 2020. Hii imetokana na pesa zilizotolewa na Serikali, kiasi cha shillingi bilioni 7.9, kwa ajili ya ujenzi wa maabara hii na ununuzi wa seti za kufanyia upasuaji.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 6.41 kutibu wagonjwa waliohitaji upasuaji wa kibingwa ambapo kama wangepelekwa nje ya nchi wangegharimu Serikali zaidi ya shilingi bilioni 18.34 na kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 11.93. Vilevile, katika kutekeleza Sera ya afya kwa wazee, watoto na wagonjwa wasiojiweza, Taasisi imekua ikitoa huduma kwa wagonjwa mbalimbali wasio na uwezo wa kuchangia gharama za matibabu katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Taasisi imeweza kusamehe zaidi ya wagonjwa 1,011 ambapo kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 580,037,806 zimesamehewa.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi iliingia mkataba na Hospitali ya Nyangao Lindi kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi, ambapo hadi kufikia Machi 2020, madaktari bingwa wa MOI wamewahudumia wagonjwa 1,047 na wamewafanyia upasuaji wagojwa 236. Vilevile, Taasisi imepewa eneo kwenye Hospitali ya Rufaa ya Kwangwa/ Mwalimu Nyerere Memorial Hospital - Musoma inayomaliziwa kujengwa, ili kuwezesha huduma za kibingwa na bobezi za mifupa na mishipa ya fahamu kwa wananchi wa kanda ya ziwa kutolewa kwenye hospitali hiyo.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imekamilisha chumba cha Tiba Mtandao (Telemedicine) kwa kufunga mitambo inayounganisha Hospitali za Rufaa za Mikoa na Wilaya. Kupitia huduma

hiyo, picha za X-ray na CT Scan zitakua zinatumwa MOI, na kusomwa na wataalamu wa MOI kisha ripoti kurudishwa kwa haraka kwenye hospitali husika. Vilevile, Hospitali kwa kushirikiana na Taasisi ya BMVSS ya India, iliendesha kambi ya mwezi mmoja ambapo wagonjwa 551 walitengenezewa viungo bandia pasipo malipo na mashine zilizotumika

kwenye kambi hiyo, zenye thamani ya shilingi milioni 300 zilibaki kwenye Hospitali.

**Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)**

**107.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 77,200 ikilinganishwa na wagonjwa 69,601 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2018/19. Kati yao, wagonjwa 74,369 walikuwa wa nje (OPD) na wagonjwa wakulazwa (IPD) walikuwa 2,831. Miongoni mwa waliopata huduma ni pamoja na wagonjwa kutoka nchi za DRC, Comoro, Uganda, Malawi na Burundi. Aidha, wagonjwa wa misamaha walikuwa 633 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 1,022,702,926 katika kipindi hicho.

**108.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeweza kufanya upasuaji kwa wagonjwa 384, kati ya wagonjwa waliofanyiwa upasuaji, wagonjwa 283 walifanyiwa upasuaji mkubwa wa kufungua kifua na kusimamisha moyo, kati yao watu wazima walikuwa 103 na watoto walikuwa

180. Aidha, wagonjwa wengine 101 ambao ni watu wazima wenye matatizo ya mishipa ya damu walifanyiwa upasuaji kwa njia ya kisasa (Vascular surgery), upasuaji huu umefanywa na wataalam wa ndani. Taasisi imefanikiwa kufanya upasuaji huo mgumu ikiwa ni ishara ya kuimarika kwa uwezo wa waatalam wazalendo katika utoaji wa huduma za kibingwa na za kisasa kwa magonjwa ya moyo. Aidha, jumla ya wagonjwa 1,410 walipata huduma za upasuaji wa moyo bila kufungua kifua kwa kutumia mtambo maalum *Catheterization Laboratory* ikilinganishwa na wagonjwa 246 waliofanyiwa huduma hiyo kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/16

**109. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 4.69 kwa ajili ya kununua na kusimika mtambo mwingine wa pili ambao ni maalum na wa kisasa wa *Cathlab* na mtambo wa *Cath 2* kwa ajili ya tiba za mfumo wa umeme wa moyo. Mitambo hii itaifanya Tanzania kuwa kinara katika nchi za Afrika Mashariki na Kati kwa kuongeza uwezo wa kufanya upasuaji kwa wagonjwa wa moyo bila ya kufungua kifua.

### Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI)

**110. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya wagonjwa 58,208 waliohudumiwa katika Taasisi, ambapo wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 43,704 na wagonjwa waliolazwa (IPD) walikuwa 14,504.

Kati ya wagonjwa hao, jumla ya wagonjwa 22,462 walipatiwa huduma za tiba mionzi, wagonjwa 14,384 walipatiwa huduma ya tiba kemia na wagonjwa 21,362 walipata tiba ya kemia na mionzi. Aidha, wagonjwa wa misamaha walikuwa 45,447 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 8,021,770,407 katika kipindi hicho. Huduma za kibingwa za tiba ya saratani zimeendelea kuimarishwa baada ya Hospitali kununua na kusimika mashine za kisasa za LINAC, uwepo wa mashine za kuchunguza matokeo ya tiba saratani kwa njia ya damu (**tumor markers**) na upatikanaji wa dawa za aina zote za kutibu saratani na hivyo kuchangia kupungua kwa rufaa za wagonjwa nje ya nchi kufikia wagonjwa kutoka wagonjwa 164 mwaka 2015/16 hadi wagonjwa 2 mwaka 2019/20 Vilevile, Taasisi imenunua majokofu manne (4) kwa ajili ya maabara na kufunga mashine mpya yenye uwezo mkubwa ya vipimo vya *chemistry* na kununua mashine za *oxygen concentrators* 9 kwa ajili ya wagonjwa wanaolazwa wakiwa na wenye uhitaji maalum wa hewa ya *oxygen*.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Taasisi iliendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba za dawa nyuklia ambapo katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya wagonjwa **1,831** walipatiwa huduma. Wagonjwa **698** walifanyiwa uchunguzi (diagnostic scans) katika mifupa, figo, ubongo, na tezi ya shingo; na wagonjwa **25** walipatiwa tiba ya nyuklia. Pia,

Taasisi ilitoa huduma za uchunguzi wa awali wa dalili za saratani za mlango wa kizazi, matiti, tezi dume, Kaposi sarcoma, utumbo mpana

na ngozi kwa wenye ualbino kwa wananchi **10,871** ambapo wananchi **7,002** walifanyiwa uchunguzi katika Taasisi na wananchi **3,869** katika huduma **za mikoa minne (4)** ambayo ni Iringa, Tanga, Dodoma na Urambo - Tabora.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, ukusanyaji takwimu za usahihi za ugonjwa wa saratani uliendelea kutekelezwa nchini kwa kusimamiwa ambapo hadi sasa, jumla ya takwimu za wagonjwa **23,356** zimeingizwa katika mfumo huo unaoitwa *Cancer Registry Software Version 5 (CANREG-5).* Huduma za maabara zimezidi kuimarika ambapo katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya vipimo vya maabara **129,669** vilifanyika, na kati ya vipimo hivyo **127,403** vilikuwa vipimo vya kawaida na **2,266** ni vya patholojia. Taasisi ilifanikiwa kutoa jumla ya vipimo **13,563** vya radiolojia, kati ya vipimo hivyo, vipimo **4,941** ni vya X-ray, **7,028** vya ultrasound na **1,594** vya CT Scan.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili iliendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi **72** wa Shahada

ya Kwanza ya Tiba ya Mionzi (Bachelor of Science in Radiation Therapy Technology) na wanafunzi **32** wa Shahada ya Uzamili ya Onkolojia (Masters of Medicine in Clinical Oncology). Mafunzo haya yameongeza uwepo wa wataalam wa huduma za saratani hapa nchini; kwa sasa Taasisi ina madaktari bingwa wa **Onkolojia 30**, ikilinganishwa na madaktari bingwa 13 waliokuwepo mwaka 2015.

### Hospitali ya Benjamin Mkapa

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Hospitali imeendelea kutoa huduma ambapo jumla ya wagonjwa 89,681 walihudhuria na kupata matibabu, ikilinganishwa na wagonjwa 57,624 waliopata huduma kwa kipindi kama hiki mwaka 2018/19. Kati ya hao, wagonjwa 85,619 walikuwa wa nje (OPD) na wagonjwa waliolazwa (IPD) 4,062. Wagonjwa wanaopatiwa huduma katika hospitali wameendelea kuongezeka ikilinganishwa na wagonjwa 16,235 mwaka 2015/16 wakati Serikali ya Awamu ya Tano ilipokuwa inaingia madarakani. Ongezeko hilo limetokana na uboreshwaji wa huduma zinazotolewa kutokana uwepo wa vifaa vya kisasa na wataalam wenye ujuzi. Aidha, wagonjwa wa misamaha walikuwa 1,146 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 146,426,900 katika kipindi hicho.

Jumla ya vipimo 87,308 vya maabara vilifanyika ambapo kati ya vipimo hivyo, wagonjwa 18,271 walifanyiwa vipimo vya mionzi na *imaging* kama ifuatavyo: *Ultra-Sound* wagonjwa 8,038, *X-Ray* wagonjwa 5,785; *Mammography* wagonjwa 127; *CT- Scan* wagonjwa 2,117; *MRI* wagonjwa 1,270, *Fluoroscopy* wagonjwa 148, *Esophagogastroduodenascopy* (EGD) wagonjwa 674 na *Colonoscopy* wagonjwa 112.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia machi 2020, jumla ya wagonjwa watano (5) walipata huduma ya Upandikizwaji wa figo na kufikisha jumla ya **wagonjwa 12** waliopata huduma hii toka hospitali ilipoanza kutoa huduma za kupandikiza figo mwezi Machi 2018. Gharama ya upandikizaji figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa ni kati ya shilingi milioni 22 hadi milioni 25 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na shilingi milioni 100 hadi milioni 120 mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Upatikanaji wa huduma hizo hapa nchini kumeiwezesha Serikali kuokoa jumla ya shilingi bilioni 1.14. Aidha, kati ya wagonjwa waliohudumiwa na Taasisi, mgonjwa mmoja (1) alipandikizwa figo na wataalam wa ndani bila usaidizi wa wataalam kutoka nje ya nchi na wagonjwa wote hali zao zimeimarika. Katika kipindi hiki, jumla ya *session* 4,247 za uchujaji wa damu zilifanyika kwa wagonjwa 109 ambao figo zao zimeshindwa kufanya kazi ikilinganishwa na *session* 1,549

zilizofanyika kwa kipindi kama hiki kwa mwaka 2018/19, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 164.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali ilifanikiwa kuanzisha huduma ya uchunguzi na matibabu ya moyo kwa kutumia maabara maalum *cathlab* yenye thamani ya shilingi 2,449,648,100, ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2020, jumla ya wagonjwa 141 wenye maradhi ya moyo wamechunguzwa na kutibiwa kwa kutumia maabara hii toka ilipozinduliwa Februari, 2019. Vilevile, jumla ya wagonjwa 2,218 walipata huduma ya upasuaji, kama ifuatavyo; *general surgery* (513), *Urology* (440), *Obstetric and Gynaecolgy* (418), magonjwa ya pua, masikio na koo (324), macho (298), *orthopaedics* (205) na kinywa na meno (20). Hospitali pia ilitoa huduma za mkoba (outreach medical services) katika Mikoa 3 ambapo jumla ya wananchi 2,243 walihudumiwa, kati yao 153 walifanyiwa upasuaji. Mikoa hiyo ni Manyara (245), Dodoma (1,507) na Iringa (491).

**Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Hospitali ilihudumia wagonjwa 105,320, kati yao 103,013 ni

wagonjwa wa akili wa nje (OPD) na wagonjwa wa akili wa ndani (IPD) 2,307. Aidha, wagonjwa wa misamaha waliopewa huduma walikuwa 86,202 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 746,188,692 katika kipindi hicho. Jumla ya wagonjwa 440, walipata huduma za kibingwa za walipewa huduma za Saikolojia na wagonjwa *Neuro-recognative and dementia* wagonjwa 165 wapatao 94 walifanyiwa uchunguzi na kuandikiwa taarifa za kisheria. Vilevile, katika kliniki ya afya ya akili kwa watoto na vijana wagonjwa 1,293 walihudumiwa. Taasisi pia, ilipokea wagonjwa wapya 150 wenye matatizo ya utumiaji wa madawa ya kulevya na hivyo kufanya jumla ya waraibu wanaohudumiwa na kituo cha Itega kufikia 479 toka kilipoanza kutoa huduma mwaka 2018.

**Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto.**

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 22,610 ambapo wagonjwa wa nje walikuwa 18,808 na wagonjwa waliolazwa 3,802. Kati ya wagonjwa waliolazwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu walikuwa 243, Kifua kikuu sugu ambata na VVU 20, Kifua kikuu cha kawaida 478 na kifua kikuu ambata na VVU walikuwa 56. Aidha, wagonjwa

waliomaliza matibabu ni zaidi ya asilimia 80.4 na kati yao asilimia 80 walithibitishwa kupona kifua kikuu sugu. Vilevile, Hospitali imeweza kufanya ufuatiliaji wa vimelea vya magonjwa ambukizi ya Kifua kikuu ambapo wagonjwa 205 walipimwa na kati yao 36 waligundulika kuwa na kifua kikuu na kuanzishiwa matibabu. Hospitali imeendelea pia kutoa huduma kwa wagonjwa wa misamaha, ambapo jumla yao walikuwa 6,103 ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 1,076,209,833 katika kipindi hicho.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali iliweza kufanya Usimamizi Shirikishi katika mikoa 26 ya Tanzania bara na Mikoa mitano (5) ya Zanzibar yenye vituo vya kuhudumia wagonjwa wa kifua kikuu sugu. Katika zoezi hilo, jumla ya vituo 121 vilitembelewa na Wagonjwa 459 walifanyiwa uchunguzi na kushauriwa kuendelea na dawa pamoja na matibabu. Aidha, jumla ya watumishi 367 walipewa elimu elekezi kuhusu matibabu ya Kifua kikuu sugu. Hospitali imeendelea kupanua wigo na uelewa katika Tiba ya Kifua Kikuu Sugu bila utumiaji wa sindano (Free Injectable DR-TB Regimens) ambapo, jumla ya watumishi 361 kutoka Mikoa ya Mwanza, Iringa, Rukwa, Mtwara, Singida, Morogoro na Kilimanjaro walijengewa uwezo

wa kutibu wagonjwa wanaogunduliwa na kuanzishiwa tiba isiyojumuisha matumizi ya sindano.

Vilevile, mafunzo ya kudhibiti magonjwa ambata ya Kifua Kikuu na Kisukari yalitolewa kwa wataalamu 89 kupitia mradi wa *adaptive diseases control expert program in Tanzania* - ADEPT) unaotekelezwa katika mikoa mitatu ya Iringa, Dar es salaam na Kilimanjaro. Baada ya mafunzo hayo Hospitali ilikabidhi vituo 27 *HbA1c Analyser Machine* kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa wenye magonjwa ambata ya Kifua Kikuu na Kisukari.

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha huduma zinazotolewa, Hospitali imenunua jumla ya Mashine tano ambazo zitatumika kwa ajili ya uchunguzi na ugunduzi wa kina wa vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa Kifua kikuu. Machine hizo ni *Mycobacteria Indicator Growth Tube – MIGT, Elisa Reader, Elisa Washer, Blood Culture Machine* na *Erythrocyte Sedimentation Rate Machine,* mashine hizi zimeigharimu Hospitali kiasi cha shilingi milioni 305. Uwepo wa mashine hizi unaifanya hospitali kuwa na uwezo wa kuchunguza vimelea vinavyosababisha magonjwa kwa njia ya damu (Blood borne diseases) pamoja na kupunguza

muda wa ufuatiliaji wa kuuawa kwa vimelea vya Kifua kikuu kutoka siku 60 mpaka siku 21.

### Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Hospitali imehudumia wagonjwa 235,408, ikilinganishwa na wagonjwa 234,347 waliopatiwa huduma mwaka 2018/19. Kati yao, wagonjwa 200,444 walikuwa wa nje na wagonjwa 34,964 walilazwa. Hospitali imeendelea pia kutoa huduma kwa wagonjwa wa misamaha, ambapo jumla ya wagonjwa 25,817 walihudumiwa na waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 565,439,719 katika kipindi hicho. Hospitali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa kwa kuongeza miundombinu ya kutolea huduma ambapo ukarabati na upanuzi wa jengo la kutolea huduma za dharura uliendelea kufanyika. Baada ya kukamilika hospitali imekuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa mahututi watano (5) kwa wakati mmoja na eneo la mapokezi ya wagonjwa limepanuliwa hivyo kupunguza msongamano na muda wa kupatiwa huduma.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ambapo jengo la huduma za Uzazi na Mtoto (RCH) katika kitengo cha wazazi Meta

limepanuliwa kwa kuongezwa vyumba vinne pamoja na sehemu ya kusubiria ambapo kwa sasa hospitali ina jumla ya vitanda 553. Vilevile, Serikali imetoa kiasi cha shilingi 3,695,934,111 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa 6 la kutolea huduma za afya ya uzazi na mtoto Meta ambapo hadi kufikia Machi 2020, ujenzi umefikia asilimia 50.

### Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 Hospitali ilihudumia jumla ya Wagonjwa 269,281 ikilinganishwa na wagonjwa 250,721 katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 249,535 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 19,746. Aidha, Hospitali imeendelea pia kutoa huduma kwa wagonjwa wa misamaha, ambapo wagonjwa 7,155 walihudumiwa ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 2,277,337,259. Vilevile, Hospitali imeendelea kuboresha huduma za kibingwa kwa kuanza kutoa matibabu yote ya Saratani baada ya kununua mashine ya tiba ya mionzi iitwayo *Brachytherapy* kwa shilingi bilioni 1.4

Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 821 wa matibabu ya Saratani ikilinganishwa na wagonjwa 5,367 waliopata huduma hiyo

mwaka 2018/19. Kati yao, wagonjwa 433 walipatiwa tiba ya Saratani kwa kutumia dawa (Chemotherapy) na wagonjwa 388 walipatiwa mionzi (Radiotherapy). Upatikanaji wa huduma hii umepunguza rufaa za wagonjwa wa saratani wa Kanda ya Ziwa kwenda Taasisi ya Saratani *Ocean Road*.

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ilifanikiwa kufanya upasuaji wa kibingwa kwa wagonjwa 8,612 ikiwemo upasuaji wa Moyo kwa kufungua Kifua (224), Upasuaji wa Ubongo (591) na Upasuaji wa mifupa (1,083), upasuaji wa fistula - VVF (133) na Upasuaji wa Mdomo Sungura (62). Kwa sasa hospitali ipo kwenye hatua za kukamilisha kuanzisha upasuaji kwa kutumia matundu madogo yaani *Laparoscopic surgery*. Aidha, huduma za kusafisha damu (Renal Dialysis) zimeendelea kuimarika ambapo jumla ya wagonjwa 311 walipata huduma hii, ikilinganishwa na wagonjwa 82 waliopata huduma hii mwaka 2018/19.

Hospitali kwa kushirikana na *Centre for Disease Control* (CDC) na *Tanzania Health Promotion Support* (THPS), ilifanikiwa kujenga Maabara ya kisasa ya uchunguzi wa magonjwa kupitia Vinasaba (DNA) yaani *Molecular Biology Laboratory*. Huduma ya maabara hii imesaidia kuondoa mrundikano wa vipimo vya UKIMWI kutoka katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

### Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kaskazini (KCMC)

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Hospitali ilihudumia wagonjwa 209,679. Kati yao wagonjwa 192,000 walikuwa ni wa nje (OPD) na wagonjwa 17,679 walikuwa wa kulazwa (IPD). Kwa upande wa huduma za upasuaji jumla ya wagonjwa 1,963 walifanyiwa upasuaji kama sehemu ya tiba zao. Hospitali imeendelea kutoa huduma za kusafisha damu ambapo jumla ya wagonjwa 1,527 wenye matatizo ya figo walihudumiwa, ikilinganishwa na wagonjwa 1,245, waliohudumiwa mwaka 2018/19. Aidha, Hospitali imeendelea pia kutoa huduma kwa wagonjwa wa misamaha, ambapo wagonjwa 499 walihudumiwa ambao waliigharimu Hospitali kiasi cha shilingi 388,420,591.

**126.** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali pia imeendelea kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa kwa kununua na kufunga mitambo mipya ya *MRI, CT na Digital X- ray*. Maboresho hayo yamewezesha wagonjwa 670 kufanyiwa kipimo cha MRI, wagonjwa 4,137 vipimo vya *CT Scan*, wagonjwa 12,502 vipimo vya *Ultrasound* na wagonjwa 12,754 vipimo vya *X-ray*. Aidha, Hospitali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za kibingwa ambapo, ujenzi wa wodi maalumu ya wagonjwa wa saratani unaendelea na umefikia asilimia 70. Vilevile, ujenzi wa vyumba vinne vya upasuaji

unaendelea na umefikia asilimia 50. Hospitali pia, imenunua kinu cha kufua hewa ya Oksijeni chenye uwezo wa kuzalisha mitungi 400 kwa siku hivyo kuokoa kiasi cha shilingi milioni 3 kwa siku kuanzia mwezi Februari 2020 ambapo mtambo huo ulipoanza kufanya kazi.

### Hospitali za Rufaa za Mikoa

**127.*Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa zilihudumia jumla ya wagonjwa 2,532,650 ambapo wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 2,308,401 na wagonjwa waliolazwa (IPD) walikuwa 224,249 ikilinganishwa na wagonjwa 3,292,103 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. **Jedwali Na. 2(a)** linatoa ufafanuzi kuhusu idadi ya vitanda na wagonjwa waliohudumiwa katika kipindi cha taarifa hii. Aidha, kati ya wagonjwa hao waliohudumiwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, jumla ya wagonjwa 559,030 walikuwa ni wagonjwa wa misamaha, na walizigharimu Hospital hizo jumla ya shilingi 7,019,675,521 mchanganuo wa misamaha kwa kila Hospitali ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 2(b)**

**Jedwali Na. 2(a): Wagonjwa waliohudumiwa-hospitali za Rufaa za Mikoa, Julai 2019 hadi Machi, 2020**

| Na. | Hospitali | Mkoa | Idadi ya Vitanda | Wagonjwa Julai 2019 hadi Machi 2020 | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | NJE (OPD) | WAKULAZWA (IPD) | |
| 1 | Amana | DSM | 341 | 126,197 | 14,586 | 140,783 |
| 2 | Bombo | Tanga | 457 | 69,671 | 11,316 | 80,987 |
| 3 | Bukoba | Kagera | 308 | 120,973 | 7,723 | 128,696 |
| 4 | Dodoma | Dodoma | 423 | 150,248 | 19,216 | 169,464 |
| 5 | Geita | Geita | 300 | 101,874 | 5,453 | 107,327 |
| 6 | Iringa | Iringa | 377 | 63,194 | 7,248 | 70,442 |
| 7 | Katavi | Katavi | 106 | 30,018 | 8,156 | 38,174 |
| 8 | Kitete | Tabora | 270 | 44,883 | 5,256 | 50,139 |
| 9 | Ligula | Mtwara | 222 | 28,257 | 3,222 | 31,479 |
| 10 | Manyara | Manyara | 89 | 20,506 | 2,536 | 23,042 |
| 11 | Maweni | Kigoma | 168 | 21,283 | 4,850 | 26,133 |
| 12 | Mawenzi | Kilimanjaro | 220 | 69,538 | 5,590 | 75,128 |
| 13 | Mbeya | Mbeya | 179 | 44,280 | 4,668 | 48,948 |
| 14 | Morogoro | Morogoro | 365 | 98,479 | 15,251 | 113,730 |
| 15 | Mt. Meru | Arusha | 379 | 79,986 | 12,526 | 92,512 |
| 16 | Musoma | Mara | 272 | 40,566 | 6,915 | 47,481 |
| 17 | Mwananyamala | DSM | 225 | 352,082 | 11,299 | 363,381 |
| 18 | Njombe* | Njombe | 64 | 3,247 | 362 | 3,609 |
| 19 | Sekeu Toure | Mwanza | 315 | 84,938 | 14,216 | 99,154 |
| 20 | Shinyanga | Shinyanga | 279 | 34,911 | 7,329 | 42,240 |
| 21 | Simiyu* | Simiyu | 20 | 4,732 | 492 | 5,224 |
| 22 | Singida | Singida | 300 | 60,809 | 8,235 | 69,044 |
| 23 | Sokoine | Lindi | 212 | 33,407 | 6,672 | 40,079 |

| Na. | Hospitali | Mkoa | Idadi ya Vitanda | Wagonjwa Julai 2019 hadi Machi 2020 | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | NJE (OPD) | WAKULAZWA (IPD) | |
| 24 | Songea | Ruvuma | 395 | 66,904 | 12,825 | 79,729 |
| 25 | Songwe | Songwe | 157 | 78,545 | 3,424 | 81,969 |
| 26 | Sumbawanga | Rukwa | 217 | 36,550 | 5,624 | 42,174 |
| 27 | Temeke | DSM | 304 | 376,073 | 12,471 | 388,544 |
| 28 | Tumbi | Pwani | 214 | 66,250 | 6,788 | 73,038 |
| | **Jumla** | | **7,178** | **2,308,401** | **224,249** | |

**Chanzo:** *WAMJW*

*Hospitali ya Njombe na Simiyu zina idadi ndogo ya wagonjwa kwa kuwa huduma zimeanza kutolewa hivi karibuni.

**Jedwali Na.2(b): Idadi ya Wagonjwa wa misamaha waliohudumiwa pamoja na gharama zao - hospitali za Rufaa za Mikoa, Julai 2019 hadi Machi, 2020**

| Na. | Hospitali | Idadi ya Wagonjwa Waliosamehewa | Gharama za Msamaha |
|---|---|---|---|
| 1 | Amana | 26,071 | 593,399,431 |
| 2 | Bombo | 23,997 | 545,012,870 |
| 3 | Bukoba | 9,307 | 129,041,370 |
| 4 | Dodoma | 24,803 | 572,797,340 |
| 5 | Geita | 30,423 | 277,760,331 |
| 6 | Iringa | 2,452 | 22,413,220 |
| 7 | Katavi | 12,201 | 236,684,750 |
| 8 | Kitete | 17,041 | 369,938,956 |
| 9 | Ligula | 5,123 | 64,678,965 |
| 10 | Manyara | 2,492 | 114,336,907 |
| 11 | Maweni | 4,147 | 78,034,625 |

| Na. | Hospitali | Idadi ya Wagonjwa Waliosamehewa | Gharama za Msamaha |
|---|---|---|---|
| 12 | Mawenzi | 7,368 | 67,143,775 |
| 13 | Mbeya | 4,130 | 54,902,930 |
| 14 | Morogoro | 18,075 | 254,627,066 |
| 15 | Mount Meru | 23,955 | 343,030,154 |
| 16 | Musoma | 15,437 | 189,284,312 |
| 17 | Mwananyamala | 206,955 | 649,396,650 |
| 18 | Njombe | 146 | 3,962,700 |
| 19 | Sekou Toure | 27,386 | 684,915,530 |
| 20 | Shinyanga | 4,886 | 72,107,270 |
| 21 | Simiyu | 122 | 2,878,050 |
| 22 | Singida | 8,001 | 404,255,399 |
| 23 | Sokoine | 5,050 | 102,627,875 |
| 24 | Songea | 16,607 | 195,286,283 |
| 25 | Songwe | 27,905 | 357,515,560 |
| 26 | Sumbawanga | 10,755 | 137,119,320 |
| 27 | Temeke | 20,033 | 391,137,740 |
| 28 | Tumbi | 4,162 | 105,386,142 |
| | **Jumla** | **559,030** | **7,019,675,521** |

**Chanzo:** *WAMJW*

## MABORESHO YANAYOENDELEA KUTEKELEZWA KATIKA HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA

### Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa tiba na Vitendanishi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

**128.** ***Mheshimiwa Spika***, hali ya upatikanaji wa dawa muhimu zaidi 30 (Tracer Medicines) katika hospitali za rufaa za mikoa umefikia asilimia 94 ukilinganisha na asilimia 93 mwaka 2018/19. Upatikanaji wa aina 312 za dawa zilizopitishwa na Wizara kama dawa muhimu umefikia asilimia 79.9. Vilevile, katika kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa, Wizara imenunua Mashine nne (4) za *X-ray* za kidigitali na kufanya jumla ya X-ray za aina hiyo kuwa 12. Mashine hizo zilipelekwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Simiyu, Singida, Njombe, Kagera, Dar es Salaam (Amana na Mwananyamala), Katavi, Manyara, Arusha (Mount Meru) na Songwe. Ufungaji wa mashine hizi umesaidia upatikanaji wa huduma za X-ray katika maeneo haya na pia kuongeza ubora wa matibabu kutokana na uchunguzi ulio sahihi kwa mgonjwa. Vilevile, kati ya mashine 12 za kidigitali, mashine 8 zimepatiwa kibali na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) kwa ajili ya kuanza kutoa huduma katika hospitali za Ruvuma, Morogoro, Simiyu, Singida, Njombe, Kagera, Amana (Dar es Salaam) na Katavi.

## Miundombinu ya Kutolea Huduma katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya, Wizara inatekeleza mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali za Mikoa ya; **Njombe** (Jengo la maabara, jengo la huduma za Uzazi na Mtoto, jengo la Upasuaji, jengo la huduma za dharura, jengo Benki ya damu, jengo la kufulia nguo), **Simiyu** (Jengo la maabara, jengo la huduma za Uzazi na Mtoto, jengo la Upasuaji na Radiolojia), **Geita** (Jengo la maabara na jengo la huduma za Uzazi na Mtoto), **Katavi** (Jengo la kutoa huduma za wazazi, dharura, wagonjwa wa nje, famasia, radiolojia, na wagonjwa mahututi), **Songwe** (jengo la wagonjwa wa nje, jengo la maabara na jengo la huduma za afya ya uzazi na mtoto), **Mara** – Mwalimu Nyerere Memorial Hospital, (jengo moja linalotoa huduma za utawala, wagonjwa wa nje, wagonjwa wa ndani, uchunguzi wa magonjwa, famasia, utakasaji wa vifaa, dharura, upasuaji na mahututi),

Miradi mingine ya miundombinu inaendelea kutekelezwa katika mikoa ya; **Dar es Salaam - Mwananyamala** (jengo la huduma za afya ya uzazi na mtoto), **Mwanza** (jengo la kutolea huduma za afya ya uzazi na mtoto), **Kilimanjaro** (jengo la kutolea huduma za afya ya uzazi na

mtoto), **Kigoma** (jengo la upasuaji), **Tabora** (jengo la kutolea huduma za dharura), **Iringa** (jengo la kutolea huduma za dharura), **Mbeya** (jengo la kutolea huduma za dharura, wodi ya upasuaji, jengo la huduma za upasuaji na utakasaji wa vifaa), **Ruvuma** (jengo la kutolea huduma za dharura), **Rukwa** (jengo la kutolea huduma za dharura), **Kagera** (jengo la kujifungulia na jengo la upasuaji), **Shinyanga** (jengo la huduma ya afya ya uzazi na mtoto), **Manyara** (jengo la wagonjwa wa nje na jengo la utawala), na **Singida** (jengo la kutolea huduma za maabara, famasia, upasuaji na wodi za wagonjwa).

### Upatikanaji wa Madaktari Bingwa

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma zitolewazo na Hospitali za rufaa za mikoa, Serikali imetoa kipaumbele katika kuhakikisha kuwa huduma za kibingwa katika fani za Upasuaji wa jumla (General Surgery), Magonjwa ya wanawake na uzazi (Obstetric & Gynaecology), Watoto (Paediatric & Child health), Magonjwa ya Ndani (Internal Medicine), Radiolojia (Radiology), Huduma za dharura (Emergency Medicine), huduma za Upasuaji wa mifupa na magonjwa ya ajali (Orthopaedic Surgery), na huduma za usingizi (Anaesthesiology) zinapatikana kwa uhakika.

131. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 2020, Hospitali hizi zimeweza kuongeza idadi ya madaktari bingwa wa fani tofauti takribani 64 na kufikia 258 ikilinganishwa na wale waliokuwepo 194 mwaka 2018/19. Idadi kubwa ikionekana kwa fani zote isipokuwa kwa Huduma za dharura na ajali, Huduma ya usingizi, Huduma za Magonjwa ya Kinywa na Meno, Masikio, Pua na Koo na Macho. Serikali inaendelea kuboresha huduma hizi ili kuhakikisha huduma zote 13 za kibingwa zinapatikana kwa ngazi hii. Hali halisi ya upatikanaji wa madaktari bingwa wa huduma mbalimbali imeelezwa katika **Jedwali Na.3**

**Jedwali Na.3: Idadi ya Madaktari bingwa wa huduma mbalimbali-Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa miaka mitatu mfululizo**

| Aina ya Huduma | Machi-20 | 2019 | 2018 |
|---|---|---|---|
| Upasuaji wa jumla | 36 | 28 | 28 |
| Huduma za Magonjwa ya wanawake na uzazi | 62 | 52 | 52 |
| Magonjwa ya watoto | 35 | 25 | 26 |
| Magonjwa ya Ndani | 32 | 27 | 27 |
| Radiolojia | 15 | 12 | 8 |
| Huduma za dharura na ajali | 3 | 3 | 1 |
| Upasuaji wa Mifupa na magonjwa ya ajali | 23 | 19 | 19 |

| Aina ya Huduma | Machi-20 | 2019 | 2018 |
|---|---|---|---|
| Huduma ya usingizi | 7 | 2 | 1 |
| Huduma za Magonjwa ya Kinywa na Meno | 29 | 28 | 27 |
| Huduma za Magonjwa Masikio, Pua na Koo | 8 | 1 | 1 |
| Huduma za Magonjwa ya Macho | 8 | 5 | 4 |
| **Jumla** | **258** | **202** | **194** |

**Chanzo:** *WAMJW*

## Huduma za Kujifungua

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya akina mama 82,315 walijifungua katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ukilinganisha na kina mama 120,696 waliojifungua mwaka 2018/19. Kupungua kwa idadi hii ni kutokana na jitihada za Serikali za kuboresha Vituo vya Afya katika halmashauri mbalimbali nchini, ambavyo vimewezeshwa kutoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni (CEmONC). Aidha, katika kipindi hicho vilitokea vifo 197 vinavyohusiana na uzazi kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.4.**

**Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa idadi ya akina mama waliojifungua na vifo vilivyotokana na uzazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, 2018/19 na 2019/20**

| Na | Hospitali | Waliojifungua | Vifo Vilivyotokana na Uzazi | Waliojifungua | Vifo Vilivyotokana na Uzazi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | | 2019/20 | |
| 1 | Amana | 10,306 | 12 | 7,250 | 8 |
| 2 | Bombo | 4,499 | 15 | 3,371 | 7 |
| 3 | Bukoba | 2,817 | 3 | 2,163 | 7 |
| 4 | Dodoma | 6,344 | 32 | 5,315 | 13 |
| 5 | Geita | 5,774 | 25 | 4,310 | 14 |
| 6 | Iringa | 3,483 | 12 | 1,751 | 5 |
| 7 | Katavi | 4,678 | 10 | 3,027 | 12 |
| 8 | Kitete | 4,105 | 14 | 3,202 | 6 |
| 9 | Ligula | 1,858 | 5 | 994 | 1 |
| 10 | Manyara | 943 | 3 | 907 | 1 |
| 11 | Maweni | 1,154 | 12 | 896 | 9 |
| 12 | Mawenzi | 2,417 | 2 | 2,133 | 1 |
| 13 | Mbeya | 3,218 | 7 | 2,535 | 2 |
| 14 | Morogoro | 5,299 | 34 | 3,960 | 20 |
| 15 | Mount Meru | 5,509 | 21 | 4,091 | 15 |
| 16 | Musoma | 3,718 | 4 | 2,321 | 8 |
| 17 | Mwananyamala | 8,299 | 11 | 5,768 | 7 |
| 18 | Njombe | 2,429 | 4 | 59 | 1 |
| 19 | Sekou Toure | 7,151 | 6 | 5,208 | 8 |
| 20 | Shinyanga | 3,108 | 21 | 2,475 | 9 |
| 21 | Simiyu | 2,132 | 11 | - | - |
| 22 | Singida | 4,448 | 15 | 2,735 | 9 |
| 23 | Sokoine | 1,566 | 9 | 906 | 5 |
| 24 | Songea | 7,244 | 8 | 5,485 | 4 |

| Na | Hospitali | Waliojifungua | Vifo Vilivyotokana na Uzazi | Waliojifungua | Vifo Vilivyotokana na Uzazi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **2018/19** | | **2019/20** | |
| 25 | Songwe | 3,417 | 10 | 3,457 | 6 |
| 26 | Sumbawanga | 5,134 | 16 | 2,281 | 9 |
| 27 | Temeke | 8,563 | 9 | 4,417 | 2 |
| 28 | Tumbi | 1,482 | 13 | 1,298 | 8 |
| | **Total** | **120,696** | **345** | **82,315** | **197** |

**Chanzo:** *WAMJW*

******Njombe na Simiyu ni Hospitali mpya ambazo zimeanza kutoa huduma mwezi Julai 2019. Katika kipindi hiki, Simiyu ilikuwa haitoi huduma za kujifungua. Aidha kwa mwezi Januari 2020, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi imesimamisha kutoa huduma za kujifungua kwa ajili ya kufanya ukarabati. Huduma hizi zinatolewa katika kituo cha Afya Irembo.*

## Huduma za Mkoba (outreach services)

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa kwenye mazingira ya karibu na wananchi, ambapo katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020 Hospitali za Rufaa za Mikoa 20 zilitoa huduma za mkoba katika fani za ubingwa zifuatazo; magonjwa ya macho, magonjwa ya watoto, dawa za usingizi, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya ndani, upasuaji

wa kawaida, afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, magonjwa ya sikio, pua na koo, afya ya akili, radiolojia, afya ya kinywa na meno, magonjwa ya damu, magonjwa ya ngozi na huduma za tiba kwa mazoezi (physiotherapy). Katika kliniki hizo, jumla ya wagonjwa 15,526 walihudumiwa, kati yao 1,999 walifanyiwa upasuaji kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.5**

**Jedwali Na.5: Idadi ya wagonjwa waliohudumiwa kupitia huduma ya mkoba na Hospitali za Rufaa za Mikoa**

| Na | Hospitali | Wagonjwa Waliohudumiwa | Wagonjwa Waliofanyiwa Upasuaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Amana | 84 | 0 |
| 2 | Bombo | 843 | 31 |
| 3 | Bukoba | 64 | 3 |
| 4 | Dodoma | 274 | 45 |
| 5 | Geita | 31 | 1 |
| 6 | Iringa | 410 | 91 |
| 7 | Manyara | 1,216 | 65 |
| 8 | Maweni | 2,330 | 131 |
| 9 | Mawenzi | 295 | 0 |
| 10 | Morogoro | 3,944 | 1,101 |
| 11 | Mount Meru | 1,083 | 78 |
| 12 | Musoma | 1,239 | 0 |
| 13 | Mwananyamala | 94 | 0 |
| 14 | Shinyanga | 242 | 34 |

| Na | Hospitali | Wagonjwa Waliohudumiwa | Wagonjwa Waliofanyiwa Upasuaji |
|---|---|---|---|
| 15 | Simiyu | 860 | 5 |
| 16 | Sokoine | 998 | 400 |
| 17 | Songea | 253 | 1 |
| 18 | Songwe | 45 | 13 |
| 19 | Sumbawanga | 451 | 0 |
| 20 | Temeke | 770 | 0 |
| | **Jumla** | **15,526** | **1,999** |

**Chanzo:** *WAMJW*

## UHAKIKI UBORA WA HUDUMA ZA AFYA

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa huduma za afya zinazotolewa zinakidhi viwango vya ubora, Wizara imeendesha mafunzo kwa wajumbe 245 wa timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa (RHMTs) na Halmashauri (CHMTs) kuhusu matumizi ya nyenzo za ufuatiliaji wa mpango kazi ulioachwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi baada ya zoezi la kufanya tathmini na kutoa nyota (Star Rating Assessment) kwa mchanganuo ufuatao: Dar es Salaam (20), Pwani (60), Rukwa (36), Katavi (31), Dodoma (56) na Njombe (42). Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa watumishi 1020 na kusambaza Mwongozo mpya wa Kitaifa wa Kukinga na Kudhibiti Maambukizo katika Vituo vya Kutolea

Huduma za Afya katika mikoa ya Mwanza watumishi 98, Kagera 81, Dar es Salaam 210, Kigoma 85, Katavi 66, Rukwa 61, Pwani 98, Njombe 65, Mbeya 82, Songwe 77 na Dodoma 97. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizo kwa walimu wa Vyuo vya Afya nchini ili kuwawezesha wanavyuo kupata taarifa ya mabadiliko na mapendekezo mapya yaliyotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwenye eneo la kukinga na kudhibiti maambukizi. Jumla ya walimu 61 kutoka vyuo 59 wenye fani mbalimbali za afya walipatiwa mafunzo hayo.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa huduma za afya zinazotolewa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa zinaboreshwa, Wizara imeziwezesha Bodi za Ushauri za Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRHAB) kusimamia Hospitali hizo kwa kutoa mafunzo kwa Timu za Usimamizi na Uendeshaji za Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRHMTs) zipatazo 28 na kufanya idadi ya Wajumbe waliopatiwa mafunzo kufikia 308. Wajumbe hao walipatiwa mafunzo juu ya namna ya kuanzisha, kuziendesha na kuzisimamia Bodi za Ushauri katika hospitali husika. Aidha, mwongozo wa kuanzisha, kusimamia na kupima Bodi za Ushauri za Hospitali za Rufaa za Mikoa umeandaliwa na umeanza kutumika.

## UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na jitihada za kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za afya nchini kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwemo **Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund),** ambapo kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, kiasi cha Shilingi 86,222,819,841 kimepokelewa kupitia Mfuko huo ikilinganishwa na Shilingi 92,440,912,680 zilizopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 68,313,229,142 sawa na asilimia 79.2 ya fedha zote zilizopokelewa zilipelekwa na kutumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuboresha huduma za afya ngazi ya msingi.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 25,867,451,925.22 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali katika sekta ya Afya ikilinganishwa na kiasi cha shilingi 87,840,050,111.47 zilizopokelewa kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi 20,447,241,499.31 ni kwa ajili ya utekelezaji wa **Mpango wa Malipo kwa Ufanisi (Results Based Financing-RBF)** ambao ni ubunifu unaolenga kuongeza uwajibikaji wa Watoa huduma za afya pamoja

na kuboresha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuboresha upatikanaji na utumiaji wa huduma za afya nchini na shilingi 5,420,210,425.91 kwa ajili ya mradi wa Maabara ya Jamii ya Afrika Mashariki iliyopo Mabibo Dar es Salaam. Aidha, kwa kipindi cha Aprili - Juni 2020 Wizara inatarajia kupokea kiasi cha jumla ya shilingi 56,194,181,015.32 kutoka Benki ya Dunia. Kiasi cha shilingi 4,250,384,463.04 ni kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya Afya, Shilingi 22,733,830,824.62 ni mchango wa Benki ya Dunia kwenye Mfuko wa Afya wa Pamoja na kiasi cha Shilingi 29,209,965,727 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Malipo kwa Ufanisi (Results Based Financing- RBF)

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na maandalizi ya kutunga sheria ya bima ya afya kwa watu wote. Kwa hivi sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho ikiwa ni pamoja na kukusanya maoni ya wadau kabla ya kuanza kuandaa Muswada wa sheria hiyo.

## RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

**139.** ***Mheshimiwa spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ilifanya uchaguzi wa wanafunzi 25,077 sawa na asilimia 57.2 ya wanafunzi

43,835 waliotuma maombi kujiunga na vyuo vya Afya. Kati yao wanafunzi 5,682 sawa na asilimia 22.7 walichaguliwa kwenye vyuo vya Serikali vya afya na wanafunzi 19,395 sawa na asilimia 77.3 walichaguliwa kwenye vyuo binafsi na taasisi za dini katika program za Uuguzi na Ukunga na Sayansi Shirikishi za Afya. Aidha, katika kuboresha mafunzo na kuhakikisha kwamba rasilimali zilizopo katika eneo moja zinatumika vizuri na mafunzo kutolewa kwa tija zaidi, Wizara imeviunganisha baadhi ya vyuo ambapo vyuo 37 vilivyokuwa katika maeneo ya karibu vimeunganishwa na kuwa vyuo 9. Uamuzi huo umepunguza idadi ya vyuo vya Serikali vya afya kutoka vyuo 77 hadi kufikia vyuo 43. Hatua hii siyo tu itapunguza gharama za uendeshaji wa vyuo bali pia itawezesha ufanisi katika matumizi ya rasilimali ikiwemo watumishi na miundombinu ya majengo.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi katika Sekta ya Afya, ili kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo imefanikiwa kutoa fursa za mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika nyanja mbalimbali za ubingwa na ubobezi, ambapo jumla ya watumishi 550 wameendelea kulipiwa gharama za masomo ya uzamili (postgraduate studies) katika vyuo vikuu vya ndani (531) na

nje ya nchi (19). Katika kipindi hicho jumla ya wataalam bingwa 137 walihitimu mafunzo ya shahada ya uzamili kwa ufadhili wa Serikali ikilinganishwa na wataalam bingwa 82 ambao walihitimu mafunzo hayo mwaka 2018.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kushughulikia suala la ajira za watumishi katika Sekta ya Afya, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuhakikisha Sekta ya Afya inakuwa na watumishi wa kutosha katika kuwahudumia wananchi. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya wataalam 1,817 wa kada mbalimbali waliajiriwa na kupangwa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, Wizara imetangaza nafasi 1,000 za madaktari ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Februari 2020, wakati akizungumza na Madaktari kupitia Chama cha Madaktari Tanzania (MAT).

## MABARAZA YA WANATAALUMA NA BODI ZA USHAURI ZA AFYA

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia utendaji wa wataalam wa Sekta ya Afya. Katika kutekeleza hilo, mabaraza na bodi mbalimbali za kitaaluma ziliundwa kisheria kwa ajili ya kusimamia majukumu hayo.

Mabaraza na bodi za kitaaluma ni pamoja na; Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Macho, Baraza la Radiologia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya (PHLB) na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Mabaraza na bodi hizi zimetekeleza majukumu yafuatayo:-

## Baraza la Madaktari Tanganyika

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Baraza limesajili wanataaluma wa kada mbalimbali kama ifuatavyo; Madaktari na Madaktari wa Kinywa Watarajali *(Provisional Registration)* 1,358; Uhuishaji wa Usajili (*Retention)* wa Madaktari na Madaktari wa Kinywa 572; Usajili wa Kudumu *(Full registration)* Madaktari na Madaktari wa kinywa 415; Usajili wa Muda *(Temporary registration local*) Madaktari 835; na Usajili wa Muda Wageni (*Temporary registration foreigners)* kwa Madaktari 144.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limefanya uhamasishaji katika mikutano ya Medical Association of Tanzania (MAT), Tanzania Dental

Association (TDA) na Chama cha Wafiziotherapia Tanzania (APTA) wa kuanza kutekelezwa kwa Elimu Endelevu ya Kitaaluma (Continuing Medical Education) ifikapo mwaka 2020. Katika kutekeleza hilo, Baraza limeingia makubaliano na Taasisi ya *The World Continuing Education Alliance* ili kurahisisha upatikanaji wa Mafunzo endelevu kwa njia ya mtandao. Aidha, Ofisi ya Msajili imeandaa Mwongozo wa kuratibu Mafunzo hayo endelevu kwa kuwa ni takwa la kisheria ili kuwezesha kuhuishwa kwa leseni ya Kufanya kazi (Practicing licence). Baraza limepokea mashauri ya ukiukwaji wa Taaluma 3 na kwa sasa taratibu za kuyashughulikia zinaendelea.

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania**

**145.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2020, Baraza limetoa usajili wa awali (Provisional Registration) kwa Wauguzi (Watarajali) 840 na wamepangiwa kufanya mazoezi ya vitendo katika vituo 25 ikiwepo Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda, na Baadhi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa. Aidha, Baraza limesajili Wauguzi na wakunga 1,490, kati yao wauguzi 550 ni wa ngazi ya shahada ya kwanza na Wauguzi 940 ni ngazi ya stashahada na astashahada. Jumla ya wauguzi na wakunga wa kigeni 58 (Foreign Nurses and Midwives) wamesajiliwa na kupewa vyeti vya kutoa huduma za uuguzi na ukunga nchini.

**146. *Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia utoaji wa huduma kulingana na taratibu na maadili ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga, Baraza lilipokea tuhuma 11 za ukiukwaji wa maadili kutoka maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za afya. Tuhuma hizo zilifanyiwa kazi na Baraza, na hatimaye wauguzi 7 walikutwa na hatia na kupewa adhabu, ambapo Wauguzi 5 walipewa ONYO, na kufanya kazi chini ya uangalizi kwa mwaka mmoja, wauguzi 2 walisimamishwa kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga kwa muda wa mwaka mmoja, na mwingine miaka miwili (2).

**Baraza la Famasia**

**147. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Baraza lilisajili jumla ya wanataaluma 877 ambapo kati yao Wanataaluma 328 (wafamasia 108, fundi dawa sanifu 206 na fundi dawa wasaidizi 14) walipatiwa usajili wa kudumu, na Wafamasia 549 walipatiwa Usajili wa muda (Provisional Registration). Hivyo, Baraza lina jumla ya wanataaluma 5,200 waliosajiliwa. Katika kipindi hiki, Baraza lilifanya ukaguzi katika majengo 937. Kati ya hayo, 327 ni majengo mapya, na 551 ni maduka ya dawa muhimu yanayotoa huduma. Kati ya maeneo yaliyokaguliwa maeneo 350 yalikidhi vigezo na kuruhusiwa kuendelea na biashara. Maeneo ambayo hayakukidhi vigezo, wamiliki walishauriwa kurekebisha upungufu ulioonekana. Vilevile,

Baraza lilihuisha vibali 1,258 sawa na asilimia 79.2 (vilivyokuwa vinakaribia kuisha muda wake) vya biashara ya famasi kati ya vibali 1,589 zilizosajiliwa na kufuta vibali 46 sawa na asillimia 2.9 vya maduka ya famasi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukiukwaji wa utaratibu wa uendeshaji wa maduka hayo. Vilevile, ilani za kufunga famasi (closure order) ziliandikwa kwa famasi 130.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza pia limeratibu mitihani ya usajili kwa waombaji 1,468 wakiwemo Wafamasia 409, Fundi dawa sanifu 973, Fundi dawa wasaidizi 66 na Watoa dawa 20 wa mwaka mmoja. Kati yao watahiniwa 596 waliofanya mtihani Mwezi Oktoba 2019, watahiniwa 263 walifaulu na 333 hawakufikia viwango vya ufaulu. Watahiniwa waliofaulu wameshapatiwa leseni za utendaji kazi za taaluma na hivi sasa wanatoa huduma katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, matokeo ya watahiniwa 872 waliofanya mtihani Februari 2020, yako kwenye mchakato wa kusahihishwa.

Vilevile, katika kuhakikisha kwamba Wataalam wa dawa (Wafamasia) wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taaluma na maadili, Baraza lilipokea malalamiko ya ukiukwaji wa maadili kwa wanataaluma watatu (3). Mashauri yao yaliwasilishwa na kujadiliwa kwenye Kamati ya maadili na wahusika waliandikiwa barua za ONYO.

## Baraza la Wataalam wa Maabara

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Baraza limetoa leseni kwa wataalam 1,221 na hivyo kuwa na jumla ya wataalam 7,399 waliosajiliwa na kupewa leseni. Kati ya wataalam waliopewa leseni kati ya kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, wataaluma 1,102 walipewa usajili wa awali, na wataalam 119 walipewa usajili wa kudumu. Vilevile, Baraza lilisajili wataalam 80 katika ngazi ya cheti, na wataalam 1,676 wa kada ya afya ambao wanatoa huduma za kimaabara, lakini sio wataalam waliosomea maabara, kwa ajili ya kutoa huduma za upimaji.

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limefanya ukaguzi katika Vyuo vitatu ambavyo ni *Lake College of Health and Allied Science* (Singida), Santa Maria CHAS na *Janesa Institute Health and Allied Science* (JAIHAS) kwa ajili ya kuanzisha kozi ya Maabara kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Vyuo hivyo vilikidhi vigezo na kupewa kibali cha kutoa mafunzo hayo na hivyo sasa kuwepo kwa jumla ya Vyuo 45 vinavyotoa mafunzo hayo. Vilevile, Baraza limewatahini wataalam wa Maabara kwa ngazi ya Astashahada 221 na Stashahada 242 kwa ajili ya usajili wa leseni za kudumu.

## Baraza la Macho Tanzania

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Baraza limesajili jumla ya wataalam 37 wa Optometria na hivyo kufikia jumla ya wataalam 317 waliosajiliwa. Baraza lilifanya ukaguzi shirikishi kwa wataalam 50 na vituo 18 vinavyotoa huduma ya Optometria katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Aidha, Baraza linaendelea kusimamia utoaji wa Elimu Endelevu Kitaaluma (Continuing Professional Development - CPD).

## Baraza la Wataalam wa Radiolojia

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Baraza la wataalam wa Radiolojia nchini limeendelea kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na Wataalamu wa Radiolojia nchini na kuhakikisha kuwa jamii inapata huduma za Radiolojia zilizo bora na salama. Baraza limesajili jumla ya wataalam 368. Kati yao wataalam 128 ni wa Usajili kamili (Full Registration); wataalam 117 ni Usajili wa Matazamio (Provisional); mtaalam mmoja (1) amesajiliwa usajili wa muda (Temporary Reg.); wataalam wanne (4) wameorodheshwa (Enrolment) na wataalam wawili (2) wameandikishwa (Enrolment). Baraza pia limetembelea vyuo viwili vinavyotoa mafunzo ya Diploma (Muhimbili na Bugando) kwa lengo la kutoa elimu juu ya Baraza na miiko na maadili ya kitaaluma.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limefanya ukaguzi shirikishi katika Hospitali za Mikoa ya Manyara, Arusha, na Kilimanjaro; na kutoa elimu juu ya miiko na maadili ya kitaaluma, ili kuwabaini wataalam ambao hawajasajiliwa na kuwapatia fomu za usajili, na wataalam ambao hawajahuisha leseni, kuwapatia *control number* kwa ajili ya malipo. Kupitia ukaguzi huu Baraza limeongeza idadi ya wataalam waliosajiliwa kutoka 219 kwa mwaka 2019 hadi wataalam 368 mwezi Machi, 2020.

**Baraza la Afya Mazingira**

**154.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Baraza limesajili wataalam wapya 152 (Shahada, Stashahada na Astashahada), usajili wa awali 112 (provisional registration), Taasisi zinazotoa huduma za afya mazingira 47 na wataalam waliouhuisha leseni 233. Baraza limeratibu zoezi la ukusanyaji wa maoni kwa ajili ya utengenezaji wa C*ontinuous Professional Development* (CPD) katika vyuo vinavyofundisha Sayansi ya Afya Mazingira nchini ambavyo ni Ngudu, Kagemu, Tanga, Muhimbili, Mpwapwa na RUCU. Vilevile, Baraza limeendelea kuratibu Mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa Shahada ya Sayansi ya Afya Mazingira, ambapo Wahitimu 127 wamemaliza mwezi Novemba 2019 na 112 wanaendelea na mafunzo kwa vitendo (Internship) katika mikoa 26 Tanzania Bara.

## Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala imesajili jumla ya waganga wa tiba asili na tiba mbadala pamoja na wasaidizi wao 23,245 sawa na ongezeko la watoa huduma 1,524; vituo 705 sawa na ongezeko la vituo 283; na dawa za asili 23 sawa na ongezeko la dawa 10. Aidha, katika kipindi hicho Baraza kwa kushirikiana na sehemu ya Tiba Asili na Tiba Mbadala ya Idara ya Tiba imeendelea kusimamia, kuratibu na kuendeleza huduma za tiba asili na tiba mbadala ambazo ni miongoni mwa huduma za afya zinazotolewa hapa nchini. Baraza limeendelea kuratibu mafunzo ya kujiendeleza kwa waganga wa tiba asili yanayotolewa na vyuo vitatu vya afya vya Mirembe, PHN-Morogoro na ITM-MUHAS. Katika mafunzo hayo mafupi ya siku saba jumla ya waganga 65 wamepata mafunzo kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya tiba asili na tiba mbadala pamoja na namna bora za utengenezaji wa dawa za tiba asili na tiba mbadala. Vilevile, jumla ya waganga 41 walipatiwa mafunzo ya utengenezaji wa dawa za asili kwa njia ya vitendo katika wiki ya tiba asili ya Mwafrika.

## Bodi ya Maabara Binafsi za Afya (PHLB)

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya imesajili jumla ya Maabara

Binafsi za Afya 321 na kufikia jumla kuu ya maabara Binafsi za Afya 1905 zilizosajiliwa kote nchini. Aidha, katika kuhakikisha kuwa wamiliki wa maabara binafsi za Afya nchini wanazingatia sheria, kanuni na miongozo, Bodi imefanya ukaguzi shirikishi wa maabara katika wilaya zote za Mikoa ya Dodoma, Mbeya na Songwe na jumla ya maabara 216 zilifikiwa. Katika ukaguzi huo Bodi ilibaini kuwepo kwa baadhi ya maabara zisizo na usajili na zingine muda wa usajili kumalizika, pia kuwepo kwa watendaji wasio wataalam wa maabara ambapo ni mazingira hatarishi kwa wagonjwa, na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria.

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Maabara Binafsi ya Afya pia ilitoa elimu ya ubora wa huduma za maabara, sheria, kanuni za maabara kwa wamiliki na watendaji wa maabara ili kuondoa mazingira hatarishi kwa mgonjwa, kuhakikisha wamiliki wanasajili maabara zao kwa mujibu wa Sheria Na. 10 ya 1997 na kanuni zake kuboresha huduma za maabara na pia kuhuisha leseni zao pindi zinapoisha muda wake. Bodi ya Maabara Binafsi za Afya imeweza kufanya mafunzo kwa waratibu wa huduma za maabara nchini katika wilaya 67 za mikoa Tisa (9) ambayo ni Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Tanga, Mbeya, Songwe, Lindi, Mtwara na Dodoma. Katika mafunzo hayo jumla ya Waratibu wa huduma za Maabara ngazi ya wilaya 67 walipata nafasi ya kujengewa uwezo

kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya Bodi ya Maabara Binafsi za Afya. Aidha, walielimishwa juu ya mbinu za ukaguzi, malipo ya tozo mbalimbali za Bodi kupitia mfumo wa malipo ya Serikali "GePG", maadili ikiwa ni pamoja na kuepuka Rushwa na kutumia lugha zuri kwa wateja kwa lengo la kuboresha huduma za maabara na vipimo kwa ustawi wa umma wa watanzania. **Jedwali Na.6** linaonesha mchanganuo wa wataalam waliosajiliwa na mabaraza ya kitaalam kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020

**Jedwali Na.6: Mchanganuo wa usajili wa wataalam wa huduma za afya uliofanywa na Mabaraza kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020**

| Na | BARAZA | USAJILI (2019/2020) | | | JUMLA KUU (Cumulative) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | MUDA (Provisional) | KUDUMU (Full) | JUMLA NDOGO (2019/20) | |
| 1 | BARAZA LA MADAKTARI | 1,358 | 1,350 | 2,708 | 13,841 |
| 2 | BARAZA LA WAFAMASIA | 549 | 328 | 877 | 5,200 |
| 3 | BARAZA LA WAUGUZI | 820 | 1,490 | 2,310 | 28,150 |
| 4 | BARAZA LA RADIOLOJIA | 114 | 151 | 265 | 1,124 |
| 5 | BARAZA LA OPTOMETRIA | 35 | 2 | 37 | 317 |
| 6 | BARAZA LA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA | 2,255 | 727 | 2,982 | 23,915 |

| Na | BARAZA | USAJILI (2019/2020) | | | JUMLA KUU (Cumulative) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | MUDA (Provisional) | KUDUMU (Full) | JUMLA NDOGO (2019/20) | |
| 7 | BARAZA LA AFYA YA MAZINGIRA | 112 | 152 | 264 | 3,571 |
| 8 | BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA | 1,102 | 119 | 1,221 | 7,399 |
| | **JUMLA KUU** | **6,345** | **4,319** | **10,664** | **83,517** |

**Chanzo:** *WAMJW*

# D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA IDARA KUU YA AFYA (FUNGU 52)

## Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**158.*Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umesajili jumla ya wanachama wapya 364,007 na hivyo kuwezesha Mfuko kuwa na jumla ya wanufaika 4,858,022 sawa na asilimia 9 ya Watanzania wote, ikilinganishwa na wanufaika 3,377,023 mwaka 2015/16. Ili kuongeza wigo wa wanachama katika mfumo wa bima ya afya nchini, Mfuko unatekeleza mikakati mbalimbali ili kufikia lengo hilo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwafikia Wanachama wa Vyama vya Msingi

(AMCOS) vya mazao ya kimkakati kupitia mpango wa Ushirika Afya, kusajili makundi ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na vyuo vinginevyo, wafanyakazi kutoka kwa waajiri wa Sekta Binafsi, wanafunzi wa shule za msingi na Sekondari, makundi ya wajasiliamali ikiwemo Bodaboda, Wamachinga, Baba na Mama Lishe na makundi mengine yenye kufafana na hayo.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwawezesha wananchi wengi zaidi kujiunga katika mfumo wa bima ya afya, Mfuko umeanzisha mpango wa hiari wa vifurushi vya bima ya afya ambavyo vilizinduliwa rasmi mwezi Novemba 2019 Jijini Dar es Salaam. Vifurushi hivi vimeanzishwa kwa kuzingatia gharama halisi za huduma za matibabu nchini, uhitaji wa huduma, ukubwa wa familia pamoja na umri. Ili kutoa nafuu ya uchangia kwa wananchi, Mfuko kwa sasa unakamilisha utaratibu wa kulipa kwa awamu utakaojulikana kwa jina DUNDULIZA. Takwimu za ujumla za usajili wa wanachama na ukusanyaji michango zinaonesha kwamba hadi kufikia Machi 2020, jumla ya wananchi 6,437 wamesajiliwa kwa utaratibu wa hiari na kiasi cha shilingi bilioni 4.93 kimekusanywa kama michango kutoka kwa wanachama hawa. Katika kuhakikisha kwamba wananchi wote wanakuwa na uelewa wa dhana na umuhimu wa kuwa na bima ya afya, Mfuko unaendelea kutekeleza mkakati wa uhamasishaji wa wananchi katika mikoa yote.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha wanachama wa Mfuko kupata huduma za afya wanapozihitaji, Mfuko husajili na kuingia mikataba na vituo vinavyomilikiwa na Serikali, Mashirika ya Dini na watu binafsi. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, vituo vipya 384 vya kutolea huduma za afya nchini vilisajiliwa na kuanza kutoa huduma. Hivyo, hadi kufikia Machi 2020, Mfuko ulikuwa umesajili jumla ya vituo 7,940 kwa ajili ya kutoa huduma ikilinganishwa na vituo 6,439 vilivyokuwa vimesajiliwa mwaka 2015/16.

**161.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa makusanyo, Mfuko umekusanya jumla ya shilingi bilioni 378.31 kama mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali ambapo shilingi bilioni 323.37 zimekusanywa kama michango ya wanachama na waajiri, shilingi bilioni 53.48 kutoka katika vyanzo vya uwekezaji na shilingi bilioni 1.46 kutoka kwenye mapato mengineyo. Katika kipindi husika, jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 353.74 kililipwa kwa watoa huduma za afya waliosajiliwa na Mfuko. Katika malipo hayo, asilimia 37 yalilipwa kwenye vituo vya Serikali, asilimia 28 yalilipwa kwenye vituo vinavyomilikiwa na madhehebu ya dini na asilimia 35 kwa vituo binafsi.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko katika kutekeleza juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano za kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi

wa kati kupitia viwanda, unashirikiana na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) katika ujenzi wa kiwanda Mkoani Simiyu. Kiwanda hicho kinalenga kuzalisha bidhaa za pamba ambazo ni mahitaji muhimu katika utoaji wa huduma za afya katika Hospitali, vituo vya afya na Zahanati. Taarifa ya upekuzi wa teknolojia bora (due diligency report) itakayotumika katika mradi huo iliyofanyika nchini India na China iliwasilishwa kwenye kamati ya mawaziri wenye dhamana ya mradi huu Februari 2020 na kuridhiwa mradi uendelee. Kadhalika, hatua za utangazaji wa zabuni za kupata kampuni itakayotoa teknolojia hiyo imeanza. Kwa sasa mradi upo kwenye hatua ya manunuzi ya kupata kampuni itakayofanya usanifu wa mitambo itakayotumika katika kiwanda hicho.

**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Mamlaka ilifanya tathmini ya maombi 837 ya usajili wa dawa za binadamu kati ya 942 yaliyokuwepo katika kipindi husika. Maombi 572 kati ya maombi yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa na hivyo kusajiliwa. Aidha, maombi manne (4) ambayo hayakukidhi vigezo, wahusika walishauriwa kurekebisha maeneo yaliyokuwa na upungufu. Vilevile, Mamlaka ilipokea maombi 105 ya usajili wa dawa za mifugo ambapo maombi 79

yalifanyiwa tathmini na kati ya hayo maombi 46 yalikidhi vigezo na hivyo kusajiliwa. Maombi 340 ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi yalipokelewa ambapo maombi 270 yalifanyiwa tathimini na kati ya hayo 106 yalikidhi vigezo vya usajili.

**164.** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ilifanyia kazi maombi 632 ya usajili wa maeneo ya biashara ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi kati ya maombi 645 yaliyopokelewa. Maombi 618 sawa na asilimia 98 ya yaliyofanyiwa kazi yalikidhi vigezo na hivyo maeneo husika kusajiliwa na kupewa vibali vya kuanza biashara za bidhaa hizo. Aidha, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa viwanda 15 vya ndani vya uzalishaji dawa ambapo viwanda viwili (2) havikukidhi vigezo vya usajili na hivyo wahusika kupewa maelekezo ya kuboresha viwanda hivyo ili viweze kusajiliwa. Vilevile, maeneo 5,045 yanayojihusisha na biashara ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi yalifanyiwa ukaguzi ambapo maeneo 3,931 sawa na asilimia 77.9 yalikidhi vigezo.

**165.** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya sampuli 1,145 kati ya sampuli 1,435 za bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi zilichunguzwa ambapo sampuli 1,134 sawa na asilimia 98.6 zilikidhi vigezo. Bidhaa ambazo sampuli zake hazikukidhi vigezo hazikusajiliwa na nyingine kuondolewa kwenye soko kwa njia ya ukaguzi. Kiwango cha asilimia 99 cha bidhaa za dawa,

vifaa tiba na vitendanishi zilizokidhi vigezo kwa kipindi hiki, kinaashiria uhakika wa uwepo wa bidhaa bora na salama kwenye soko kwa watumiaji. Katika kulinda afya za watumiaji wa bidhaa za dawa, Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa tani 15,105.84 za bidhaa za dawa na vifaa tiba zenye thamani ya takriban shilingi bilioni 6.67 kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka iliendelea kudhibiti ubora wa bidhaa za dawa, vifaa na vifaa tiba vinavyoingizwa au kusafirisha nje ya nchi. Katika kipindi hicho, jumla ya maombi 7,463 ya kuingiza nchini bidhaa za dawa, vifaa na vifaa tiba, vitendanishi na malighafi ya kutengeneza dawa nchini yalipolewa na kufanyiwa tathmini ambapo maombi 7,389 sawa na asilimia 99 yalikidhi vigezo. Aidha, Mamlaka ilipokea na kufanyia kazi jumla ya maombi 379 ya kusafirisha nje ya nchi bidhaa za dawa na vifaa tiba ambapo maombi 372 sawa na asilimia 98 yalikidhi vigezo na hivyo kuidhinishwa.

### Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Mamlaka ilipokea jumla ya sampuli 52,917 kwa ajili ya uchunguzi

wa Kimaabara unaojumuisha maswala ya kijinai na kijamii, maji, maji taka, kemikali, vyakula, dawa na bidhaa nyingine za viwandani. Sampuli zilizochunguzwa ni 52,249 sawa na asilimia 98.7. Vilevile, Wizara kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilifanya matengenezo kinga ya vifaa na mitambo na kununua vitendanishi ambavyo vimesaidia kufanya uchunguzi, kutoa matokeo sahihi na kwa wakati hivyo kulinda afya na mazingira na kusaidia utoaji haki katika vyombo vya maamuzi. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepokea na kuitikia wito wa mahakama kwenye jumla ya kesi 1,278 kwa lengo la kutoa ushahidi wa kitaalam (expert opinion) na ambao umeisaidia vyombo mbalimbali vya kimaamuzi kutekeleza majukumu yao kwa wakati.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imekamilisha ununuzi wa mitambo mitano (5) uliogharimu jumla ya shilingi 1,054,246,616. Mitambo iliyonunuliwa ni *Atomic Absorption Spectroscopy (AAS), High Performance Liquid Chromatography (HPLC), X-Ray Diffraction (XRD), Cyanide Analyser na Kjeldah Digester* ambayo inatumika kwa ajili ya uchunguzi wa sampuli mbalimbali zikiwemo sampuli za Makosa ya jinai, dawa za kulevya, vyakula na dawa. Mitambo hii inaweza kufanya utambuzi katika viwango vya juu kabisa kwa sampuli mbalimbali na kutoa majibu kwa usahihi.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Mamlaka imeweza; kusajili wadau wa kemikali 468 sawa na asilimia 93.6 ya lengo la kusajili wadau wa kemikali 500, kukagua maghala ya kuhifadhia kemikali yapatayo 1,341 sawa na asilimia 79.3 ya lengo la kukagua maghala 1,691 na kutoa vibali 23,926 vya kuingiza na kusafirisha kemikali nchini ukilinganisha na kusajili wadau 19,118 kwa kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Pia, Mamlaka imefanikiwa kutoa mafunzo kwa wadau wanaojishughulisha na masuala ya kemikali wapatao 1,220 ambayo ni sawa na asilimia 83.5 ya lengo la 1,461. Wadau hao walielimishwa juu ya Sheria, Taratibu na Kanuni zinazohusiana na usalama wa kemikali za viwandani na majumbani na ukaguzi wa kemikali. Mafunzo hayo kwa Wadau wa kemikali yameimarisha utekelezaji wa sheria na kuepusha madhara ambayo yangeweza kutokea kwa afya ya binadamu na mazingira nchini.

**Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)**

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi hii inajukumu la kufanya tafiti zinazohusu magonjwa ya binadamu. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Taasisi iliendelea

kutekeleza tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Utafiti wa Tiba ya Tahadhari ya MALARIA kwa Wajawazito; Utafiti wa KIFUA KIKUU unafualitilia mwenendo wa ugonjwa wa Kifua Kikuu na viashiria vya madhara ya muda mrefu ya kifua kikuu cha mapafu na athari zake kwa afya ya umma (TB Sequel project); Utafiti wa EXIT TB: unaohusu kutafsiri matokeo ya utafiti kwenda katika Sera na kuboresha utendaji kwenye huduma za vipimo na matibabu ya kifua kikuu; Utafiti wa Magonjwa yasiyoambukiza (NCD) unaoangalia Kisukari na matatizo mengine ya afya yanayoambatana na ugonjwa wa UKIMWI (CICADA study); Utafiti unaoangalia hatari ya maambukizi ya UKIMWI kutokana na maambukizi ya minyoo; Utafiti unaohusu Majaribio ya Tiba kinga dhidi ya TB iliyojificha (Latent TB) kwa wagonjwa wa Kisukari (PROTID Project). Kwa ujumla, muda wa kukamilika kwa tafiti zinazoendelea ni kati ya mwaka mmoja hadi mitano ambapo Taasisi imejipanga kutoa matokeo pindi hizo zitakapokamilika.

**171.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ilipokea na kuratibu tathmini za maadili na usalama maombi ya tafiti 296. Katika maombi haya, zaidi ya asilimia 35 ya tafiti hizi zililenga kwenye Mifumo ya afya, asilimia 15 magonjwa yasiyoambukiza, asilimia 14 UKIMWI, asilimia 8 malaria na asilimia 5 kifua kikuu. Maeneo mengine ambayo katika kipindi hiki yameonekana kufanyiwa

utafiti ni pamoja na mama na mtoto, magonjwa ya kuhara na kipindupindu, viashiria vya afya vya jamii (Social Determinants of Health), pamoja na mabadiliko ya tabia.

**172.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi kupitia Bohari ya Dawa (MSD) inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kiwanda na Maabara ya Dawa za Asili Mabibo ambao upo kwenye hatua za manunuzi ya mitambo. Tayari Bohari ya Dawa (MSD) na wazabuni wameshasaini mikataba ya ununuzi wa mitambo. Mitambo ya kuzalisha dawa inatarajiwa kuanza kufungwa Mabibo mwishoni mwezi Mei, 2020.

## E. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU CHINI YA IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII (FUNGU 53)

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, utekelezaji wa majukumu ya Wizara (Fungu 53) ulijikita katika maeneo yafuatayo:-

### Ushiriki wa Jamii katika Shughuli za Maendeleo

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu dhana ya **ushirikishaji wananchi katika shughuli za maendeleo** ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia nguvukazi pamoja na rasilimali

zinazowazunguka katika maeneo yao. Miradi hiyo ni: Ukarabati wa jiko linalowezesha wanafunzi 470 kupata huduma ya lishe katika Shule ya Msingi Mnyigumba, Kijiji cha Kitelewasi, Kata ya Rungemba Wilaya ya Mufindi. Ukarabati huo uligharimu kiasi cha shilingi 3,622,000; na Kupaua jengo la mashine ya kukamua alizeti kwa ajili ya kuchangia juhudi za kuinua kipato cha kikundi cha wasichana ambao hawakubahatika kuendelea na elimu ya Sekondari katika Kata ya Kising'a Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi 3,098,000 kimetumika.

**175.** ***Mheshimiwa Spika***, aidha, wananchi wameendelea kuhamasishwa kushiriki katika ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa na ofisi 1 katika Shule ya Sekondari ya Utengule iliyopo Tarafa ya Mbalizi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Ujenzi huo utagharimu kiasi cha shilingi 156,031,320 hadi kukamilika. Hadi Machi, 2020, wananchi na wadau wameweza kuchangia kiasi cha shilingi 13,399,000. Wananchi pia kwa kushirikiana na Vikundi 52 vya Wanawake Wahandisi wameweza kushiriki katika ujenzi wa madaraja ya gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi katika Kijiji cha Manda, Wilaya ya Ludewa Mkoani Njombe; na Ujenzi wa Zahanati ya Lembeni iliyopo Wilaya ya Mwanga katika Mkoa wa Kilimanjaro. Jumla ya madaraja 7 yamejengwa ambayo yamegharimu kiasi cha shilingi 62,000,000.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utendaji wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zote nchini ili kusimamia shughuli za maendeleo ya jamii ikiwemo kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara imefanikisha Mkutano wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Mkutano huo ulijumuisha wataalam wa maendeleo ya jamii 402 kutoka ngazi za Wizara, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali uliofanyika mwezi Oktoba, 2019 Mkoani Dodoma. Washiriki walijengewa uwezo wa kiutendaji utakaowawezesha kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza **Kampeni ya ujenzi wa nyumba bora kwa gharama nafuu zinazotumia teknolojia rahisi.** Kampeni hii yenye Kaulimbiu "***Piga Kazi: Boresha Makazi"*** imelenga kupunguza kaya zenye makazi duni kwa asilimia 50 kutoka asilimia 15.9 ya sasa hadi kufikia asilimia 8 ifikapo mwaka 2022 katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Katika kuhakikisha kampeni hii inafanikiwa, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uhamasishaji Ujenzi wa Nyumba Bora Ngazi ya Jamii na kusambaza kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata, Wilaya na Mkoa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara. Kampeni imelenga kutokomeza makazi duni katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ifikapo mwaka 2022.

**178.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia kampeni hii, wananchi wamehamasishwa kujenga nyumba bora 751 katika mikoa ya Pwani, Katavi, Singida na Mwanza. Katika Mkoa wa Pwani nyumba 220 zimejengwa, Mkoa wa Katavi nyumba 445, Mkoa wa Singida nyumba 27 na Mkoa wa Mwanza nyumba 59 zimejengwa kwa kushirikiana na Shirika la Kivulini. Ujenzi wa nyumba bora moja unagharimu kiasi cha shilingi 9,500,000 hadi shilingi 12,579,330 kwa nyumba yenye vyumba vitatu, sebule, choo na jiko kwa kutegemea aina ya ujenzi katika eneo husika. *Nitumie Bunge lako tukufu kuwashukuru na kuwapongeza wananchi kwa kujitolea katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Ni matumaini yangu kuwa, wataendelea kujitokeza kutekeleza miradi mbalimbali ya jamii na mtu mmoja mmoja katika maeneo yao. Serikali itaendelea kutambua na kuthamini mchango wa wananchi katika kutekeleza miradi ya maendeleo*.

**Mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii**

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia **utoaji wa mafunzo kwa kada ya Maendeleo ya Jamii** kupitia Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii vya; Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli. Katika mwaka 2019/20, jumla ya wanafunzi 3,986 (Me 1,548 na Ke 2,438) walidahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 2,015 (Me 757 na Ke 1,258) waliodahiliwa mwaka 2015/16. Aidha, katika mwaka 2018/19, jumla

ya wanafunzi 5,564 (Me 1,853 na Ke 3,711) walihitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ikilinganishwa na wanafunzi 3,434 (Me 1,353 na Ke 2,081) waliohitimu mwaka 2015/16 sawa na ongezeko la asilimia 62 la wahitimu.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mafunzo ya maendeleo ya jamii nchini, Wizara imefanya ufuatiliaji wa taaluma ya maendeleo ya jamii ngazi ya Cheti na Stashahada kwenye vyuo vya umma na binafsi 10 vinavyotoa taaluma hiyo. Lengo la ufuatiliaji ni kukagua ubora wa mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivyo. Aidha, Vyuo 11 vya Umma na Binafsi vimepatiwa mafunzo ya namna ya kutumia mtaala wa maendeleo ya jamii. Vyuo hivyo ni; Mwalimu Nyerere Memorial Academy Dar es Salaam Campus, Mwalimu Nyerere Memorial Academy Karume Campus Zanzibar, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (Umma), KAPS Mafinga, KAPS Mbeya, Masoka Professionals Training Institute Moshi (kwa sasa Saint Stefano), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhemba, Tandabui Institute of Health Science and Technology, Amani College of Technology and Management - Njombe na Tusaale Business Planning Mafinga Iringa (Binafsi). Mafunzo ya matumizi ya mtaala huo yanaendelea kutolewa kwa vyuo vingine vilivyobaki.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuibua na kukuza mawazo na vipaji vya wanafunzi na jamii inayozunguka Vyuo vya Maendeleo ya

Jamii, **Vituo 7 vya Kidigitali vya Ubunifu** vimeanzishwa kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Monduli, Rungemba, Buhare, Ruaha, Misungwi, Uyole na Mlale. Vituo hivi vitawezesha kuibua na kukuza mawazo na vipaji vya kibunifu miongoni mwa wanafunzi na jamii ili waweze kuchangia katika maendeleo ya Taifa kwa kuzalisha teknolojia zinazohitajika katika maendeleo ya viwanda, usindikaji wa mazao na bidhaa mbalimbali ili kuongeza mnyororo wa thamani.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza **Dhana ya Uanagenzi** kupitia Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii (CDTIs) ili kuzalisha wahitimu wenye weledi na umahiri unaoendana na soko la ajira na watakaoweza kujiajiri. Katika mwaka 2019/20, Wizara imeanzisha Programu za Uanagenzi ambapo wanafunzi na wahitimu wa Taaluma ya Maendeleo ya Jamii watawezeshwa kupata ujuzi wa kujiajiri. Hadi kufikia Machi 2020, jumla ya Taasisi, Kampuni, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mashirika ya Umma 201 yatakayowachukua wanafunzi na wahitimu kwa ajili ya kupata ujuzi yametambuliwa. Utaratibu huu unatarajiwa kuwezesha idadi kubwa ya wanafunzi na wahitimu kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kunufaika na programu hii kwa namna mbalimbali ikiwemo kupata ajira za kudumu.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kwa kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu. Katika mwaka 2019/20, ukarabati umefanyika kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya: Ruaha (bweni na choo kimoja); Misungwi (vyoo, mabafu, miundombinu ya umeme, bweni la wanaume, bwalo na Kituo cha Kidigitali cha Ubunifu); Monduli (nyumba nne za watumishi, bweni la wasichana, maktaba na kuzungushia ukuta choo cha wasichana); na Uyole (ujenzi wa Maktaba). Ukarabati huo umefanyika kwa kutumia kiasi cha shilingi 142,230,200.

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii imeendelea kutekeleza dhana ya ushirikishaji jamii kama ifuatavyo:-

(i) Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli kimetoa elimu ya ujasiriamali, ufugaji (nyuki, kuku) kwa vikundi vitatu vya akiba na mikopo vya vijana kutoka Vijiji vya Eluwai, Einguiki na Emairete (Arusha) ambapo kila kikundi kimeanzisha VICOBA na kufanikiwa kuwa na mtaji kwa mchanganuo ufuatao; Eluwai shilingi 146,000, Enguki shilingi 122,000 na Emairete shilingi 152,000;

(ii) Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole kupitia tathmini shirikishi iliyofanyika Mtaa wa Itanji Kata ya Iganjo (Mbeya) ilibaini kuwa kati ya nyumba 327 zilizotembelewa, nyumba 51 tu zilikuwa na vyoo bora. Chuo kilihamasisha ujenzi wa vyoo bora ambapo vyoo 52 vimejengwa na kufikia vyoo bora 103. Thamani ya ukarabati kwa choo kimoja ni shilingi 320,000; na

(iii) Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba kimetoa mafunzo ya kuandaa chakula bora na unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa washiriki 240 katika vitongoji viwili vya kijiji cha Rungemba na Itimbo (Iringa) ili kutatua changamoto ya lishe. Elimu ya lishe pia imetolewa kwa wanafunzi 400 katika shule ya msingi Mnyigumba na wanafunzi 250 Shule ya Sekondari Mnyigumba. Ili kuongeza kipato cha jamii, Chuo kimetoa mafunzo kwa vitendo kuhusu uoteshaji wa miche ya parachichi kwa washiriki 64 katika Kijiji cha Itimbo ambapo jumla ya miche 1,000 imeoteshwa. Aidha, mafunzo kwa vitendo kuhusu uboreshaji wa vyakula kwa kuongeza virutubishi yametolewa kwa akinamama katika Kijiji cha Kitelewasi (Iringa).

### Haki na Maendeleo ya Mtoto

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea **kuratibu na kusimamia utoaji wa haki za mtoto** zikiwemo **haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushiriki na kutobaguliwa.** Wizara kwa kushirikiana na wadau imetekeleza afua mbalimbali zinazohusu ulinzi na usalama wa mtoto kwa lengo la kuzuia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto visitokee na kushughulikia matukio ya ukatili dhidi ya watoto yanapotokea katika jamii. Hadi kufikia Machi 2020, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imewezesha uanzishwaji wa **Madawati 10 ya Jinsia na Watoto** katika vituo vya Polisi vya Mbweni, Kimara, Mburahati, Kakonko, Kibondo, Kigoma Central, Mugumu Serengeti, Kiabakari na Butiama. Idadi ya madawati imeongezeka kutoka madawati 417 mwaka 2015/16 na kufikia madawati 427 Machi, 2020. Uwepo wa Madawati haya umewezesha kuongezeka kwa utoaji wa taarifa za matukio ya ukatili dhidi ya watoto kutoka matukio 10,551 mwaka 2016 hadi kufikia matukio 15,680 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 49. Aidha, jumla ya Maafisa Polisi 84 wanaohudumia Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo hivyo walipatiwa mafunzo ya kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea **kuelimisha jamii kuhusu athari za mila, desturi na tamaduni zenye madhara** zinazosababisha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto nchini. Elimu hiyo ilitolewa kwa wananchi 875 katika mikoa ya Mara, Geita, Tanga, Rukwa, Mbeya na Kigoma ikiwahusisha walimu 78, wanafunzi 790, Viongozi wa kisiasa 23, viongozi wa dini 16, viongozi wa kimila 40 na watangazaji wa radio jamii 6. Aidha, ujumbe maalum kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari za ukatili wa mtandaoni kwa watoto zimeandaliwa na kufanyiwa majaribio ya matumizi kwa jamii katika mkoa wa Iringa ambapo wanafunzi 120 na wazazi 60 walishiriki na kutoa maoni ya namna bora ya kufikisha ujumbe huo kwenye jamii.

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea na **kampeni ya kutokomeza mimba na ndoa za utotoni** katika mikoa ya Shinyanga, Mara, Tabora, Singida, Rukwa, Tanga na Dodoma na jumla ya wanafunzi 8,978 katika shule za msingi na wanafunzi 345 katika shule za sekondari pamoja na walimu 40 walifikiwa na kupata uelewa kuhusu madhara ya mimba na ndoa za utotoni kiafya, kielimu na kiuchumi.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua umuhimu wa mazingira salama kwa watoto wanapokuwa shuleni kwa vile shule ni sehemu inayotumiwa na watoto kupata maarifa na

taaluma mbalimbali zinazowawezesha kuwa wataalam wa baadaye. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Wizara na wadau imetekeleza afua mbalimbali kukabiliana na vitendo hivyo. Afua hizo ni pamoja na kutoa mafunzo ya malezi chanya kwa walimu 12,370, ushauri na unasihi kwa walimu 37,878 katika shule za msingi 14,900 na sekondari 4,039. Kupitia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ijulikanayo kama **"TWENDE PAMOJA: UKATILI TANZANIA SASA BASI"** niliyoizindua tarehe 08/03/2019, jumla ya madawati 25 ya ulinzi wa watoto yameanzishwa katika Shule 17 za Msingi na Shule 8 za Sekondari katika Halmashauri za Mkoa wa Rukwa.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) ikiwa ni sehemu ya makubaliano ambayo nchi yetu iliingia na Umoja wa Mataifa mwaka 1989. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali imeandaa Taarifa ya 6 ya Nchi kuhusu Utekelezaji wa Mkataba huu inayoeleza hali halisi ya utoaji haki za mtoto, mafanikio yaliyopatikana katika kukuza ustawi na haki za mtoto na kubainisha mifano bora inayofaa kuigwa katika afua za kuimarisha upatikanaji wa haki za watoto pamoja na kueleza changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa afua za haki za mtoto hapa nchini.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea **kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22)** na kuwezesha uanzishwaji wa Kamati 7,496 za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika ngazi mbalimbali za Vijiji/Mitaa, Kata, Halmashauri na Mikoa. Lengo la Kamati hizi ni kuimarisha ulinzi na usalama wa wanawake na watoto katika jamii na kuwa chombo muhimu cha kuimarisha na kufuatilia mashauri ya vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Aidha, uanzishaji wa kamati umeongezeka kutoka Kamati 7,316 mwaka 2017/18 hadi kufikia Kamati 16,343 Machi, 2020.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha **ustawi na maendeleo ya familia nchini,** Wizara imetoa mafunzo ya malezi chanya kwa wazazi na walezi 110,805 kwenye ngazi ya familia katika Mikoa 23 ya Kilimanjaro, Kigoma, Shinyanga, Katavi, Kagera, Songwe, Ruvuma, Mwanza, Mbeya, Iringa, Mara, Tabora, Dodoma, Singida, Dar es Salaam, Geita, Morogoro, Lindi, Tanga, Shinyanga, Rukwa, Pwani na Mtwara. Aidha, elimu hiyo imewezesha kuanzishwa kwa vikundi vya malezi 2,777 mwaka 2019/20 ikilinganishwa na vikundi 1,186 vilivyoundwa mwaka 2018/19. Kati ya vikundi vilivyoundwa, vikundi 2,384 vimeshaanza kutoa elimu ya malezi katika jamii husika. Tangu kuanza kutekelezwa kwa programu hii, jumla ya vikundi

vya malezi 3,963 vimeanzishwa katika Mikoa mbalimbali hapa nchini.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vikundi hivi vimekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha na kuhimiza malezi chanya kwa familia na jamii katika maeneo yao na kuanzisha miradi ya kiuchumi ikiwemo ya kilimo ambapo mapato hutumika kuboresha hali ya lishe na afya kwa watoto katika jamii na kuhamasisha jamii kutoa misaada kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kutoa mchango wa chakula kwa watoto katika shule.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika Lisilo la Kiserikali la C-SEMA imeendelea kutoa **huduma kwa watoto waliofanyiwa ukatili kupitia Huduma ya Simu kwa Watoto Na. 116 (Child Help Line).** Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya simu 3,044 za matukio ya ukatili dhidi ya watoto zilishughulikiwa ambapo watoto walipatiwa huduma mbalimbali zikiwemo za chakula, vifaa vya shule, unasihi, huduma za sheria, malazi na afya. Aidha, idadi ya watoto waliopata huduma kupitia Huduma ya Simu kwa Watoto Na. 116 imeongezeka kutoka watoto 493 mwaka 2015/16 hadi kufikia watoto 6,877 Machi, 2020.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua na kuheshimu haki ya watoto ya kushiriki katika ajenda zao za maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara imewezesha **ushiriki wa watoto** katika ajenda zao za maendeleo kupitia Mabaraza ya Watoto 1,669 yaliyoanzishwa katika ngazi ya Taifa, Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji/ Vitongoji. Aidha, kupitia mkutano wa Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanyika Jijini Mwanza Novemba, 2019 na kuwahusisha jumla ya wawakilishi 40 wa watoto kutoka mikoa 30 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Watoto walipata fursa ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wao na kukusanya maoni kuhusu masuala ya vipaumbele yanayohusu watoto kuelekea kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka 2020 ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa upatikanaji wa huduma za afya hususan kwa watoto walio katika mazingira hatarishi pamoja na kuwajengea watoto uelewa kuhusu mbinu za kukabiliana na vitendo vya ukatili.

**Uwezeshaji kwa Vijana Balehe**

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha **Vijana Balehe Kujikinga dhidi ya VVU na UKIMWI,** Wizara imeendelea kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Wizara imetoa elimu kwa **wanafunzi 34,954**

katika Halmashauri za Wilaya 10 za mikoa ya Dodoma, Singida na Morogoro ambapo kati yao, wanafunzi 28,574 walitoka katika shule za msingi na wanafunzi 6,380 shule za sekondari pamoja na walimu 230 kutoka shule 50 (shule za msingi 30 na shule za sekondari 20). Aidha, watumishi na viongozi 184 walipewa elimu kuhusu ujumbe wa kuwakinga vijana balehe dhidi ya maambukizi ya VVU ambapo watumishi 7 walitoka Sekretarieti ya Mkoa, watumishi 63 kutoka kwenye Halmashauri, watu mashuhuri 30, viongozi wa siasa 40 na viongozi wa dini 44 kutoka katika Halmashauri za mikoa ya Singida, Morogoro na Dodoma.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa elimu kuhusu madhara ya VVU/UKIMWI inawafikia idadi kubwa zaidi ya vijana balehe, Wizara ilitoa elimu kwa umma kwa kurusha taarifa zinazohusu athari za VVU/UKIMWI kupitia vipindi na mahojiano katika vituo mbalimbali vya habari vikiwemo Standard Radio (Singida) na Abood Radio (Morogoro) na Rasi FM (Dodoma), ITV na Channel Ten.

## Watoto Walio katika Mkinzano na Sheria

**197.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa huduma za ustawi wa jamii katika **mahabusu 5 za watoto** za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Mahabusu hizi zinatoa huduma za msingi ikiwa ni pamoja na malazi, chakula na unasihi wakati wakiendelea

kuhudhuria mashauri yao Mahakamani. Katika mwaka 2019/20, watoto 138 (wavulana 120 na wasichana 18) waliwezeshwa kupata huduma hizi ikilinganishwa na watoto 386 (wavulana 37 na wasichana 349) waliopata huduma mwaka 2018/19 sawa na upungufu wa asilimia 64 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 7.**

**Jedwali Na. 7: Mwenendo wa Watoto walio katika Mahabusu za Watoto**

| Mwaka | Wavulana | Wasichana | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2015/16 | 349 | 37 | **386** |
| 2016/17 | 237 | 18 | **255** |
| 2017/18 | 278 | 13 | **291** |
| 2018/19 | 320 | 34 | **354** |
| 2019/20 | 120 | 18 | **138** |

**Chanzo:** *WAMJW*

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa, **huduma za msingi, elimu na mafunzo zinaendelea kutolewa kwa watoto waliobainika kufanya makosa ya jinai** waliopo katika Shule ya Maadilisho Irambo Mbeya. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, watoto 32 waliobainika kufanya makosa ya jinai walipatiwa amri ya Mahakama kwenda Shule ya Maadilisho. Idadi ya watoto katika Shule ya Maadilisho Irambo imeongezeka kutoka watoto 152 mwaka 2015/16 hadi watoto 366 Machi, 2020. Shule hii inatoa huduma ya marekebisho ya tabia kwa watoto na kuwapatia ujuzi ili wanapokamilisha hukumu zao waweze kujitegemea na kuwa raia wema.

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za marekebisho ya tabia kwa watoto Wizara kwa kushirikiana wadau inatekeleza Programu ya Marekebisho ya Tabia kwa Watoto waliopatikana na makosa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Lengo la programu hii ni kuwachepusha watoto waliopatikana na makosa mbalimbali hususan makosa ya jinai kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na huduma za unasihi, mafunzo ya ufundi na Sanaa. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, watoto 148 (wavulana 89 na wasichana 59) walichepushwa. Programu hii imewezesha watoto waliopata huduma ya marekebisho ya tabia kuongezeka kutoka watoto 91 mwaka 2015/16 hadi watoto 501 Machi, 2020.

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara imetoa mafunzo kwa Maafisa 140 wa Mahakama za Watoto wakiwemo Maafisa Ustawi wa Jamii 39, Mawakili 6, Waendesha Mashtaka 16, Mahakimu 62 na Wanasheria 17 kutoka Mikoa ya Kilimanjaro, Geita na Simiyu kuhusu namna bora ya kuendesha mashauri ya watoto katika mahakama za watoto. Lengo la mafunzo haya ni kuboresha uendeshaji wa mashauri ya watoto katika Mahakama za Watoto zilizopo katika mikoa 24 ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Kagera, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Iringa, Njombe, Mtwara, Dar es Salaam, Lindi,

Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Mara, Geita, Songwe, Rukwa, Tabora, Kigoma na Tanga. Aidha, hadi Machi 2020, Mahakama za Watoto saba zimeanzishwa. Uanzishwaji wa mahakama za watoto umeongezeka kutoka Mahakama 3 mwaka 2015/16 hadi Mahakama 141 nchi nzima. Vilevile, jumla ya watoto 737 walihudumiwa katika mahakama za watoto nchini ambapo watoto 516 (wavulana 217 na wasichana 299) waliachiwa huru na watoto 221 (wavulana 93 na wasichana 128) walikutwa na hatia.

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa **huduma za sheria na marekebisho ya tabia kwa watoto** walio katika mkinzano na sheria kupitia Mahakama za Watoto. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya **watoto 1,087** walihusika na ukinzani wa sheria. Kati yao, watoto wa kiume 757 sawa na asilimia 70 ndiyo walioongoza katika uvunjaji wa sheria. Watoto walipatiwa huduma mbalimbali ikiwemo marekebisho ya tabia, unasihi, msaada wa kisaikologia na kisheria wakati wanapoendelea na mashauri yao.

### Huduma ya Malezi ya Kambo na Kuasili

**202.** ***Mheshimiwa Spika***, **huduma za malezi ya kambo na kuasili** zimeendelea kutolewa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi hususan watoto wasio na wazazi, walezi au

ndugu. Huduma hii inalenga kuhakikisha watoto wanalelewa katika malezi ya familia ya kudumu. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, watoto 13 (wavulana 6 na wasichana 7) walipata huduma ya kuasili na watoto 24 (wavulana 12 na wasichana 12) walipata huduma ya malezi ya kambo. Watoto waliopata huduma ya kuasili wameongezeka kutoka watoto 28 mwaka 2015/16 hadi kufikia watoto 95 Machi, 2020 na watoto waliopata huduma ya malezi ya kambo wameongezeka kutoka watoto 57 mwaka 2015/16 hadi kufikia watoto 217 Machi, 2020 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 8**.

**Jedwali Na. 8: Mwenendo wa Watoto Waliopata Huduma ya Malezi ya Kambo na Kuasili**

| Mwaka | Malezi ya Kambo | | | Kuasili | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ke | Me | Jumla | Ke | Me | Jumla |
| 2015/16 | 31 | 26 | 57 | 9 | 19 | 28 |
| 2016/17 | 21 | 33 | 54 | 11 | 10 | 21 |
| 2017/18 | 24 | 20 | 44 | 9 | 8 | 17 |
| 2018/19 | 22 | 16 | 38 | 8 | 8 | 16 |
| 2019/20 | 12 | 12 | 24 | 7 | 6 | 13 |
| **Jumla** | **110** | **107** | **217** | **44** | **51** | **95** |

**Chanzo:** *WAMJW*

**203.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaratibu **huduma ya Mtu/Familia ya Kuaminika** ambayo hutolewa kwa watoto wanaohitaji malezi ya muda. Watoto hao, hujumuisha watoto waliopotea, waliofanyiwa ukatili, watoto waliounganishwa na programu ya marekebisho ya tabia na waliotelekezwa. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Watu wa


Kuaminika 33 walitambuliwa na kupewa mafunzo hadi kufikia Watu wa Kuaminika 295 nchi nzima. Kupitia programu hii, idadi ya watoto waliolelewa na Watu wa Kuaminika imeongezeka kutoka watoto 243 mwaka 2017/18 hadi kufikia watoto 527 Machi, 2020.

### Huduma kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi

**204.** ***Mheshimiwa Spika***, utoaji huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaoishi kwenye makao ya watoto ni eneo lililopewa kipaumbele na Serikali. Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za Dini, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Binafsi imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za msingi za malazi, chakula, malezi, mavazi, ulinzi, matibabu na elimu kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaoishi katika makao ya watoto nchini. Jumla ya watoto 15,365 (wavulana 8,270 na wasichana 7,095) walipatiwa huduma za msingi katika makao ya watoto mwaka 2019/20 kama inavyoonesha katika Kielelezo Na. 1. Kati ya watoto walio katika mazingira hatarishi, watoto 75 (wavulana 33 na wasichana 42) walipatiwa huduma za msingi kwenye Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini yanayomilikiwa na Serikali mwaka 2019/20, ikilinganishwa na watoto 71 (wavulana 38 na wasichana 33) waliopata huduma mwaka

2018/19. Idadi ya watoto wanaopata huduma katika Makao ya Watoto imeongezeka kutoka watoto 4,379 mwaka 2015/16 hadi kufikia watoto 15,365 Machi, 2020. *Nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa jamii kuzingatia misingi na utamaduni wa kitanzania wa kuwajibika kutoa malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto, ili kuepusha watoto kulelewa katika Makao ya Watoto.*

**Kielelezo Na. 1:** Mwenendo wa Watoto Wanaoishi katika Makao ya Watoto ya Serikali na Binafsi




**Chanzo:** *Makao ya Watoto Yanayomilikiwa na Serikali na Binafsi*

**205.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi, Serikali imeendelea kutoa leseni za usajili kwa kuzingatia sheria, kanuni,

taratibu na miongozo. Kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, leseni 35 za usajili wa makao ya watoto zimetolewa. Usajili wa makao ya watoto umeongezeka kutoka makao ya watoto 130 mwaka 2015/16 na kufikia makao ya watoto 178 Machi, 2020 ambapo Makao moja yanamilikiwa na kuendeshwa na Serikali (Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini).

**206.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya STANBIC imeendelea kuwezesha huduma ya afya kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Katika mwaka 2019/20, Wizara imewapatia watoto 350 wanaoishi katika mazingira hatarishi kadi za bima ya afya katika Jiji la Dodoma ikilinganishwa na watoto 992 waliopatiwa kadi za bima ya afya kutoka mikoa mitano ya Dar es Salaam, Mbeya, Kilimanjaro, Mwanza na Arusha mwaka 2018/19.

**207.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za msingi kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, imewatambua jumla ya watoto 2,398,354 walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Watoto hawa wamepatiwa huduma mbalimbali ikiwemo chakula, malazi, mavazi, matibabu, vifaa vya

shule, ada, ujuzi na huduma za msaada wa kisaikolojia na kuwaunganisha na familia zao. *Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote kuwatambua watoto, kutafuta familia zao na kuwaunganisha na familia zao.*

**Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto**

**208.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha **huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto** kwa kusimamia utoaji wa huduma zinazotolewa katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya vituo 125 vya kulelea watoto wadogo mchana vimesajiliwa na kufikia jumla ya vituo 1,543 vilivyosajiliwa nchi nzima. Kupitia vituo hivi, jumla ya watoto 159,479 (wasichana 76,940 na wavulana 82,539) waliandikishwa katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ikilinganishwa na watoto 149,093 walioandikishwa katika vituo mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 7. Takwimu zinaonesha uandikishaji wa watoto katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana unaongezeka kila mwaka kutoka watoto 67,997 mwaka 2015 hadi kufikia uandikishaji wa watoto 159,479 mwaka 2019.

Aidha, jumla ya vituo 33 vya kulelea watoto wadogo (Crèches) wa chini ya miaka miwili vimesajiliwa. *Natumia fursa hii kuwahamasisha wananchi wote kuwaandikisha watoto wao katika vituo hivi ambavyo humuandaa mtoto kiakili, kimwili, kimaadili na kisaikolojia. Aidha, nawasihi wadau wa watoto kuanzisha vituo vingi zaidi ili watoto wengi waweze kupata huduma hii muhimu***.**

**209.** ***Mheshimiwa Spika***, weledi wa walezi wa watoto katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ni suala linalopewa kipaumbele na Wizara ili kuimarisha makuzi na uchangamshi wa awali kwa watoto wa chini ya miaka mitano ambao ni muhimu katika maendeleo ya afya ya akili na mwili. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Serikali imeendelea kuratibu utoaji wa huduma katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kwa kutoa miongozo na mafunzo kwa Wamiliki wa Vituo pamoja na Walezi wa Watoto 221. Idadi ya Walezi wa Watoto imeongezeka kutoka walezi 2,482 mwaka 2018/19 hadi kufikia walezi 2,924 Machi, 2020 ikiwa ni ongezeko wa Walezi wa Watoto 442.

**210.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia **utoaji wa mafunzo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto** ili kukabiliana na upungufu wa Walezi wa Watoto nchini kupitia vyuo 21. Kati ya vyuo

hivyo, chuo kimoja ni cha Serikali na 20 ni vya Binafsi. Katika mwaka 2019/20, wanafunzi 748 walidahiliwa katika vyuo 21 vinavyotoa mafunzo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto Tanzania Bara. Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara kinachomilikiwa na Serikali kimeendelea kutoa mafunzo ya malezi ya watoto na ustawi wa jamii ambapo jumla ya wanafunzi 169 (Me 31 na Ke 138) walidahiliwa mwaka 2019/20 ikilinganishwa na wanafunzi 63 (Me 17 na Ke 46) waliodahiliwa mwaka 2016/17.

**Huduma kwa Waathirika wa Vitendo vya Ukatili**

**211.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhakikisha kuwa watoto na wanawake wahanga wa ukatili wanapata sehemu za muda za kuishi wakati mashauri yakiendelea. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya watoto 167 (wavulana 111 na wasichana 56) na wanawake 269 walipata huduma katika **nyumba salama** 9 zilizoanzishwa katika mikoa ya Arusha (2), Iringa (1), Kigoma (1), Mara (2), Manyara (1), Morogoro (1) na Mwanza (1). Aidha, Serikali imeendelea kushughulikia **mashauri ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto** ikiwemo ukatili wa kimwili, ukatili wa kihisia, kingono na ukatili wa kiuchumi. Hadi kufikia Machi, 2020, jumla ya mashauri 11,270 ya watu wazima na mashauri 6,651 ya watoto yalipokelewa na kufanyiwa kazi.

**212.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha **utoaji wa huduma kwa wazee na watoto walio katika mazingira hatarishi**, Serikali imeandaa miongozo ambayo ni: Mwongozo wa Wawakilishi wa Watoto Mahakamani (2019); Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Programu za Kijamii za Marekebisho ya Tabia kwa watoto waliokinzana na sheria na wale walio katika hatari ya kukinzana na sheria (2019); Mwongozo wa Kuwaunganisha Watoto na Familia zao (2019); Mwongozo wa Utambuzi na Huduma kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi (2019); Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Makazi ya Wazee (2019); Mwongozo wa Majukumu ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri (2019); na Mwongozo wa Usimamizi Saidizi wa Huduma za Watoto wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi ambao ulifanyiwa mapitio.

**213.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha **utoaji wa huduma kwa waathirika wa ukatili**, Serikali imeendelea kuongeza idadi ya wataalam wanaoshughulikia masuala ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika mikoa yote nchini hadi kufikia wataalam 50,304 Machi, 2020. Kati yao, Polisi Jamii ni 4,542, Wasimamizi wa Mashauri ya Watoto wa Kujitolea 15,255, Wahudumu wa Afya 10,534, Maafisa Ustawi wa Jamii 3,582, Walimu wa Unasihi/Malezi 13,636 na Wasimamizi wa Mashauri ngazi ya Jamii 2,755. Serikali itaendelea kutekeleza mpango huu ili kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wanawake na watoto.

**214.** ***Mheshimiwa Spika***, katika **kutokomeza utumikishwaji wa watoto**, Serikali imetoa elimu kwa umma kwa washiriki 8,873 kuhusu madhara ya utumikishwaji wa watoto katika sekta ya kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi katika mikoa ya Tabora, Mbeya na Songwe. Kati ya washiriki hao, washiriki 4,925 ni wanawake na washiriki 3,948 ni wanaume. Aidha, jumla ya watoto 900 (wavulana 522 na wasichana 378) wanaofanyakazi katika ajira hatarishi wametambuliwa. Vilevile, jumla ya watoto 4,504 (wavulana 1,461 na wasichana 3,043) wanaoishi na kufanya kazi mitaani wametambuliwa na kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo huduma ya unasihi (3,023); msaada wa kisheria (272); mafunzo ya ufundi (231); kutengamanishwa (265); na kuwezeshwa kuanzisha biashara (713).

**Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa na Matunzo ya Watoto**

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** Familia ni kitovu cha maendeleo ya binadamu na Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha utulivu na uimara wa familia kama msingi wa jamii, Serikali imeendelea kuratibu na kutoa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na matunzo kwa watoto walio kwenye ndoa zenye migogoro na waliozaliwa nje ya ndoa kupitia Mabaraza ya Usuluhishi ya Ndoa. Kwa kutambua hili, Serikali imeendelea kufanyia kazi mashauri ya migogoro ya ndoa katika jamii kupitia Mabaraza ya Usuluhishi ya Ndoa. Katika kipindi cha Julai,

2019 hadi Machi 2020, **mashauri ya migogoro ya ndoa 38,659** yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya mashauri hayo, mashauri 3,464 yalifikishwa mahakamani, mashauri 19,272 yamesuluhishwa ili kuwawezesha wanawake kupata haki zao na mashauri 15,923 yanaendelea kufanyiwa kazi kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 1.**

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mashauri ya ndoa mengi huchukua muda mrefu kufanyiwa kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Kazi ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa huchukua zaidi ya mwaka mmoja ili kuwapa wanandoa muda zaidi wa kujitafakari na kuamua mwelekeo wa ndoa yao; utaratibu wa usuluhishi unahitaji umakini mkubwa ambao unaambatana na hatua nyingi kabla ya kuhitimisha shauri. Mfano kuwapa muda wanandoa wakae pamoja wazungumzie juu ya ndoa yao, matunzo ya watoto wao na familia kwa ujumla. Pia, wanapewa muda waende kujitafakari zaidi kabla ya kuchukua hatua za kupeleka shauri mahakamani ili kuvunja ndoa.

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha watoto wanapata huduma na malezi kutoka kwa wazazi wao, Serikali imeendelea kusimamia **utoaji wa huduma za matunzo kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa na katika ndoa zenye migogoro** kulingana na Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, **watoto 13,200**

walipata huduma kutoka kwa wazazi wao ikilinganishwa na watoto 11,897 waliowezeshwa kupata matunzo mwaka 2018/19. Kati ya mashauri yaliyopokelewa, mashauri 12,068 yalishughulikiwa na kuwezesha watoto kupata huduma na mashauri 1,132 yalipelekwa mahakamani kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 2.**

### Huduma za Ustawi wa Jamii kwa Wazee

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 ili kuhakikisha ulinzi na usalama kwa wazee. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, **mabaraza ya wazee 2,292** yameanzishwa katika ngazi mbalimbali hadi kufikia mabaraza ya wazee 14,425 kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 3.** Mabaraza haya hutumika kama majukwaa ya wazee kujadili masuala yanayohusu haki zao.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutoa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa **wazee wasiojiweza** wanaoishi katika Makazi ya Wazee yanayomilikiwa na Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi kufikia Machi 2020, Serikali imefunga Makazi 4 ya Wazee ya Ngehe, Chazi, Nandanga na Nkaseka kati ya Makazi ya Wazee 17 yaliyokuwepo hapo awali hivyo kubaki na makazi ya wazee 13 yanayohudumia

wazee 349 (wanaume 200 na wanawake 149) ikilinganishwa na wazee 445 (wanaume 238 na wanawake 207) waliokuwa wakipatiwa huduma mwaka 2016/17 katika Makazi ya Wazee 17 kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 4.** Makazi ya Wazee 13 yaliyobaki ni pamoja na; Kibirizi, Njoro, Kolandoto, Bukumbi, Ipuli, Fungafunga, Mwanzange, Misufini, Nunge, Nyabange, Kilima, Sukamahela na Magugu. Wazee wasiojiweza wamekuwa wakiongezeka na kupungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwa na pamoja na baadhi ya wazee kuunganishwa na familia zao.

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha wazee wasiojiweza wanapata huduma za msingi kupitia makazi ya wazee yanayomilikiwa na Taasisi Binafsi, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya Makazi ya Wazee 20 yanayomilikiwa na taasisi binafsi katika mikoa 11 ya Kagera, Lindi, Njombe, Dar es Salaam, Tabora, Morogoro, Dodoma, Tanga, Pwani, Shinyanga na Mara yameendelea kutoa huduma kwa wazee wasiojiweza. Makazi haya yamewezesha huduma mbalimbali za msingi ikiwa ni pamoja na chakula, mavazi, malazi na matibabu kwa wazee 451 (wanawake 235 na wanaume 216) ikilinganishwa na wazee 383 waliopata huduma mwaka 2018/19 kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 5.**

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea kuwawezesha wazee kupata **huduma za matibabu bila malipo** ili kuboresha afya za wazee. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya wazee 167,566 (wanaume 71,801 na wanawake 95,765) wamepata vitambulisho vya matibabu bila malipo. Juhudi hii imewezesha wazee waliopata vitambulisho vya matibabu bila malipo kuongezeka kutoka wazee 213,025 mwaka 2015/16 hadi kufikia wazee 856,052 Machi, 2020, sawa na ongezeko la asilimia 301.

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** elimu kuhusu haki za wazee imeendelea kutolewa katika jamii kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo Maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Kimataifa ya Wazee yaliyofanyika tarehe 1 Oktoba 2019, Mkoani Mtwara ambapo Kaulimbiu ilikuwa “**Tuimarishe Usawa Kuelekea Maisha ya Uzeeni”**. Mgeni rasmi katika maadhimisho haya alikuwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo la maadhimisho haya ni kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya haki na ustawi wa wazee nchini ikiwa ni pamoja na matunzo, ulinzi na usalama kwa wazee pamoja na kutokomeza mauaji ya wazee.

**Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi**

**la Wanawake** lililoanzishwa katika **Benki ya Posta Tanzania (TPB)**. Mikopo hii inatolewa kwa riba ya **asilimia 3** kwa mwezi kwa vikundi vyenye wanawake wajasiriamali watano hadi kumi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, mikopo yenye thamani ya shilingi 3,586,400,000 imetolewa kwa wanawake wajasiriamali 14,271 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi 2,050,100,000 kilichotolewa kwa wanawake wajasiriamali 3,035 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 75. Aidha, mafunzo ya ujasiriamali yametolewa kwa wajasiriamali 718 wakiwemo wanawake 334 na wanaume 384 katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Geita na Mbeya. Mafunzo yamewawezesha wanawake kupata ujuzi wa namna ya kuongeza ubora wa bidhaa, jinsi ya kutafuta mitaji, utafutaji wa masoko, uwekaji wa akiba na utunzaji wa fedha.

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwawezesha wanawake wajasiriamali kiuchumi, Wizara imeratibu Kongamano la Kiuchumi la Wanawake Wajasiriamali lililofanyika Mkoani Arusha tarehe 20/12/2019, ambapo lengo lake ni kuwaunganisha wanawake wajasiriamali na watoa huduma mbalimbali za uwezeshaji wanawake kiuchumi. Huduma hizo ni pamoja na masuala ya mikopo yenye masharti nafuu,

matumizi ya teknolojia rahisi na sahihi katika uzalishaji, kuanzisha na kujiunga na vikundi vya kiuchumi pamoja na umuhimu wa kuzingatia ubora wa viwango wa bidhaa zinazozalishwa ili kukidhi matakwa ya kisheria na kimasoko. Jumla ya wanawake wajasiriamali 203 walinufaika na Kongamano hilo.

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo ya jamii ikiwemo uwezeshaji wanawake kiuchumi, Watalaam wa Maendeleo ya Jamii kutoka Halmashauri ya Mpanda mkoani Katavi wamepatiwa pikipiki 15 na Halmashauri ya Chamwino mkoani Dodoma pikipiki 14. Wataalam wanatumia pikipiki hizo kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, masuala ya jinsia na kuwaunganisha wanawake na makundi mengine katika jamii na fursa mbalimbali. Pikipiki zitawasaidia wataalam wa maendeleo ya jamii wa kata kurahisisha usafiri ili kuwafikia wananchi hususan wanawake wa maeneo ya vijijini.

**Kuzuia Ukatili wa Kijinsia**

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuzuia na kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kuzindua Kampeni ya Siku

16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia iliyofanyika mkoani Dodoma tarehe 26/11/2019 ikiwa na kaulimbiu inayosema "**Kizazi Chenye Usawa: Simama Dhidi ya Ubakaji**". Katika Kampeni hiyo, watu 1,567,343 walifikiwa kupitia mitandao ya kijamii (Facebook 652,530, Twitter 787,020 na Instagram 127,793). Aidha, Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Mwanamke wa Kijijini yalifanyika katika Kijiji cha Gehandu mkoani Manyara tarehe 15 – 17 Oktoba, 2019 ili kutambua na kuthamini mchango wa mwanamke wa kijijini na kuweza kuongeza kasi ya uwekezaji kwenye afua za kimkakati zenye lengo la kuboresha hali ya kiuchumi na kijamii kwa wanawake wa vijijini.

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, Wizara imeratibu makongamano mawili ya kikanda katika Mikoa ya Singida na Ruvuma na Kongamano moja kwa ngazi ya Kitaifa lililofanyika Dodoma ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Wanawake Duniani. Jumla ya washiriki 1,985 (Singida 209, Dodoma 1,576 na Ruvuma 200) walishiriki. Makongamano hayo yalihudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka Serikalini ikiwemo Mawaziri, viongozi ngazi mbalimbali, wastaafu wa Taasisi za Serikali, Mashirika ya Kimataifa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Viongozi wa Dini, Wabunge,

Wanafunzi, Wasanii, vyombo vya Habari pamoja na wananchi ambao ndiyo walikuwa walengwa wakuu wa makongamano hayo. Lengo la makongamano hayo ilikuwa ni kutafakari kwa pamoja tulipotoka, tulipo na tunapoelekea na kuona ni kwa namna gani ambavyo Tanzania imeweza kutekeleza maazimio ya Kitaifa na Kimataifa ambayo ni: Azimio la Ulingo wa Beijing (1995); Malengo Endelevu ya Maendeleo (2030) hususan lengo namba 5 linalohusu Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi; na Ajenda ya Maendeleo ya Bara la Afrika (2063).

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau inatekeleza **mradi wa kutokomeza vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto katika maeneo ya masoko** ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Julai, 2019 Jijini Dodoma. Lengo la mradi huu wenye kaulimbi "**Mpe Riziki Si Matusi**" ni kutokomeza vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto katika maeneo ya masoko kwa kutoa elimu kwa jamii ya wafanyabiashara walio katika masoko. Kupitia mradi huu, Madawati ya mfano ya kutolea taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yameanzishwa katika maeneo ya masoko ya Jiji la Dodoma na Manispaa ya Shinyanga.

Mradi huu ni wa majaribio chini ya ufadhili wa Shirikisho la Mamlaka za Serikali za Mitaa – ALAT.

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa kutekeleza kampeni ya **"Tokomeza Ukatili, Twende Pamoja"** kupitia Misafara ya Kijinsia (Gender Caravans). Misafara miwili ilifanyika ambapo msafara wa kwanza ulianzia Mkoa wa Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa, Tabora, Shinyanga hadi Simiyu na msafara wa pili ulianzia Mkoa wa Arusha, Manyara, Singida, Mwanza hadi Simiyu. Lengo la misafara hii lilikuwa ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia na kuhimiza upatikanaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wanawake. Katika misafara hii, huduma na elimu mbalimbali zilitolewa kwa wananchi 9,000 ikiwa ni pamoja na: upimaji wa Afya ya Mama na Mtoto, Elimu ya Biashara na Ujasiriamali, Utoaji wa Vyeti vya Kuzaliwa, Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Masuala ya Mirathi, Msaada wa Kisheria, Mabadiliko ya Tabia Nchi na ushiriki wa jamii katika nafasi za uwakilishi na vyombo vya kutoa maamuzi.

## Kuimarisha Usawa wa Jinsia na Haki za Wanawake

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada za kusimamia na kuleta usawa wa kijinsia katika jamii, wanawake wameweza kushika nafasi mbalimbali za uongozi. Nafasi hizo ni za Makamu wa Rais na Naibu Spika wa sasa. Pia, wapo Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao ni Wanawake. Takwimu zinaonesha kuwa Wabunge Wanawake waliongezeka kutoka 127 mwaka 2015 hadi kufikia 143 mwaka 2019. Wabunge wanawake wa kuchaguliwa waliongezeka kutoka 21 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 26 mwaka 2019 na Majaji wanawake waliongezeka kutoka 24 mwaka 2015 hadi kufikia 40 mwaka 2019. Hii ni kutokana na kufanya uhamasishaji wa ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi pamoja na dhamira ya Serikali ya kuthamini mchango wa wanawake na kutoa nafasi mbalimbali katika uongozi na maamuzi kutokana na juhudi wanazozifanya katika utendaji wao wa kazi.

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kila mwaka tarehe 8 Machi, huungana na Mataifa mengine Wanachama wa Umoja wa Mataifa katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. Lengo la Maadhimisho haya ni kujenga hamasa, mshikamano na uwezo wa wanawake katika

kushiriki na kunufaika na maendeleo ili kufikia usawa wa kijinsia na malengo ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa. Maadhimisho ya mwaka 2020 yalifanyika Kitaifa mkoani Simiyu na Kaulimbiu ilikuwa "**Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na Baadaye**". Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea kuratibu uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, mikakati na miongozo mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Serikali imesimamia utendaji wa madawati ya jinsia yaliyoanzishwa katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuhakikisha programu zote zinatekelezwa kwa kuzingatia mlengo wa kijinsia ili kuleta haki na usawa wa jinsia nchini. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Jeshi la Magereza limeanzisha Madawati ya Jinsia 153 ili kuwezesha uwepo wa fursa sawa za kijinsia na kupambana na vitendo vya ukatili katika taasisi hiyo na kuzuia ukatili kwa wafungwa wakiwemo watoto walio kwenye magereza. Pia, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeanzisha Dawati la Jinsia kwa ajili ya kushughulikia masuala ya rushwa ya ngono. Katika kipindi cha Machi 2019 hadi Machi 2020, majalada 31 yalipokelewa kutoka katika mikoa 15 ya Mwanza, Kagera, Mtwara, Mara, Arusha, Dodoma, Geita, Iringa,

Katavi, Kinondoni, Manyara, Rukwa, Singida, Temeke na Ruvuma. Kati ya taarifa hizo, kesi 14 zilipelekwa mahakamani ambapo kesi tisa (9) watuhumiwa walihukumiwa baada ya kukutwa na hatia (conviction), kesi tatu (3) watuhumiwa hawakukutwa na hatia kutokana na kukosekana kwa ushahidi, kesi moja (1) iliondolewa mahakamani (acquittal) na kesi moja (1) bado inaendelea mahakamani. Aidha, majalada 17 yanaendelea na uchunguzi.

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kuhusu umuhimu wa uanzishwaji wa madawati ya jinsia. Katika mwaka 2019/20, Wizara iliratibu kikao cha Wakuu wa Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Kati kwa lengo la kukubaliana kuhusu kuanzisha **Dawati la Jinsia katika vyuo**. Hadi kufikia Machi, 2020 jumla ya madawati matano (5) ya Jinsia yameanzishwa katika Vyuo vya Elimu ya Juu (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu Mzumbe) ili kuzuia ukatili wa kijinsia hususan rushwa ya ngono.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Serikali kwa kushirikiana na wadau imetekeleza afua mbalimbali ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Afua hizo ni pamoja na;

kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na kuwajengea uwezo wanawake ambao wameonesha nia ya kugombea nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Aidha, wanawake watia nia 915 wamepewa elimu kuhusu umuhimu wa kugombea nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali kupitia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za "Uongozi Institute" na TGNP Mtandao.

**Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yachangie katika kuleta maendeleo kwa Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya **Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,403** yalisajiliwa na kupatiwa vyeti cha usajili. Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali umeongezeka kutoka mashirika 404 mwaka 2005 na kufikia mashirika 10,446 Machi, 2020 kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 6**. Mashirika haya yamewezesha utoaji wa huduma za kijamii katika nyanja za afya, elimu, maji, mazingira, kilimo, haki za binadamu, utawala bora, jinsia, ufugaji na uvuvi, wanyama pori, nishati, watu wenye ulemavu na ustawi wa watoto na wazee.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, taratibu, mila na desturi za nchi, Wizara imewezesha marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 3/2019. Aidha, Serikali imetunga kanuni tatu zenye lengo la kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Sheria hiyo. Kanuni hizo ni: Kanuni Na. 685/2019 kwa lengo la kuhuisha vyeti vya Mashirika katika kipindi cha miaka 10 ikiwa ni pamoja na utoaji wa tuzo kwa Mashirika yanayozingatia uwazi na uwajibikaji; Kanuni Na. 686/2019 inayoainisha majukumu ya Wasajili Wasaidizi pamoja na taratibu za uteuzi wao; na Kanuni Na. 687/2019 inayolenga kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kutoa utaratibu wa kupokea taarifa za robo mwaka za utendaji wa Mashirika.

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 pamoja na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24 ya mwaka 2002 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 206 yalifuatiliwa katika mikoa s mitano ambayo ni: mkoa wa Mwanza (mashirika 43), Dar es Salaam (mashirika 63), Iringa (Shirika moja), Arusha (mashirika 55) na Mbeya (mashirika 44). Ufuatiliaji huo ulibaini kuwa Mashirika

Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kuchangia katika jitihada mbalimbali za Serikali za kuleta maendeleo katika nyanja za kijamii na kiuchumi. Mashirika haya yanashirikiana na watendaji wa Serikali katika kutoa hamasa, kuzijengea jamii uwezo wa kuboresha maisha, kutambua fursa ikiwa ni pamoja na kutoa rasilimali fedha kwa ajili ya uwekezaji katika utoaji wa huduma za jamii na uendelezaji wa rasilimali zenye tija. Ufuatiliaji huu wa mashirika 206 katika mikoa 5 umebaini jumla ya shilingi 69,160,254,172 zilitumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo afya, uwezeshaji kiuchumi, maji, ujenzi wa shule na vituo vya afya pamoja na utoaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa watoto walio katika mazingira hatarishi.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 3/2019 na Kanuni zake, Wizara imeendelea kupokea mikataba ya fedha ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambapo kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya Mashirika 113 yaliwasilisha mikataba yao yenye kiasi cha shilingi 3,047,581,824,753 kwa lengo la kupata kibali cha Msajili kabla ya kutekeleza miradi yao.

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

yatokanayo na ada mbalimbali kama ada za usajili, ada za mwaka, ada za uhakiki wa taarifa na faini zitokanazo na ucheleweshwaji wa uwasilishaji taarifa. Katika Kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya shilingi 298,200,173 zilikusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi na ubora wa utoaji huduma kwa umma, Serikali imeandaa mfumo wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambao unawezesha usajili, utumaji wa taarifa na utunzaji wa kumbukumbu za taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hadi kufikia Machi 2020, taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 10,446 yaliyosajiliwa zimeingizwa kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mashirikiano baina ya Serikali ya Muungano Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) katika uratibu wa utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, vikao viwili vya mashirikiano vilifanyika tarehe 24 - 25 Septemba, 2019 Zanzibar na tarehe 23 Desemba, 2019 Jijini Dar es Salaam. Lengo la vikao hivyo lilikuwa ni kubadilishana uzoefu wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. Vikao hivi vimekuwa na mafanikio makubwa hasa katika

kuhakikisha Ofisi za Wasajili kwa SMT au SMZ kukubaliana kutoa barua za utambulisho kwa Shirika Lisilo la Kiserikali litakalohitaji kusajiliwa upande mwingine wa muungano.

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi ya mikoa na Halmashauri, Wizara imewezesha uteuzi wa **Wasajili Wasaidizi (Maafisa Maendeleo ya Jamii) 211** katika ngazi ya mkoa na Halmashauri wakiwemo Wasajili Wasaidizi 26 kutoka katika mikoa na 185 kutoka katika Halmashauri. Majina ya Wasajili Wasaidizi yametangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 115/2020 la tarehe 14 Februari, 2020 ili kuwafahamisha wadau mbalimbali kuhusu uteuzi huo kwa mujibu wa Kifungu cha 22 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama kilivyorekebishwa na Sheria Na. 3/2019. Majukumu ya Wasajili Wasaidizi ni pamoja na: kupokea na kufanya uchambuzi wa maombi ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; kupokea maombi na kusajili asasi za Kijamii; kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya shughuli yamesajiliwa; na kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayotekeleza afua zinazofanana hayafanyi kazi katika eneo moja.

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni wadau muhimu sana katika kufikia maendeleo ya jamii katika afua za uwezeshaji wa jamii, utawala bora, afya, miundombinu,

huduma za jamii na uwezeshaji wa makundi maalum kama vile wazee, watoto na vijana. Kwa kipindi cha mwaka 2019 hadi Machi 2020, jumla ya watu 320,000 walinufaika na huduma za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambapo 40,000 walijengewa uwezo katika elimu ikijumuisha TEHAMA na ujasiriamali; 250,000 walijengewa uwezo katika masuala ya uchumi na mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia na magonjwa mbalimbali; 10,000 walipatiwa elimu ya utawala bora na masuala ya Sheria na Haki za Binadamu; na 20,000 walipatiwa huduma za kinga ya jamii ikiwemo watoto, wazee, wasiojiweza na wenye ulemavu. Aidha, watu 200 wakiwemo vijana na akina mama walipatiwa elimu ya uongozi, kuwezeshwa katika ujengaji wa maabara, vyumba vya madarasa na nyumba za walimu.

**245.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kuchangia katika shughuli za maendeleo ya jamii nchini ikiwemo utoaji wa ajira za kudumu na za muda mfupi kwa wananchi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliajiri jumla ya watu 6,325 wakiwemo watanzania 6,168 na wasio watanzania 157.

## RASILIMALIWATU KATIKA SEKTA YA MAENDELEO NA USTAWI WA JAMII

**246.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutatua changamoto ya uhaba wa Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini, Serikali imeendelea kuajiri watumishi hao katika Halmashauri zote nchini. Idadi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii waliajiriwa katika Halmashauri na Mikoa mbalimbali nchini imeongezeka kutoka maafisa 2,846 mwaka 2016/17 hadi kufikia maafisa 2,983 Machi, 2020 sawa na ongezeko la maafisa 137. Hatahivyo, takwimu za Halmashauri zinaonesha uhitaji wa Maafisa Maendeleo ya Jamii 5,428 katika ngazi mbalimbali za Halmashauri. Hali hii inapelekea kuwepo kwa upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii 2,445 katika ngazi zote sawa na asilimia 45 kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 7**.

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii katika maeneo mbalimbali ikiwemo Halmashauri ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto walio katika mazingira hatarishi. Hadi kufikia Machi 2020, Maafisa Ustawi wa Jamii 740 wanafanya kazi katika ngazi mbalimbali za Serikali ikiwemo hospitali kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 8.** Idadi hii inaonesha kuna upungufu wa asilimia 97 ya mahitaji halisi nchi nzima. *Napenda kuzielekeza Halmashauri kutoa kipaumbele katika kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi zote.*

## F. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII (FUNGU 53)

### Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeendelea kutoa mafunzo ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2019/20, Taasisi ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 2,254,210,000 kwa mwaka 2019/20 ambapo ni mapato ya ndani yanayotokana na ada za wanafunzi waliodahiliwa. Hadi kufikia Machi, 2020, Taasisi iliweza kukusanya Shilingi 1,664,186,824.37 sawa na asilimia 74 ya makadirio.

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ilidahili jumla ya wanafunzi 1,971 (Me 1,350 na Ke 621) mwaka 2019/20 katika fani ya maendeleo ya jamii ikilinganishwa na wanafunzi 628 (Me 237 na Ke 391) waliodahiliwa mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia 213.85. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2019/20, wanafunzi 439 (Me 324 na Ke 115) walidahiliwa katika ngazi ya Astashahada, wanafunzi 694 (Me 643 na Ke 210) ngazi ya Stashahada, wanafunzi 629 (Me 367 na Ke 262) ngazi ya Shahada na wanafunzi 209 (Me 117 na Ke 92) ngazi ya Shahada ya Uzamili. Aidha, katika mwaka 2019/20, wanafunzi 917 (Me 286 na Ke

631) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 200 (Me 75 na Ke 125) waliohitimu mwaka 2016/17.

**250.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeanzisha programu ya kukuza vipaji vya wanafunzi. Taasisi imeanzisha Kituo cha Kidigitali cha Ubunifu kijulikanacho kama Jamii Outreach Digital Innovation Centre (JODIC) mwezi Novemba, 2019 kwa ajili ya kuatamia na kuboresha mawazo ya ubunifu ili kutatua changamoto zinazoikabili jamii. Kituo hiki kitawasaidia wanafunzi kufikiri na kuboresha mawazo yao na kuyaweka kwa vitendo. Kituo hicho kitasimamia maeneo makuu matatu ambayo ni: Ushirikishwaji Jamii; Uanagenzi; na Ubunifu wa Kidijitali.

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imehamasisha ujenzi wa kivuko cha Mto Malala kinachounganisha vijiji vya Kata ya Akheri na Kata ya Siera Sing'isi kilichogharimu Shilingi 34,000,000. Hadi sasa imefanyika harambee ya kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali za ujenzi wa daraja. Wananchi, wadau na Taasisi zimechangia mifuko 100 ya saruji yenye thamani ya Shilingi 1,500,000 na fedha taslimu Shilingi 1,125,000. Wananchi na Taasisi zitashiriki kwenye nguvu kazi ambayo itaokoa kiasi cha Shilingi 10,200,000 za vibarua.

**252.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kuwa na weledi kulingana na mahitaji ya wateja na soko. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Taasisi imewezesha watumishi 18 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ambapo watumishi 7 Shahada ya Uzamivu; 3 Shahada ya Uzamili; 4 masomo ya uhasibu; mtumishi mmoja Stashahada ya Uzamili; na watumishi 11 waliwezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Taasisi pia imeandaa kanuni na kitabu cha miongozo kwa wanafunzi wa uzamili. Vilevile, Taasisi imeratibu midahalo ya wanafunzi wa kike kila mwezi kwa ajili ya kuwajengea uwezo kuhusu utawala binafsi, ustawi kitaaluma na mafunzo kwa vitendo.

**253.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na tatizo la ukatili wa kijinsia ikiwemo rushwa sehemu za kazi, Taasisi imeendelea kupambana na masuala ya rushwa kwa watumishi na wanafunzi kwa kuanzisha Dawati la Malalamiko na Afisa wa kufuatilia masuala ya rushwa ameteuliwa. Taasisi imeanzisha Masanduku ya Maoni 12 ili kuwezesha wanafunzi na watumishi kutoa taarifa za rushwa.

**254.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Taasisi imefanya ukarabati wa

karakana ya ufundi seremala, mabomba ya maji safi, ofisi ya kituo cha ubunifu, miundombinu ya umeme, viti 120 visivyohamishika na ofisi za watumishi. Taasisi pia imefanya ukarabati katika ukumbi wa mihadhara wa Mwalimu Nyerere, uboreshaji wa miundombinu ya barabara na huduma ya mitandao ya TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano na Tume ya Vyuo Vikuu na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Ukarabati huo na ujenzi umegharimu kiasi cha Shilingi 165,226,664.00.

**Taasisi ya Ustawi wa Jamii**

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2019/20, Taasisi ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi 9,270,372,000.00 ambapo hadi Machi, 2020 Taasisi iliweza kukusanya Shilingi 6,054,913,160.00 sawa na asilimia 65.31 ya makadirio.

**256.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ilidahili wanafunzi 1,799 (Me 524 na Ke 1,275) mwaka 2019/20 ikilinganishwa na wanafunzi 1,246 (Me 410 na Ke 836) waliodahiliwa mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 44.38. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2019/20, wanafunzi 920 walidahiliwa katika

ngazi za Astashahada, wanafunzi 225 ngazi ya Stashahada, wanafunzi 611 ngazi ya Shahada, wanafunzi 25 ngazi ya Stashahada ya Uzamili na wanafunzi 18 ngazi ya Shahada ya Uzamili. Aidha, katika mwaka 2018/19, jumla ya wanafunzi 1,541 (Me 472 na Ke 1,069) walihitimu masomo katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,172 (Me 383 na Ke 789) waliohitimu mwaka 2016/17. Kati yao, wanafunzi 736 wamehitimu katika ngazi ya Astashahada, wanafunzi 330 wamehitimu ngazi ya Stashahada, wanafunzi 418 wamehitimu ngazi ya Shahada, wanafunzi 15 wamehitimu ngazi ya Stashahada ya Uzamili na wanafunzi 42 wamehitimu ngazi ya Shahada ya Uzamili.

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea na ujenzi wa jengo la maktaba na utawala (Information Resource Centre). Lengo la mradi ni kuwa na maktaba ya kisasa pamoja na ofisi za wafanyakazi ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kukidhi vigezo vya NACTE. Mradi wa kujenga "Information Resource Centre" ulianza mwaka 2006/07 na ulitarajiwa kumalizika katika kipindi cha miaka miwili. Kutokana na changamoto ya kifedha Taasisi imekuwa ikitekeleza mradi huu kwa awamu kwa kutumia mapato yake ya ndani na hii ni awamu ya saba. Taasisi imesaini mkataba na SUMA JKT wa Shilingi 845,152,226.00 ili kutekeleza awamu ya saba. Katika mwaka

2019/20, shughuli zilizofanyika katika awamu ya saba ni pamoja na; kufunga mfumo wa habari na mawasiliano (TEHAMA), mfumo wa umeme, mfumo wa mabomba ya maji, ujenzi wa kuta za ndani na kupiga rangi na kufunga kiinua (lift) ambayo imeshafika eneo la mradi na ipo katika utekelezaji.

**258.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imefanikiwa kununua jenereta yenye uwezo wa KVA 400 kwa thamani ya Shilingi 216,000,000.00 yenye uwezo wa kuhudumia madarasa yote, hosteli za wanafunzi na ofisi zote. Uwepo wa jenereta hii utaiwezesha Taasisi kuwa na umeme wa uhakika katika madarasa, mabweni ya wanafunzi na ofisi zote pale panapokuwa na changamoto ya umeme wa TANESCO.

**259.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imenunua viti vya madarasani 220, kurekebisha viti 45 pamoja na kununua viti 100 vya maktaba kwa thamani ya Shilingi milioni 91.27. Viti hivyo vinatumika katika madarasa matatu na hivyo kupunguza uhaba wa vyumba vya kusomea unaotokana na kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika mwaka 2019/20. Taasisi pia ilinunua majoho ya mahafali 615 yenye thamani ya Shilingi milioni 63.36. Taasisi pia imepanga kukarabati hosteli za wanafunzi kwa njia ya "force account" kwa jumla ya Shilingi milioni 311.

**260.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mafunzo, tafiti na ushauri elekezi, Taasisi imefanikiwa kuandaa mtaala wa Stashahada ya Kazi za Jamii, Vijana na Watoto (Ordinary Diploma in Community Work with Youth and Children) na mtaala wa Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Rasilimaliwatu (Master in Human Resource Management) na kuwasilisha NACTE. Taasisi pia imechapisha kitabu kimoja ambacho ni "Social Welfare Services, Political Ideologies and Economic Development in Tanzania: Past, Present and Future" (Manyama, W. 2019). Vilevile, katika mwaka 2019/20, Taasisi imefanya tathmini (Tracer Study) juu ya Uwezo wa Wahitimu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii katika Kutumia Elimu yao tangu Taasisi kuanzishwa na kutoa ripoti mwezi wa Septemba, 2019.

**261.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kuhakikisha kuwa, watumishi wake wanajiendeleza kitaaluma kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kufanya mapitio ya muundo wake wa utumishi na mpango wa motisha kwa wafanyakazi ambavyo viliwasilishwa kwa Msajili wa Hazina. Muundo huo ulipitiwa kutokana na kuongezeka na mahitaji ya Taasisi. Aidha, jumla ya watumishi 40 waliendelea na mafunzo ya elimu ya juu katika vyuo mbalimbali ambapo 31 wanasomea Shahada ya Uzamivu (PhD) kwa ajili ya kuimarisha uendeshaji wa Taaluma

wakiwemo wanawake 18 na wanaume 13. Kwa kuzingatia umuhimu wa suala la utawala bora, Taasisi pia iliweza kuandaa warsha na semina kwa wafanyakazi wake na kuwaruhusu kuhudhuria semina zilizoandaliwa na wadau mbalimbali ikiwa na lengo la kuboresha utawala bora kupitia mafunzo hayo na kuhakisha kuwa vikao yote vya maamuzi vinakuwa shirikishi.

**262.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi pia imetoa huduma ya unasihi na upimaji wa VVU. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Taasisi kwa kushirikiana na Kituo cha Afya cha Oasisi ilifanikiwa kutoa huduma ya upimaji VVU kwa wanafunzi 53 na wafanyakazi 20. Huduma nyingine iliyotolewa ni upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza (shinikizo la damu, kisukari na unene uliopitiliza). Vilevile, Taasisi ilitoa huduma ya unasihi kuhusu changamoto za ndoa, ulinzi na matunzo ya watoto na matumizi ya madawa ya kulevya kwa wateja 50.

**263.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutokomeza ukatili wa kijinsia ikiwemo rushwa ya ngono, Taasisi ya Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imetoa uelewa kwa wanafunzi kuhusiana na masuala ya rushwa, hasa rushwa ya ngono. Taasisi pia imeanzisha klabu ya wanafunzi ya kupambana na rushwa.

**264.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mafunzo yanayotolewa na Taasisi yanawajengea uwezo wahitimu kujiajiri au kuajirika, Taasisi imeanzisha programu ya uanagenzi (apprenticeship) inayolenga kuwajengea wanafunzi na wahitimu uzoefu katika ajira. Taasisi imeshatambua na kufanya mazungumzo na waajiri ambao watawapokea wanafunzi na wahitimu kwa kipindi cha miezi mitatu ikiwa ni sehemu yao ya kujifunza wakiwa kazini chini ya uangalizi maalum. Aidha, Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kukuza ubunifu wa wanafunzi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao baada ya kuhitimu mafunzo. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Taasisi imeanzisha Ukumbi wa Ubunifu (ISW Digital Innovation Hub). Lengo la ukumbi huu ni kuwapa wanafunzi nafasi ya kuibua ubunifu katika nyanja mbalimbali.

**265.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi pia imeendelea na jitihada za kuhakikisha inatoa huduma kwa jamii inayoizunguka na hivyo kuanzisha mpango shirikishi wa jamii (Community Engagement Program) inayohusisha uongozi wa wilaya, kata na mitaa katika Wilaya ya Kinondoni. Mafunzo yameanza kutolewa kwa viongozi wa mitaa na kata ili kuwapa stadi ya namna ya kushirikisha jamii katika kujiletea maendeleo yao wenyewe kwa kutambua fursa zinazozunguka jamii husika.

**266.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wateja mbalimbali kutokana na uhitaji. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Taasisi imetoa mafunzo ya utoaji wa huduma za ushauri nasaha kwa wateja 15 kutoka sehemu mbalimbali. Aidha, Taasisi imetoa mafunzo ya malezi kwa walezi 15 wanaofanya kazi katika vituo vya kulea watoto vya SOS. Taasisi pia imewajengea uwezo Maafisa Kazi wawili (2) katika masuala ya majadiliano na maridhiano sehemu za kazi.

## G. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2020/21

### IDARA KUU YA AFYA - FUNGU 52

**267.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21 Wizara kupitia Fungu 52 (Afya) imejiwekea vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha huduma za afya nchini:-

i. Kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo ili kuwakinga na magonjwa watoto chini ya umri miaka 5, akina mama wajawazito na kutoa chanjo nyingine za kimkakati za kukinga na kudhibiti ya magonjwa yanayozuilika kama Homa ya Ini, kichaa cha mbwa na mengineyo;

ii. Kuimarisha Huduma za Lishe hususani kwa watoto chini ya miaka 5 na wanawake wa umri wa kuzaa;

iii. Kuboresha Usafi wa Mazingira nchini ili kupunguza kuenea kwa magonjwa ya kuambukizia kama vile kipindupindu, kuhara, kuhara damu, corona na minyoo;

iv. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza ikiwa ni pamoja na Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI pamoja na magonjwa yasiyoambukiza kama vile magonjwa ya moyo, kisukari na saratani;

v. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini;

vi. Kupunguza vifo vya akina mama na watoto wachanga vinavyotokana na uzazi;

vii. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya za kibingwa na ubingwa bobezi;

viii. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma katika Hospitali ya Taifa, Maalumu, Rufaa za Kanda na Mikoa;

ix. Kuimarisha mpango wa Taifa wa utayari wa kukabiliana na magonjwa ya

milipuko, ajali na majanga; na

x. Kuimarisha mafunzo na maendeleo ya wataalam katika Sekta ya Afya.

**268. *Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza vipaumbele vilivyoanishwa katika mwaka 2020/21, Wizara imekadiria kutumia kiasi cha **shilingi bilioni 900** zitakazotumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa ofisi na miradi wa maendeleo. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2020/21 ni pamoja na:-

i. Ununuzi na usambazaji wa chanjo **shilingi bilioni 51.5** zimetengwa;

ii. Kupunguza Vifo vya akina Mama vitokanavyo na Uzazi na vifo vya Watoto, jumla ya **shilingi bilioni 3.5** zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa vituo 6 vya kukusanyia Damu Salama (Satellite Blood Banks), katika mikoa 12 yenye uhitaji mkubwa;

iii. Ununuzi na Usambazaji wa Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo **shilingi bilioni 246** zimetengwa ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 46** ni kwa ajili ya Miradi Misonge ambayo ni UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu;

iv. Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma katika Hospitali ya Taifa,

Hospitali Maalumu, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa, **shilingi bilioni 28** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miundombinu katika Hospitali hizo;

v. Kuendelea kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, na Hospitali za Rufaa za Kanda ambapo, kiasi cha **shilingi bilioni 12.5** kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba;

vi. Kukabiliana na magonjwa ya milipuko, ajali na majanga ambapo **shilingi milioni 440** zimetengwa; na

vii. Kuboresha miundombinu ya vyuo vya afya na kugharamia mafunzo na maendeleo ya wataalam katika Sekta ya Afya, kiasi cha **shilingi bilioni 19** zimetengwa kwa ajili ya kugharamia mitihani, chakula na ukarabati wa miundombinu vya Vyuo vya Afya.

## IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII - FUNGU 53

**269.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia Fungu 53 itatekeleza vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha utoaji huduma za ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii:-

i. Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia nguvu kazi na rasilimali zinazowazunguka;

ii. Kuwezesha Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kuboresha utoaji wa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko na kutekeleza dhana ya uanagenzi;

iii. Kuwezesha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kuboresha utoaji wa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko na kutekeleza dhana ya uanagenzi;

iv. Kuwezesha Taasisi ya Ustawi wa Jamii kuboresha utoaji wa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko;

v. Kupambana na kutokomeza ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake, wazee na watoto ikiwa ni pamoja na kudhibiti wimbi la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani;

vi. Kuratibu na kuweka mazingira wezeshi ya kuendeleza huduma atamizi za uwezeshaji kiuchumi kwa makundi ya jamii yakiwemo wanawake na vijana;

vii. Kuhakikisha uingizwaji wa masuala ya jinsia ikiwa ni pamoja na kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi;

viii. Kuratibu kampeni ya kuhamasisha jamii kubadili mtazamo katika kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi katika kukuza ajira kwa wanawake na makundi mengine katika jamii;

ix. Kuweka na kuendeleza mifumo imara ya kijamii katika malezi, ulinzi na maendeleo ya familia na mtoto;

x. Kuimarisha uratibu na uanzishaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vituo vya kijamii vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto;

xi. Kuwezesha upatikanaji wa huduma na mahitaji ya msingi kwa makundi yenye uhitaji maalum ikiwemo wahanga wa majanga makubwa, wazee na watoto; na

xii. Kuimarisha ufuatiliaji na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kutoa mchango chanya katika ujenzi wa Taifa.

**270.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2020/21, Wizara imekadiria kutumia kiasi cha **shilingi billioni 33** ili kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

## Maendeleo ya Jamii

**271.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao na maendeleo ya mtu mmoja mmoja katika jamii, katika mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendesha Kampeni ya Kitaifa ya Kuhamasisha Jamii Ujenzi wa Nyumba Bora za Gharama Nafuu zinazotumia teknolojia rahisi na sahihi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara;

ii. Kujenga kumbi pacha na hosteli katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Jumla ya **shilingi bilioni 2.7** zimetengwa;

iii. Kukarabati majengo na miundombinu katika Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii;

iv. Kuboresha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii ili kukidhi mahitaji ya soko na kutekeleza dhana ya uanagenzi, kukuza ujuzi wa wahitimu na kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa. Jumla ya **shilingi bilioni 6.6** zimetengwa; na

v. Kutekeleza mpango wa ushirikishaji jamii ili kutoa suluhisho kwa changamoto zinazoikabili jamii.

**272.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha 2020/21, ili kukuza haki za watoto nchini, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendesha kampeni ya kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto;

ii. Kuwezesha uanzishwaji wa vituo vya jamii vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali;

iii. Kuwezesha uanzishwaji wa vikundi vya malezi katika jamii;

iv. Kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Kuwekeza Kwenye Afya na Maendeleo ya Vijana Balehe;

v. Kuimarisha na kuanzisha kamati za ulinzi za wanawake na watoto;

vi. Kuratibu uanzishwaji wa madawati ya kuzuia ukatili katika shule za msingi na sekondari ili kuzuia ukatili dhidi ya watoto; na

vii. Kuhamasisha jamii namna ya kuwakinga watoto na ukatili wa mitandaoni.

## Huduma za Ustawi wa Jamii

**273.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa kazi zifuatazo: -

i. Kuwatambua, kuwatengamanisha na kuwaunganisha na familia watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani;

ii. Kujenga Makao ya Taifa ya Watoto jijini Dodoma;

iii. Kukarabatimajengonamiundombinu katika makazi ya wazee. Jumla ya **shilingi milioni 400** zimetengwa;

iv. Kuimarisha mifumo ya kijamii ya malezi na ulinzi wa watoto na familia;

v. Kutekeleza kuwatangamanisha watoto katika Makao Mapya ya Watoto yatakayojengwa Dodoma;

vi. Kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Kusimamia Mpango wa Huduma kwa kila mtoto katika Makao ya Watoto;

vii. Kufanya usuluhishi wa migogoro ya ndoa na kuwezesha matunzo kwa watoto;

viii. Kuimarisha Mabaraza ya Wazee katika ngazi zote;

ix. Kuimarisha Kampeni ya kutokomeza ukatili dhidi ya wazee;

x. Kuimarisha ufuatiliaji wa utoaji wa huduma za ustawi wa jamii katika magereza, hospitali na shule;

xi. Kujenga Shule ya Maadilisho katika Mkoa wa Geita. Jumla ya **shilingi milioni 200** zimetengwa;

xii. Kuimarisha ujenzi wa mahabusu ya watoto katika mikoa ya Kigoma na Mtwara. Jumla ya **shilingi milioni 700** zimetengwa;

xiii. Kuwezesha Taasisi ya Ustawi wa Jamii kuboresha utoaji wa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko ili kukuza ujuzi wa wahitimu kwa ajili ya kupata uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa. Jumla ya **shilingi milioni 250** zimetengwa;

xiv. Kufungua campus ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii katika Chuo ya Ustawii wa Jamii Kisangara;

xv. Kuendelea kukarabati miundombinu na kuongeza miundombinu ili kukidhi mahitaji ya utoaji mafunzo katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii; na

xvi. Kuendelea kujenga uwezo wa rasilimaliwatu kwa kuwasomesha walimu katika kiwango cha shahada ya uzamivu (PhD).

**Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi**

**274.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kutoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali na kuwawezesha kushiriki ufugaji na kilimo cha mbogamboga;

ii. Kutokomeza ukatili wa kijinsia katika jamii. Jumla ya **shilingi milioni 827.95** zimetengwa;

iii. Kuratibu uanzishwaji wa Dawati la Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Kati; na

iv. Kuimarisha madawati ya Jinsia na Watoto kwenye Vituo vya Polisi, Jeshi la Magereza na TAKUKURU.

**Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

**275.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo na ustawi wa jamii kwa kutekeleza yafuatayo:-

i. Kufuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

ii. Kuimarisha usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

iii. Kuratibu mkutano wa mwaka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

iv. Kuandaa taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa; na

v. Kuimarisha utendaji wa wasajili wasaidizi katika ngazi ya Mkoa na Wilaya.

## H. SHUKRANI

**276.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika huduma za Afya, Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii.

**277. *Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Canada (DFATD), Denmark (DANIDA), na Ireland (Irish Aid), Uswisi (SDC), Korea Kusini (KOICA) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

**278. *Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru pia mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNAIDS, UNDP, UNFPA, UN-Women, WHO na IAEA); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU); Benki ya Maendeleo ya Afrika ($A_fDB$); GAVI; PEPFAR; CDC; USAID; PMI; Global Fund; Abbott Fund; DFID; EED; Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF); GIZ; Global Fund (for HIV, TB na Malaria); Bill and Melinda Gates Foundation; Good Samaritan Foundation (GSF); HelpAge International; John Snow Incorporation (JSI); JICA; KfW; Save the Children; World Vision; Benki ya STANBIC; na Walter REED.

**279.** ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na Benjamin Mkapa Foundation, AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, MEWATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Assosciation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, Kivulini, WiLDAF, TCRF na FSDT.

**280.** ***Mheshimiwa Spika,*** navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Aidha, nawashukuru

wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na maendeleo ya jamii, hususani katika mapambano dhidi ya Corona nchini.

**281.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, naomba kuwashukuru **Dkt. Zainabu Chaula** aliyekuwa Katibu Mkuu (Afya) na **Dkt John K. Jingu** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Muhammad Bakari Kambi**, aliyekuwa Mganga Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia wakurugenzi wakuu wa hospitali za Taifa na Kanda ambao ni **Prof. Lawrence M. Museru** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Dr. Respicious L. Boniface** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Prof. Mohamed Janabi** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dr. Julius Mwaiselage,** (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dr. Alphonce Chandika** (Hospitali ya Benjamin

Mkapa), **Dr. Riziki M. Kisonga** (Hospitali ya Kibong'oto), **Dr. Erasmus E. Mdeme** (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dr. Godlove Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Prof. Abel Makubi** (aliyekuwa Mkurugenzi wa Hospitali ya Bugando) na **Dr. Geleard Masenga** (Hospitali ya KCMC).

**282.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuwashukuru wakurugenzi na wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambazo ni MSD, NHIF, TMDA, NIMR, Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, TFNC, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa waendelee kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu.

**283.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza

majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Mkoa wetu.

## I. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2020/21

### Fungu 52 - Afya

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2020/21

**284.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha **shilingi 467,799,587,522.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 155,046,746,999** zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani (Makao Makuu ya Wizara, hospitali za rufaa za mikoa, Maalum, pamoja na mabaraza). Aidha, Mashirika yaliyo chini ya Wizara yanakadiriwa kukusanya **shilingi 312,752,840,523.** Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 21 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2019/20 ya kukusanya kiasi cha **shilingi 292,614,263,240**

## Matumizi ya Kawaida

285. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia **(Fungu 52)** imepanga kutumia kiasi cha **shilingi 900,088,240,000** ili iweze kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 539,128,874,000** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 58** ya bajeti ya Fungu 52, ambapo kiasi cha **shilingi 357,565,924,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake, na kiasi cha **shilingi 181,562,950,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## Miradi ya Maendeleo

286. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **shilingi 360,959,366,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 40** ya bajeti ya Fungu 52. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **shilingi 280,700,000,000** na fedha za nje ni **shilingi 80,259,366,000**

287. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2020/21 Wizara (Idara Kuu Afya - Fungu 52) inaomba jumla ya **Shilingi 900,088,240,000.**

## Fungu 53 - Maendeleo ya Jamii

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2020/21

**288.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara imekadiria kukusanya **shilingi 5,347,250,000** kutokana na ada na tozo mbalimbali za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mapato ya ada za mitihani na uuzaji wa mitaala ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii na mapato mengine.

### Matumizi ya Kawaida

**289.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **shilingi 26,491,375,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 12,842,081,000** ni Mishahara ya watumishi na **shilingi 13,649,294,000** ni Matumizi Mengineyo.

### Miradi ya Maendeleo

**290.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **shilingi 6,704,364,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 4,000,000,000** ni fedha za ndani na **shilingi 2,704,364,000** ni fedha za nje.

**291.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2020/21, Wizara (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii - Fungu 53) inaomba jumla ya **shilingi 33,195,739,000**

**292.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara kwa Mafungu yote (Fungu 52 na 53) ni **shilingi 933,283,979,000**

| Na. | Fungu | Matumizi ya Kawaida | Miradi ya Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fungu 52 | 539,128,874,000 | 360,959,366,000 | 900,088,240,000 |
| 2 | Fungu 53 | 26,491,375,000 | 6,704,364,000 | 33,195,739,000 |
| | **Jumla** | **565,620,249,000** | **367,663,730,000** | **933,283,979,000** |

**293.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto *www.moh.go.tz*. na *www.jamii.go.tz.*

**294.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**Kiambatisho Na. 1: Mashauri ya Migogoro ya Ndoa Yaliyoripotiwa na Kusuluhishwa**

| Na | Mkoa | 2018/19 | | | | 2019/20 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mashauri Yaliyosuluhishwa | Mashauri Yaliyopelekwa Mahakamani | Mashauri Yaliyoendelea Kufanyiwa Kazi | Jumla | Mashauri Yaliyosuluhishwa | Mashauri Yaliyopelekwa Mahakamani | Mashauri Yaliyoendelea Kufanyiwa Kazi | Jumla |
| 1 | Dar es Salaam | 1,652 | 293 | 193 | 2,138 | 1,584 | 316 | 1,268 | 3,168 |
| 2 | Kilimanjaro | 787 | 123 | 105 | 1,015 | 1,354 | 106 | 1,354 | 2,814 |
| 3 | Ruvuma | 453 | 56 | 57 | 566 | 348 | 101 | 247 | 696 |
| 4 | Singida | 323 | 39 | 64 | 426 | 827 | 142 | 685 | 1,654 |
| 5 | Kagera | 369 | 25 | 123 | 517 | 2,046 | 322 | 1,724 | 4,092 |
| 6 | Tanga | 558 | 36 | 39 | 633 | 248 | 25 | 223 | 496 |
| 7 | Geita | 472 | 20 | 39 | 531 | 522 | 78 | 444 | 1,044 |
| 8 | Simiyu | 269 | 19 | 30 | 318 | 415 | 155 | 260 | 830 |
| 9 | Morogoro | 518 | 55 | 66 | 639 | 907 | 144 | 763 | 1,814 |
| 10 | Dodoma | 597 | 46 | 23 | 666 | 170 | 67 | 103 | 340 |
| 11 | Mtwara | 431 | 43 | 50 | 524 | 337 | 118 | 219 | 674 |
| 12 | Mara | 592 | 95 | 105 | 792 | 899 | 411 | 488 | 1,798 |
| 13 | Mwanza | 747 | 83 | 76 | 906 | 1,116 | 169 | 947 | 2,232 |
| 14 | Tabora | 482 | 30 | 39 | 551 | 1,621 | 104 | 1,517 | 3,242 |
| 15 | Kigoma | 319 | 37 | 71 | 427 | 490 | 72 | 418 | 980 |
| 16 | Arusha | 926 | 101 | 32 | 1,059 | 908 | 316 | 592 | 1,816 |
| 17 | Manyara | 261 | 55 | 35 | 351 | 571 | 91 | 480 | 1,142 |
| 18 | Mbeya | 699 | 56 | 57 | 812 | 1,371 | 101 | 1,270 | 2,742 |
| 19 | Pwani | 711 | 62 | 37 | 810 | 735 | 198 | 537 | 1,470 |
| 20 | Lindi | 334 | 17 | 14 | 365 | 421 | 58 | 373 | 00 |
| 21 | Shinyanga | 441 | 26 | 21 | 488 | 646 | 9 | 637 | 1,292 |
| 22 | Iringa | 452 | 28 | 32 | 512 | 527 | 67 | 459 | 1,053 |
| 23 | Katavi | 436 | 23 | 27 | 486 | 234 | 17 | 217 | 468 |
| 24 | Njombe | 419 | 19 | 23 | 461 | 219 | 38 | 181 | 438 |
| 25 | Songwe | 402 | 14 | 18 | 434 | 500 | 144 | 356 | 1,000 |
| 26 | Rukwa | 386 | 9 | 14 | 409 | 256 | 95 | 161 | 512 |
| **Total** | | **14,035** | **1,410** | **1,387** | **16,832** | **19,272** | **3,464** | **15,923** | **38,659** |

**Chanzo:** *Ofisi ya Rais - TAMISEMI*

**Kiambatisho Na. 2: Watoto Waliopata Huduma kutoka kwa Wazazi wao kupitia Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa**

| Na. | Mkoa | Aina ya Mashauri Yaliyopokelewa | | | | Jumla | Mashauri Yaliyopelekwa Mahakamani | | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Watoto Ndani ya Ndoa | | Watoto Nje ya Ndoa | | | | | | |
| | | Me | Ke | Me | Ke | | Me | Ke | Jumla | |
| 1 | Arusha | 18 | 311 | 40 | 390 | 759 | 15 | 56 | 71 | 830 |
| 2 | Dar es Salaam | 336 | 607 | 434 | 590 | 1,967 | 157 | 176 | 333 | 2,300 |
| 3 | Dodoma | 57 | 8 | 81 | 89 | 235 | 12 | 29 | 41 | 276 |
| 4 | Geita | 36 | 65 | 1 | 14 | 116 | 2 | 13 | 15 | 131 |
| 5 | Iringa | 1199 | 73 | 183 | 256 | 1,711 | 23 | 0 | 23 | 1,734 |
| 6 | Kagera | 22 | 237 | 37 | 42 | 338 | 15 | 24 | 39 | 377 |
| 7 | Katavi | 4 | 132 | 18 | 42 | 196 | 0 | 0 | 0 | 196 |
| 8 | Kigoma | 18 | 193 | 44 | 100 | 355 | 3 | 32 | 35 | 390 |
| 9 | Kilimanjaro | 36 | 231 | 53 | 69 | 389 | 2 | 17 | 19 | 408 |
| 10 | Lindi | 34 | 245 | 69 | 105 | 453 | 7 | 11 | 18 | 471 |
| 11 | Manyara | 22 | 112 | 24 | 28 | 186 | 10 | 34 | 44 | 230 |
| 12 | Mara | 34 | 117 | 36 | 87 | 274 | 4 | 29 | 33 | 307 |
| 13 | Mbeya | 9 | 358 | 18 | 112 | 497 | 0 | 9 | 9 | 506 |
| 14 | Mwanza | 0 | 0 | 0 | 0 | - | 0 | 0 | 0 | - |
| 15 | Morogoro | 60 | 350 | 58 | 114 | 582 | 5 | 35 | 40 | 622 |
| 16 | Mtwara | 36 | 18 | 96 | 114 | 264 | 26 | 11 | 37 | 301 |
| 17 | Njombe | 29 | 152 | 13 | 14 | 208 | 23 | 5 | 28 | 236 |
| 18 | Pwani | 123 | 338 | 68 | 132 | 661 | 0 | 36 | 36 | 697 |
| 19 | Rukwa | 0 | 113 | 0 | 2 | 115 | 0 | 0 | 0 | 115 |
| 20 | Ruvuma | 116 | 255 | 52 | 99 | 522 | 27 | 29 | 56 | 578 |
| 21 | Simiyu | 38 | 103 | 57 | 56 | 254 | 13 | 19 | 32 | 286 |
| 22 | Shinyanga | 81 | 171 | 48 | 72 | 372 | 5 | 18 | 23 | 395 |
| 23 | Singida | 109 | 138 | 80 | 97 | 424 | 29 | 40 | 69 | 493 |
| 24 | Songwe | 122 | 133 | 139 | 272 | 666 | 32 | 39 | 71 | 737 |
| 25 | Tabora | 22 | 214 | 8 | 26 | 270 | 13 | 24 | 37 | 307 |
| 26 | Tanga | 0 | 143 | 0 | 111 | 254 | 0 | 23 | 23 | 277 |
| **Jumla Kuu** | | **2,561** | **4,817** | **1,657** | **3,033** | **12,068** | **423** | **709** | **1,132** | **13,200** |

**Chanzo:** *Ofisi ya Rais – TAMISEMI*

**Kiambatisho Na. 3: Idadi ya Mabaraza ya Wazee Yaliyoanzishwa**

| Na. | Mkoa | Mkoa | Halmashauri | Kata | Kijiji/Mtaa | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dar es Salaam | 1 | 5 | 98 | 532 | 636 |
| 2 | Arusha | 1 | 5 | 145 | 322 | 473 |
| 3 | Dodoma | - | 2 | 138 | 571 | 711 |
| 4 | Iringa | - | 3 | 61 | - | 64 |
| 5 | Kagera | - | 4 | 148 | 580 | 732 |
| 6 | Kigoma | 1 | 8 | 139 | 486 | 634 |
| 7 | Kilimanjaro | - | 7 | 166 | 596 | 769 |
| 8 | Mbeya | 1 | 2 | 89 | 280 | 372 |
| 9 | Mwanza | - | 4 | 125 | 380 | 509 |
| 10 | Morogoro | - | 6 | 496 | 569 | 1,071 |
| 11 | Mara | - | 5 | 83 | 316 | 404 |
| 12 | Pwani | - | 3 | 114 | 321 | 438 |
| 13 | Ruvuma | 1 | 8 | 171 | 617 | 797 |
| 14 | Rukwa | - | 1 | 32 | 59 | 92 |
| 15 | Shinyanga | 1 | 6 | 118 | 483 | 608 |
| 16 | Tanga | - | 2 | 245 | 1,035 | 1,282 |
| 17 | Tabora | 1 | 8 | 206 | 802 | 1,017 |
| 18 | Singida | - | 6 | 95 | 341 | 442 |
| 19 | Manyara | - | 3 | 66 | 254 | 323 |
| 20 | Geita | - | 4 | 118 | 521 | 643 |
| 21 | Simiyu | - | 2 | 133 | 30 | 165 |
| 22 | Njombe | - | - | 112 | 112 | 224 |
| 23 | Katavi | 1 | 5 | 58 | 212 | 276 |
| 24 | Songwe | - | 3 | 59 | 199 | 261 |
| 25 | Lindi | 1 | 6 | 112 | 365 | 484 |
| 26 | Mtwara | 1 | 9 | 153 | 835 | 998 |
| **Jumla** | | **10** | **117** | **3,480** | **10,818** | **14,425** |

**Chanzo:** *Ofisi ya Rais – TAMISEMI*

**Kiambatisho Na. 4: Wazee Walio katika Makazi ya Wazee ya Serikali**

| Na. | Mkoa | Jina la Makazi | 2016/17 | | | 2017/18 | | | 2018/19 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla |
| 1 | Kigoma | Kibirizi | 21 | 23 | 44 | 27 | 19 | 46 | 25 | 16 | 41 | 18 | 12 | **30** |
| 2 | Kilimanjaro | Njoro | 11 | 6 | 17 | 11 | 7 | 18 | 14 | 6 | 20 | 13 | 6 | **19** |
| 3 | Shinyanga | Kolandoto | 10 | 7 | 17 | 9 | 8 | 17 | 11 | 9 | 20 | 12 | 5 | **17** |
| 4 | Ruvuma | Ngehe | 18 | 23 | 41 | 15 | 23 | 38 | 13 | 17 | 30 | 0 | 0 | **0** |
| 5 | Mwanza | Bukumbi | 25 | 43 | 68 | 28 | 65 | 93 | 27 | 60 | 87 | 21 | 46 | **67** |
| 6 | Tabora | Ipuli | 12 | 13 | 25 | 17 | 16 | 33 | 22 | 15 | 37 | 14 | 16 | **30** |
| 7 | Morogoro | Fungafunga | 15 | 4 | 19 | 14 | 3 | 17 | 14 | 4 | 18 | 19 | 6 | **25** |
| 8 | Morogoro | Chazi | 10 | 7 | 17 | 11 | 7 | 18 | 10 | 7 | 17 | 0 | 0 | **0** |
| 9 | Tanga | Mwanzange | 24 | 9 | 33 | 23 | 9 | 32 | 26 | 7 | 33 | 22 | 8 | **30** |
| 10 | Tanga | Msufini | 15 | 6 | 21 | 17 | 6 | 23 | 18 | 7 | 25 | 16 | 6 | **22** |
| 11 | Dar es Salaam | Nunge | 9 | 6 | 15 | 11 | 8 | 19 | 13 | 8 | 21 | 17 | 10 | **27** |
| 12 | Mara | Nyabange | 14 | 14 | 28 | 17 | 19 | 36 | 19 | 19 | 38 | 17 | 21 | **38** |
| 13 | Kagera | Kilima | 13 | 6 | 19 | 14 | 4 | 18 | 13 | 6 | 19 | 12 | 6 | **18** |
| 14 | Singida | Sukamahela | 20 | 21 | 41 | 23 | 21 | 44 | 23 | 22 | 45 | 12 | 5 | **17** |
| 15 | Arusha | Magugu | 10 | 3 | 13 | 11 | 4 | 15 | 9 | 3 | 12 | 7 | 2 | **9** |
| 16 | Lindi | Nandanga | 11 | 16 | 27 | 13 | 14 | 27 | 13 | 13 | 26 | 0 | 0 | **0** |
| 17 | Mtwara | Nkaseka | | | | 6 | 14 | 20 | 6 | 15 | 21 | 0 | 0 | **0** |
| **Jumla** | | | **238** | **207** | **445** | **267** | **247** | **514** | **276** | **234** | **510** | **200** | **149** | **349** |

**Chanzo:** *Makazi ya Wazee Yanayomilikiwa na Serikali*

**Kiambatisho Na. 5: Wazee Walio katika Makazi ya Wazee ya Taasisi Binafsi**

| Na. | Mkoa | Jina la Makazi | 2018/19 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla |
| 1 | Kagera | Nyumba ya huruma | 0 | 12 | 12 | 0 | 0 | 0 |
| | | Missionary of Charty | | | 0 | 5 | 0 | 5 |
| | | Igabiro | | | 0 | 2 | 5 | 7 |
| 2 | Lindi | Rasbura | 6 | 9 | 15 | 1 | 1 | 2 |
| 3 | Njombe | KKKT - DKU Kibena | 0 | 5 | 5 | 0 | 6 | 6 |
| 4 | D ar es Salaam | Mburahati | 10 | 32 | 42 | 0 | 0 | 0 |
| | | Msimbazi | 5 | 5 | 10 | 5 | 5 | 10 |
| | | Nyumba ya Imani na Furaha | | | 0 | 30 | 14 | 44 |
| 5 | Tabora | Gongoni (RC) | 22 | 21 | 43 | 21 | 22 | 43 |
| | | Iduguta (FPCT) | 4 | 10 | 14 | 4 | 10 | 14 |
| | | Morovian Sikonge | | | 0 | 5 | 3 | 8 |
| 6 | Morogoro | Ikombo | 0 | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 |
| | | Nazareth | 67 | 19 | 86 | 66 | 22 | 88 |
| 7 | Dodoma | Joy and Love (missionary charity Hombolo) | 35 | 42 | 77 | 23 | 41 | 64 |
| | | Upendo brothers | 38 | 0 | 38 | 0 | 24 | 24 |
| 8 | Tanga | Kasosora | 3 | 3 | 6 | 4 | 3 | 7 |
| 9 | Pwani | Kindwiti | 21 | 15 | 36 | 8 | 7 | 15 |
| 10 | Mara | Mji wa Huruma | | | 0 | 29 | 47 | 76 |
| 11 | Shinyanga | Busanda | 0 | | 0 | 13 | 25 | 38 |
| **Jumla** | | | **212** | **171** | **383** | **216** | **235** | **451** |

**Chanzo:** *Makazi ya Wazee ya Taasisi Binafsi*

**Kiambatisho Na. 6: Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

| Mwaka | Ngazi ya Usajili | | | | | | | | Jumla | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wilaya | | Mkoa | | Taifa | | Kimataifa | | | | |
| | Cheti | Cheti cha Ukubalifu | Cheti | Cheti cha Ukubalifu | Cheti | Cheti cha Ukubalifu | Cheti | Cheti cha Ukubalifu | Cheti | Ukubalifu | |
| 2005 | 40 | 7 | 18 | 4 | 183 | 112 | 16 | 24 | 257 | 147 | 404 |
| 2006 | 183 | 13 | 113 | 24 | 338 | 131 | 21 | 13 | 655 | 181 | 836 |
| 2007 | 119 | 17 | 97 | 30 | 389 | 99 | 20 | 7 | 625 | 153 | 778 |
| 2008 | 157 | 10 | 86 | 6 | 481 | 96 | 25 | 7 | 749 | 119 | 868 |
| 2009 | 103 | 8 | 48 | 3 | 503 | 83 | 21 | 1 | 675 | 95 | 770 |
| 2010 | 62 | 1 | 29 | 0 | 416 | 25 | 12 | 2 | 519 | 28 | 547 |
| 2011 | 81 | 1 | 49 | 3 | 574 | 30 | 26 | 4 | 730 | 38 | 768 |
| 2012 | 61 | 0 | 45 | 2 | 530 | 31 | 20 | 3 | 656 | 36 | 692 |
| 2013 | 38 | 1 | 35 | 2 | 497 | 22 | 21 | 1 | 591 | 26 | 617 |
| 2014 | 36 | 4 | 22 | 1 | 511 | 13 | 26 | 0 | 595 | 18 | 613 |
| 2015 | 63 | 0 | 23 | 0 | 460 | 0 | 38 | 0 | 584 | 0 | 584 |
| 2016 | 57 | 0 | 16 | 0 | 464 | 0 | 33 | 0 | 570 | 0 | 570 |
| 2017 | 27 | 0 | 2 | 0 | 325 | 0 | 31 | 0 | 385 | 0 | 385 |
| 2018 | 13 | 0 | 4 | 0 | 458 | 4 | 37 | 0 | 512 | 4 | 516 |
| 2019 | 9 | 0 | 9 | 0 | 1,251 | 1 | 133 | 0 | 1,402 | 1 | 1,403 |
| 2020 | 0 | 0 | 1 | 0 | 86 | 0 | 8 | 0 | 95 | 0 | 95 |
| **Jumla** | **1,049** | **62** | **597** | **75** | **7,466** | **647** | **488** | **62** | **9,600** | **846** | **10,446** |

**Chanzo:** *WAMJW*

## Kiambatisho Na. 7: Maafisa Maendeleo ya Jamii Walioajiriwa katika ngazi ya Halmashauri

| Na. | Mkoa | Mkoa | | | Halmashauri | | | Kata | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | Mahitaji | Waliopo | Upungufu |
| 1 | Simiyu | 2 | 2 | 0 | 39 | 39 | 0 | 133 | 19 | 114 | 174 | 60 | 114 |
| 2 | Dodoma | 2 | 2 | 0 | 54 | 54 | 0 | 209 | 64 | 145 | 265 | 120 | 145 |
| 3 | Kigoma | 2 | 1 | 1 | 47 | 47 | 0 | 139 | 26 | 113 | 188 | 74 | 114 |
| 4 | Lindi | 2 | 2 | 0 | 71 | 71 | 0 | 150 | 6 | 144 | 223 | 79 | 144 |
| 5 | Rukwa | 2 | 2 | 0 | 28 | 28 | 0 | 99 | 21 | 78 | 129 | 51 | 78 |
| 6 | Ruvuma | 2 | 1 | 1 | 54 | 54 | 0 | 173 | 79 | 94 | 229 | 134 | 95 |
| 7 | Manyara | 2 | 1 | 1 | 58 | 58 | 0 | 142 | 43 | 99 | 202 | 102 | 100 |
| 8 | Mbeya | 2 | 2 | 0 | 55 | 55 | 0 | 181 | 91 | 90 | 238 | 148 | 90 |
| 9 | Mara | 2 | 1 | 1 | 38 | 67 | -29 | 177 | 38 | 139 | 217 | 106 | 111 |
| 10 | Kilimanjaro | 3 | 3 | 0 | 61 | 61 | 0 | 170 | 113 | 57 | 234 | 177 | 57 |
| 11 | Geita | 2 | 2 | 0 | 41 | 41 | 0 | 122 | 51 | 71 | 165 | 94 | 71 |
| 12 | Pwani | 2 | 2 | 0 | 74 | 74 | 0 | 136 | 74 | 62 | 212 | 150 | 62 |
| 13 | Iringa | 4 | 4 | 0 | 45 | 45 | 0 | 107 | 74 | 33 | 156 | 123 | 33 |
| 14 | Katavi | 2 | 2 | 0 | 21 | 21 | 0 | 58 | 30 | 28 | 81 | 53 | 28 |
| 15 | Songwe | 2 | 1 | 1 | 44 | 44 | 0 | 93 | 14 | 79 | 139 | 59 | 80 |
| 16 | Singida | 2 | 2 | 0 | 68 | 68 | 0 | 133 | 43 | 90 | 203 | 113 | 90 |
| 17 | Arusha | 2 | 2 | 0 | 49 | 49 | 0 | 158 | 90 | 68 | 209 | 141 | 68 |
| 18 | Dar es Salaam | 2 | 2 | 0 | 60 | 59 | 1 | 102 | 115 | -13 | 164 | 176 | -12 |
| 19 | Mwanza | 2 | 1 | 1 | 82 | 82 | 0 | 193 | 53 | 140 | 277 | 136 | 141 |
| 20 | Kagera | 2 | 2 | 0 | 70 | 70 | 0 | 190 | 48 | 142 | 262 | 120 | 142 |
| 21 | Njombe | 2 | 1 | 1 | 49 | 55 | -6 | 107 | 62 | 45 | 158 | 118 | 40 |
| 22 | Tanga | 2 | 2 | 0 | 75 | 75 | 0 | 251 | 109 | 142 | 328 | 186 | 142 |
| 23 | Morogoro | 2 | 2 | 0 | 89 | 89 | 0 | 205 | 94 | 111 | 296 | 185 | 111 |
| 25 | Tabora | 2 | 2 | 0 | 48 | 45 | 3 | 198 | 27 | 171 | 248 | 74 | 174 |
| 25 | Mtwara | 2 | 2 | 0 | 62 | 62 | 0 | 189 | 23 | 166 | 253 | 87 | 166 |
| 26 | Shinyanga | 2 | 2 | 0 | 46 | 46 | 0 | 130 | 69 | 61 | 178 | 117 | 61 |
| Jumla | | **55** | **48** | **7** | **1,428** | **1,459** | **-31** | **3,945** | **1,476** | **2,469** | **5,428** | **2,983** | **2,445** |

**Chanzo:** *Ofisi ya Rais - TAMISEMI*

**Kiambatisho Na. 8: Idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii**

| Na. | Eneo | Mahitaji | Waliopo | Upungufu | Asilimia ya Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Regional Secretariat (RS) | 26 | 26 | 0 | 0 |
| 2 | Regional Hospitals | 105 | 35 | 70 | 67 |
| 3 | Halmashauri (Makao Makuu) | 184 | 184 | 0 | 0 |
| 4 | Halmashauri (Idara/Kitengo) | 1,472 | 129 | 1343 | 91 |
| 5 | Hospital za Wilaya | 905 | 104 | 801 | 89 |
| 6 | Kata | 4,420 | 171 | 4249 | 96 |
| 7 | Mitaa | 4,037 | 91 | 3946 | 98 |
| 8 | Vijiji | 12,545 | 0 | 12545 | 100 |
| **Jumla** | | **23,694** | **740** | **22,954** | **97** |

**Chanzo:** *Ofisi ya Rais - TAMISEMI*




*Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt. Faustine Ndugulile (Mb) akikabidhi mifuko 50 ya saruji kwa uongozi wa Shule ya Sekondari Utengule iliyopo Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kumalizia vyumba tisa vya madarasa katika jitihada za kuunga mkono nguvu za wananchi kwenye ujenzi wa madarasa tarehe 14 Januari,*



*Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt. Faustine Ndugulile (Mb) akioneshwa mti wa maparachichi na mmoja wa mkulima aliyefaidika na uhamasishaji wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba Mzee Mbedule wakati alipofanya ziara kujionea utendaji wa Chuo hicho tarehe 7 Januari, 2020.*